**ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI**
**ZANZIBAR**
**MHE. PANDU AMEIR KIFICHO - SPIKA**

| | |
|---|---|
| 1.Mhe. Balozi Seif Ali Iddi | MBM/Makamo wa Pili wa Rais/Kuteuliwa na Rais |
| 2.Mhe. Dr. Mwinyihaji Makame Mwadini | MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi/Jimbo la Dimani. |
| 3.Mhe. Omar Yussuf Mzee | MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo/ Kuteuliwa na Rais |
| 4.Mhe. Haji Omar Kheri | MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora/Jimbo la Tumbatu |
| 5.Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji | MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais/Kuteuliwa |
| 6.Mhe. Mohammed Aboud Mohammed | MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Pili wa Rais/Kuteuliwa |
| 7.Mhe. Abubakar Khamis Bakary | MBM/Waziri wa Katiba na Sheria/Jimbo la Mgogoni. |
| 8.Mhe. Hamad Masoud Hamad | MBM/Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Ole. |
| 9.Mhe. Ali Juma Shamuhuna | MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Donge |
| 10.Mhe. Juma Duni Haji | MBM/Waziri wa Afya/ Kuteuliwa na Rais |
| 11.Mhe. Zainab Omar Mohammed | MBM/Waziri wa Ustawi wa Jamii, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto/Kuteuliwa |
| 12.Mhe. Said Ali Mbarouk | MBM/Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo/Jimbo la Gando |
| 13.Mhe. Ramadhan Abdalla Shaaban | MBM/Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/Kuteuliwa. |
| 14.Mhe. Suleiman Othman Nyanga | MBM/Waziri wa Kilimo na Maliasili/Jimbo la Jang'ombe |

| | |
|---|---|
| 15.Mhe. Nassor Ahmed Mazrui | MBM/Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Mtoni |
| 16.Mhe. Abdillah Jihad Hassan | MBM/Waziri wa Mifugo na Uvuvi/Jimbo la Magogoni |
| 17.Mhe. Haroun Ali Suleiman | MBM/Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika/Jimbo la Makunduchi |
| 18.Mhe. Mansoor Yussuf Himid | MBM/Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Kiembesamaki |
| 19. Mhe. Haji Faki Shaali | MBM/ Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Mkanyageni |
| 20.Mhe. Machano Othman Said | MBM/Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Chumbuni. |
| 21.Mhe. Othman Masoud Othman | Mwanasheria Mkuu |
| 22.Mhe. Issa Haji Ussi | Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Chwaka |
| 23.Mhe. Zahra Ali Hamad | Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Nafasi za Wanawake |
| 24.Mhe. Dr. Sira Ubwa Mamboya | Naibu Waziri wa Afya/ Kuteuliwa na Rais |
| 25.Mhe. Bihindi Hamad Khamis | Naibu Waziri wa Habari,Utamaduni, Utalii na Michezo/ Nafasi za Wanawake |
| 26.Mhe. Haji Mwadini Makame | Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/Jimbo la Nungwi |
| 27.Mhe. Thuwaybah Edington Kissasi | Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Fuoni |
| 28.Mhe. Abdalla Juma Abdalla | Jimbo la Chonga |
| 29.Mhe. Abdalla Moh'd Ali | Jimbo la Mkoani |
| 30.Mhe. Abdi Mosi Kombo | Jimbo la Matemwe |
| 31.Mhe. Ali Mzee Ali | Kuteuliwa na Rais |
| 32.Mhe. Ali Abdalla Ali | Jimbo la Mfenesini |
| 33. Mhe. Ali Salum Haji | Jimbo la Kwahani |

| | |
|---|---|
| 34.Mhe. Amina Iddi Mabrouk | Nafasi za Wanawake |
| 35. Mhe. Asaa Othman Hamad | Jimbo la Wete |
| 36.Mhe. Asha Abdu Haji | Nafasi za Wanawake |
| 37.Mhe. Asha Bakari Makame | Nafasi za Wanawake |
| 38.Mhe. Ashura Sharif Ali | Nafasi za Wanawake |
| 39.Mhe. Bikame Yussuf Hamad | Nafasi za Wanawake |
| 40.Mhe. Farida Amour Mohammed | Nafasi za Wanawake |
| 41.Mhe. Fatma Mbarouk Said | Jimbo la Amani |
| 42.Mhe. Hamza Hassan Juma | Jimbo la Kwamtipura |
| 43.Mhe. Hassan Hamad Omar | Jimbo la Kojani |
| 44.Mhe. Hija Hassan Hija | Jimbo la Kiwani |
| 45.Mhe. Ismail Jussa Ladhu | Jimbo la Mji Mkongwe |
| 46.Mhe. Jaku Hashim Ayoub | Jimbo la Muyuni |
| 47.Mhe. Kazija Khamis Kona | Nafasi za Wanawake |
| 48.Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa | Jimbo la Kikwajuni |
| 49.Mhe. Makame Mshimba Mbarouk | Jimbo la Kitope |
| 50.Mhe. Marina Joel Thomas | Kuteuliwa na Rais |
| 51.Mhe. Mbarouk Wadi Mussa | Jimbo la Mkwajuni |
| 52.Mhe. Mgeni Hassan Juma | Nafasi za Wanawake |
| 53.Mhe. Mlinde Mbarouk Juma | Jimbo la Bumbwini |
| 54.Mhe. Mohammed Haji Khalid | Jimbo la Mtambile |
| 55.Mhe. Mohamedraza Hassanali Mohamedali | Jimbo la Uzini |
| 56.Mhe. Mohammed Mbwana Hamad | Jimbo la Chambani |
| 57.Mhe. Mohammed Said Mohammed | Jimbo la Mpendae |
| 58.Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak | Nafasi za Wanawake |
| 59.Mhe. Mussa Ali Hassan | Jimbo la Koani |
| 60.Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa | Nafasi za Wanawake |

| | |
|---|---|
| 61.Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi | Nafasi za Wanawake |
| 62.Mhe. Nassor Salim Ali | Jimbo la Rahaleo |
| 63.Mhe. Omar Ali Shehe | Jimbo la Chake-Chake |
| 64.Mhe. Panya Ali Abdalla | Nafasi za Wanawake |
| 65.Mhe. Rashid Seif Suleiman | Jimbo la Ziwani |
| 66.Mhe. Raya Suleiman Hamad | Nafasi za Wanawake |
| 67.Mhe. Rufai Said Rufai | Jimbo la Tumbe |
| 68.Mhe. Saleh Nassor Juma | Jimbo la Wawi |
| 69.Mhe. Salim Abdalla Hamad | Jimbo la Mtambwe |
| 70.Mhe. Salma Mohammed Ali | Nafasi za Wanawake |
| 71.Mhe. Salma Mussa Bilali | Nafasi za Wanawake |
| 72.Mhe. Salmin Awadh Salmin | Jimbo la Magomeni |
| 73.Mhe. Shadya Mohamed Suleiman | Nafasi za Wanawake |
| 74.Mhe. Shamsi Vuai Nahodha | Jimbo la Mwanakwerekwe |
| 75.Mhe. Shawana Bukheti Hassan | Jimbo la Dole |
| 76.Mhe. Subeit Khamis Faki | Jimbo la Micheweni |
| 77.Mhe. Suleiman Hemed Khamis | Jimbo la Konde |
| 78.Mhe. Ussi Jecha Simai | Jimbo la Chaani |
| 79.Mhe. Viwe Khamis Abdalla | Nafasi za Wanawake |
| 80.Mhe. Wanu Hafidh Ameir | Nafasi za Wanawake |

**Ndugu Yahya Khamis Hamad** **Katibu wa Baraza la Wawakilishi**

**Kikao cha Kumi – Tarehe 28 Juni, 2012**

*(Kikao kilianza saa 3.00 asubuhi)*

**Dua**

*Mhe. Spika (Pandu Ameir Kificho) alisoma Dua*

**MASWALI NA MAJIBU**

**Nam. 130**

**Kitengo cha Kudhibiti Uingiaji wa Dawa za Kulevya**

*(Mhe. Mjumbe aliyetaka kuuliza swali hili ameliondoa)*

**Nam. 89**

**Kukosekana kwa Mahabusu za watoto Zanzibar**

**Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Aliuliza:**

Tanzania imesaini Mkataba wa Umoja wa Mataifa wa Haki za Mtoto na Zanzibar ikiwa ni miongoni mwa nchi mbili za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

a) Kwa nini watoto wenye umri wa chini ya miaka 18 wanaendelea kuhifadhiwa katika mahabusu za magereza kwa kuchanganywa na watu wazima.

b) Kwa kuwa ripoti ya Tume ya Haki za Binaadamu na Utawala Bra ya mwaka 2008/2009 imetaka tatizo hilo liondolewe kwa nini watoto wanaendelea kuchanganywa hadi sasa magerezani.

c) Je, Serikali ya Mapinduzi Zanzibar inalinda vipi haki za watoto katika mazingira kama hayo licha ya Sheria ya kulinda haki za watoto kupitishwa na Baraza la Wawakilishi Zanzibar.

d) Kutokana na tatizo hilo kuendelea kufanyika Je, Serikali haioni kuwa tunatunga sheria lakini tunashindwa kuzitekeleza.

**Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Alijibu:**

Mhe. Spika, naomba kumjibu Mhe. Jaku Hashim Ayoub wa Jimbo la Muyuni swali lake nambari 89 kama hivi ifuatavyo:

Mhe. Spika, kwanza naomba nimpongeze sana Mhe. Jaku kwa ufatiliaji wake mzuri wa haki za binaadam na hasa kwa shughuli za Chuo cha Mafunzo naomba atambue kwamba ni Chuo cha Mafunzo na sio magereza. Kile ni Chuo wale wanaofanya makosa tunawapa mafunzo wawe raia wema. Hili neno gereza katika Serikali ya Mapinduzi Zanzibar tumelifuta. Kwa hivyo nakuomba Mhe. Ayoub na wewe tusaidie kwa nia yako nzuri tu kuwaendeleza hao wanafunzi wa Chuo cha Mafunzo.

Sasa naomba nimjibu kwa pamoja kwa sababu haya masuala ukiyaangalia yote yanaingiliana.

Mhe. Spika, Serikali imeipa umuhimu mkubwa suala la haki za watoto kama inavyojionesha katika sheria mbali mbali ambazo tumezitunga. Hivi sasa utaratibu umewekwa katika Vyuo vya Mafunzo kuwatenganisha watoto na watu wazima. Tukisema watoto ni chini ya miaka 18 na kwa hivi sasa Mhe. Spika, watoto waliopo katika Chuo cha Mafunzo hapo Makao Makuu ni 5 tu na wametengewa sehemu yao maalum, sehemu ile iliyokuwa ya kinamama.

Labda atauliza kinamama wamepelekwa wapi? Kinamama nao wamepelekwa katika eneo lililokuwa la Bamkwe, ninafikiri Mhe. Ayoub atakumbuka hili jina maarufu Bamkwe. Kwa mipango ya baadae Mhe. Spika, Serikali tayari tumeanza mchakato wa ujenzi wa Chuo kipya cha Mafunzo huko Hanyegwa mchana ambapo patakuwepo na chuo pekee cha watoto ambacho kitakuwa na huduma zote zinazostahiki haki za watoto.

**Mhe. Jaku Hashim Ayoub:** Mhe. Spika, ahsante sana pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri je, hichi Chuo kinachotaka kujengwa huko Hanyegwa mchana tuna hakika kitakuwa ni cha watoto tu bila kuchanganyika na wanafunzi wengine. Na lini kitamalizika na kitachukuwa wanafunzi wangapi?

**Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi** Alijibu**:**

Mhe. Spika, naomba kumjibu Mhe. Jaku Hashim swali lake la nyongeza kama hivi ifuatavyo:

Mhe. Spika, hichi Chuo kipya cha Hanyegwa mchana tunakitarajia kiwe na uwezo wa kuchukua wanafunzi 1300 kati ya hao 1000 ni wanaume na 300 wanawake. Na tayari michor imeshaonesha sehemu maalum ambayo imetangwa kwa kuwekea watoto. Watoto kabisa hawatokuwa katika sehemu za watu wazima.

**Nam. 116**

**Ukosefu wa Huduma ya Umeme Kijini na Mbuyutende**

**Mhe. Abdi Mosi Kombo Aliuliza:**

Hivi sasa dunia nzima inapigania maendele na hasa katika Nishati ya Umeme. Katika Jimbo la Matemwe sehemu ya Kaskazini kama vile vijiji vya Kijini, Mbuyu tende, kwa muda mrefu sana vijiji hivi vimekosa maendeleo hayo.

Je, Serikali kupitia Wizara husika itawafikiria vipi wananchi hawa kuwapatia umeme.

**Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati Alijibu:**

Mhe. Spika, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake namba 115 kama hivi ifuatavyo:-

Mhe. Spika, Wizara yangu kupitia Shirika la Umeme limeweka mpango endelevu wa kuhakikisha vijiji vyote vya Unguja na Pemba vinapatiwa huduma hiyo ya umeme. Lakini kutokana na uhaba wa fedha ndio maana utekelezaji wake unakwenda kwa awamu. Kwa hivi sasa tayari kijiji cha Mikunguni cha Matemwe kinaendelea na kazi ya kuvutiwa umeme.

**Mhe. Kazija Khamis Kona:** Ahsante Mhe. Spika, kwa kunipa fursa ya kumuuliza Mhe. Naibu Waziri swali la nyongeza. Mhe. Naibu Waziri unasema kwa kijiji cha Mikunguni kiko karibu kufanyiwa utaratibu, lakini je, Mhe. Waziri kwa kuwa jimbo la Matemwe lina shehia nyingi hazijafanikiwa kupata nishati hiyo ya umeme, mfano Kandwi, Kijini na MK. Je, Mhe. Waziri ni lini Wizara yako itashughulikia vijiji hivi ili vipate nishati hiyo ya umeme na wananchi wale wafaidike na maendeleo ya nchi hii.

**Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati:** Ahsante Mhe. Spika, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza kama hivi ifuatavyo:

Mhe. Spika, kama nilivyosema hapo awali kwamba kinachozuia kwa sasa hivi ni upungufu wa fedha ndani ya Shirika hilo, lakini hali ya fedha itakaporuhusu basi vijiji vyote hivyo vitapatiwa huduma hiyo. Lengo la Serikali ya Mapinduzi Zanzibar ni kuvisambazia vijiji vyote ambavyo havina umeme kuvipatia huduma muhimu hiyo ya umeme.

**Mhe. Mohammed Said Mohammed:** Ahsante sana Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi hii asubuhi hii ya leo. Kwanza nimpongeze Mhe. Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri na kwa kuwa vijiji vingi vimepata umeme hapa Zanzibar, lakini nina swali dogo la nyongeza.

Mhe. Naibu Waziri katika kijiji cha Donge meli 20 kimefanyiwa utafiti na kupata nguzo 10 lakini mpaka leo hazijapelekwa nguzo zile wala kupatiwa umeme. Je, ni lini Wizara yako itapeleka umeme katika kijiji kile ili wananchi wale wawe na imani na nchi yao.

**Mhe. Spika:** Mheshimiwa swali liko nje ya swali mama. Kama majibu yapo saidia.

**Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati:** Ahsante Mhe. Spika, ingawa swali lake liko nje ya swali mama, lakini niseme kwamba wananchi hao wavute subira, lengo la Shirika la Umeme ni kuwasambazia wananchi huduma hiyo. Lakini kwa sasa hivi kidogo tu kwamba tuna upungufu wa nguzo ambazo kwa sasa hivi ziko njiani zinakuja, lakini Serikali nguzo zimetupungukia pamoja na waya, lakini utakapofika waya huo pamoja na nguzo naomba Mhe. Mwakilishi tukumbushane na tuonane tutaishughulikia kazi yako.

**Mhe. Abdalla Mohammed Ali:** Ahsante Mhe. Spika, naomba niulize swali dogo tu la nyongeza. Mhe. Naibu Waziri katika majibu yako umetueleza kuwa kuna mpango wa kuvipatia vijiji yaani mpango mkuu wa taifa. Na sisi wawakilishi tuna mfuko wetu wa maendeleo ambao katika kupeleka maendeleo huwa tunatizama pia suala la umeme. Sijui unaweza kutueleza ni vijiji vipi ambavyo mmeviweka na mmevipanga kuvipatia umeme kwa mwaka huu unafuata.

**Mhe. Spika:** Mheshimiwa na hilo pia saidia kama ulivyosaidia mwanzo.

**Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati:** Ahsante Mhe. Spika, kwa sasa hivi hatujajipangia kijiji fulani na fulani, kwa sababu ili tupate kueneza umeme vijijini ni kwamba tunasubiri bajeti yetu ipite. Kwa sababu tumeshaliingiza hili suala la kusambaza umeme vijijini, kwa hivyo bado hatujajipangia kijiji fulani na kijiji fulani. Lakini pamoja na hayo Wawakilishi ningewaomba kwamba na wanapolielekeza suala hili la umeme kijijini mwao basi wake tuonane Wizara yangu kupitia Shirika la Umeme iko tayari kushirikiana na kuwasaidia nguzo nusu ya hizo nguzo wanazozihitajia kwenye vijiji vyao. Kwa hivyo ningewaomba waje tushirikiane na nitajitahidi kuwamalizia huduma hiyo.

**Nam. 66**

**Usalama wa Barabara Pete**

**Mhe. Jaku Hashim Ayoub Aliuliza:**

Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, imekuwa ikichukua hatua mbali mbali kujenga barabara, lakini barabara hizo zimeanza kuwa hatarishi kwa watembea kwa miguu wakiwemo watoto hasa katika barabara ya Pete ambayo tayari imesababisha kifo cha mtoto mmoja.

a) Je, Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano ina mpango gani wa kuweka matuta kupunguza ajali katika barabara hiyo.

b) J, kwa nini uwekaji wa matuta hauzingatiwi wakati wa ujenzi wa barabara na badala yake husubiri kukamilika kwa ujenzi huo.

c) Ni ajali ngapi zimetokea katika barabara ya Pete tangu kukamilika kwa mradi wa ujenzi wa barabara hiyo.

**Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano Alijibu:**

Mhe. Spika, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake nambari 66 lenye vifungu (), (b), (c) kama hivi ifuatavyo:-

Mhe. Spika, kabla ya kumjibu Mhe. Mwakilishi naomba nianze kwa kuwapa pole wazazi, ndugu na jamaa wa mtoto aliyefariki kwa ajali ya barabarani hapo eneo la Pete siku chache zilizopita.

a) Mhe. Spika, barabara inayotoka Mwanakwerekwe kupitia Pete hadi Makunduchi ni barabara kuu (*Truck road*) ambayo hutumiwa na magari mengi kwa kwa shughuli za kijamii na kitaifa. Mhe. Spika, Wizara yangu imekuwa ikichukua juhudi za kuweka alama za barabarani kwa ajili ya usalama wa watumiaji wa barabara hizo wakiwemo wenye vyombo vya moto, baiskeli na wendao kwa miguu. Kwa bahati mbaya sana baadhi ya wananchi wetu wamekuwa wakiharibu na kuiba alama hizo na hivyo kuchangia uwezekano wa kutokea ajali kwenye barabara husika. Eneo la Pete ni moja ya maeneo yaliyowekwa alama hizi lakini ziliibiwa.

   Mhe. Spika, uwekaji wa matuta barabarani si suluhisho sahihi la kudumu la kuzuia ajali barabarani. Hivyo kuna haja ya jamii yetu hasa madereva na watumiaji wengine wa barabara kufuata maelekezo ya usalama barabarani, ikiwa ni pamoja na kuzitunza alama zilizowekwa kwa ajili ya kuongeza watumiaji. Wizara yangu imelichukua wazo la Mhe. Mwakilishi na italifanyia kazi kitaalamu ikiwa ni pamoja na skurudishia alama stahiki kwenye maeneo ambayo yanaonekana ni vyanzo vya ajali.

b) Mhe. Spika, lengo la Wizara yangu ni kujenga barabara zitakazozingatia usalama wa watu na si vyenginevyo. Kwa maana hiyo kila mradi wa ujenzi wa barabara unapokamilika huzingatia sana uwekaji wa alama za usalama barabarani na maeneo ambayo ni ya msongamano zaidi kwa mfano shule, hospitali na kadhalika, hulazimika kuweka matuta yanayomlazimisha dereva kupunguza mwendo katika maeneo hayo. Hata hivyo taratibu za uwekaji wa matuta barabarani hazipewi kipaumbele sana duniani kote hasa kwenye barabara kuu. Kinachozingatia zaidi ni alama maalum za usalama barabarani ambazo dereva au mtumiaji wa barabara anapaswa kuzifuata wakati wote anapokuwa barabarani. Hivyo natoa wito kwa watumiaji wa barabara na wananchi kwa ujumla kufuata wakati wote anapokuwa barabarani. Hivyo naomba kutoa wito kwa watumiaji wa barabara na wananchi kwa ujumla kufuata na kuzithamini alama za barabara zilizowekwa ili kuepusha ajali zinaweza kuepukika.

c) Mhe. Spika, takwimu inaonesha kwamba kumetokea jumla ya ajali zisizozidi 20 na taarifa ya watu waliofariki ni watu 2. Takwimu hizi zinatokana ambazo tumepatiwa na wenzetu wa Jeshi la Polisi.

**Mhe. Jaku Hashim Ayoub:** Ahsante Mhe. Spika, Mhe. Naibu Waziri mimi ninakuheshimu na nitaendelea kukuheshimu. Mimi binafsi yangu nimeona njia ya Bububu imewekwa matuta Skuli, njia ya Mwera matuta yasiopungua 21 ambapo si eneo la Skuli. Leo huoni kama unawakejeli wale watu wa Skuli ya Kitogani, Pete na Muyuni na kupoteza maisha yao? Na Katiba ya mwaka 1984 kifungu 12 (45) naomba kunukuu Mhe. Spika.

‘Hakuna mtu yoyote atakaebaguliwa na mtu anayefanya bila sheria yoyote au katika utekelezaji wa kazi wa Ofisi yoyote na Serikali na uongozi mwengine wa chama chochote na vyombo vyake’.

Katika kifungu hicho neno kubagua ni kutimiza haja kwa watu mbali mbali kwa kuwategemea utaifa wao, kabila, jinsia, ulemavu, pahala walipotokea mwelekeo wa kisiasa au dini ambapo watu wa aina fulani wanaonekana kuwa ni dhaifu na duni au wanawekewa vikwazo na pingamizi ambazo wale watu wa aina nyengine hawaonekani na wanapewa fursa ili faida ambazo hawapewi watu au aina nyengine. Mhe. Naibu Spika, huu si ubaguzi unaoufanya.

b) Leo unataka kunambia kima punju walioekewa matuta Jozani ni muhimu kuliko binaadamu wale. Je, utakuwa tayari matuta yale tuyaondoshe pale tuyaweke Pete? Mhe. Naibu Waziri mimi ninakuheshimu sana.

**Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano:** Mhe. Spika, naomba labda nirejee maelezo niliyoyatoa. Kwamba ki utaratibu unapojenga barabara kuna alama za msingi zinawekwa. Madhumuni ya barabara ni zile alama za barabarani ndizo zinazomuongoza mtumiaji wa barabara zikiwemo *signs* pamoja na ile michoro inayochorwa katika barabara yenyewe husika. Sasa Mhe. Spika, nilichokieleza kwamba msingi wa barabara zote duniani madereva na watumiaji wengine wanaongozwa na alama. Matuta tunaweka pale ambapo kuna ulazima na nimesema miongoni mwa maeneo ambayo tunalazimika kuweka matuta ni maeneo ya shule, hospitali au mkusanyiko mwengine mkubwa. Sasa maeneo aliyoyasema ni kweli matuta yamewekwa lakini kwa vigezo tulivyovitaja.

Na kama eneo lake lile analosema sababu ya kuwekwa matuta kwa eneo la kima punju, kimapunju hawafahamu alama za barabarani na tulitaka wasigongwe. Hizo alama za barabarani alizozisema kima punju hajui zebra iko wapi, kima punju hafahamu hapa upunguze mwendo, kima punju hawana uwezo wa kusoma *road sign* ndio maana wakawekewa matuta. Lakini maeneo wanayopita wanaadamu tuanze kuweka alama za barabarani. Inavyoonekana kwamba alama za barabarani hazifanyi kazi tunalazimika kuweka matuta tunafanya katika eneo moja Unguja na Pemba na hivyo ndio utaratibu wa dunia.

Zanzibar ni sehemu ya ulimwengu hatuwezi kuwa na mambo yakajitenga na ulimwengu, tunakaribisha watalii, watalii wanapokuja wasituone watu sisi vituko, lazima tuwe na sheria za ulimwengu. Barabara zinaongozwa na *road sign* sio matuta, matuta yanakuwa ni *last option* kwamba hapa hakuna namna lazima tuweke matuta tunusuru maisha kama kuna malalamiko Mheshimiwa Mwakilishi alete sisi tutakwenda kumuwekea. Sio jambo la kupiga kelele kusema nchi hii inabaguliwa watu. Hakuna mtu ambaye anapata huduma dhidi ya mwengine, watu wote wako sawa kwa mujibu wa hiyo katiba. Na alichokisema Mhe. Mwakilishi Serikali haijatoa upendeleo kwa kima punju, Serikali ilichokiona kima punju hafahamu sheria za barabarani. Kama yeye Mhe. Mwakilishi atatuthibitishia *road sign* kima punju ataweza kuzisoma sisi tutandosha matuta tutaweka hizo *road sign* ili kima punju asigongwe. Kwa sababu madhumuni ya Serikali ni kuona kwamba kima punju ni kivutio cha utalii kiwepo nchini na wasiathiriwe tuwakinge na ajali ndio madhumuni ya Serikali.

**Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano:** Mhe. Spika, na mimi nikushukuru kwa kunipa nafasi ya kuongezea ufafanuzi zaidi, lakini nimpongeze Naibu wangu kwa namna ambavyo amejibu maswali haya.

Mhe. Spika, sasa hivi suala la matuta kwenye barabara duniani ni *out dated* haliko tena. Suluhu maana ya matuta kwa hapa kwetu ni kupunguza mwendo. Alama za barabarani zinatosha kama kuna kuheshimu kwa sheria za barabarani hatungehitaji tuta mahala popote. Kwa hivyo anapogongwa mtu akafa ukasema mfano uweke tuta Mhe. Spika, barabara zote zitakuwa matuta matupu. Kama madhumuni ya matuta ni kupunguza mwendo basi labda pengine baada ya matuta ambayo yana gharama tuchimbue, lakini ukichimbua utaambiwa hiyo barabara ni mbovu.

Mimi Mhe. Spika, ninawamba kabisa wananchi wote, lakini zaidi madereva waheshimu alama za barabarani kwa sababu zipo. Mahali pa kupunguza mwendo unapunguza mwendo, mahali kuna kona, kwenye daraja alama zote zipo bila shaka alama hizo unaweza ukaziweka leo mfano hata barabara hii mpya ya Amani/Dunga zimewekwa alama lakini haijafika hata miezi 3 nusu zimeshaondolewa. Mtu anachukua paipu anakwenda kufanyia kazi, anachukua bati anakwenda kufanyia hivi. Lakini kama wananchi wote hatukushirikiana katika hili suala la matuta litakuwa kila siku lipo. Lakini kama hiyo haitoshi, kwa kawaida na kwa mujibu wa sheria Waziri ndie anayeruhusu uwekaji wa matuta barabarani.

Na kuna utaratibu zimewekwa. Mhe. Spika, suala la kuwekwa barabarani matuta lina mawazo mawili, wengine wanataka na wengine hawataki kijiji hicho kimoja. Tutakapopata barua kutoka kwa Sheha kwa sababu sheha ndie mwakilishi wa kijiji au mahali, ukiachia maeneo ya skuli, maeneo ya hospitali, maeneo ya vijiji na mwahali mwengine. Sheha anaandika barua, barua ya Sheha maana yake wananchi ndio wanakubali, inapita katika procedure Waziri ndio anasema haya weka matuta au usiweke.

Mwahali ambamo Mhe. Mwakilishi wa Muyuni anazungumzia ama hakujawekwa matuta Pete, kuna barua ya Sheha iliyoletwa kwa Waziri au mahala popote, kwa hivyo huu ni utaratibu hatuzuki tu hivi moja kwa moja tukasema weka matuta hapa, weka matuta hapa.

Kwa hivyo Mhe. Spika, alama za barabarani zipo, miongoni mwa alama hizo ni zebra cross lakini hakuna dereva mmoja anayeheshimu. Darajani pale magari yanapita wananchi wanasubiri. Kwenye maskuli magari yanapita wananchi wanasubiri. Kwa hivyo kutoheshimu alama za barabarani kila siku suala la matuta litakuwa lipo na nchi nzima hii katika barabara zetu zitaenea matuta.

**Mhe. Jaku Hashim Ayoub:** Mhe. Waziri atakuwa yuko tayari mimi kunambia ile barabara ya Mwera kuwa kuna barua za Sheha zilizoletwa kujengwa matuta 21 mpaka 25.

**Mhe. Spika:** Huo sio utaratibu hilo ni suala la nyongeza, ambalo tayari umepata nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Kwa hivyo hili sitamruhusu, na kimsingi nadhani swali hili limechukua muda mkubwa sana katika masuala haya. Kwa hivyo nishauri tukubaliane kwamba tuendelee.

**Nam. 108**

**Udanganyifu katika mitihani ya Taifa**

*(Mhe. Mjumbe aliyetaka kuuliza swali hili ameliondoa)*

**Nam. 74**

**Tatizo la Mbegu kwa wakulima**

**Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Aliuliza:**

Wakulima wengi Zanzibar msimu huu wamejitokeza kwa wingi kulima kilimo cha mpunga lakini mbegu, mbolea na dawa za kuulia wadudu zimeshindwa kuwafikia katika muda muafaka.

a) Ni tatizo gani linalopelekea hali hiyo na kusababisha malalamiko kutoka kwa wakulima.

b) Kwa kuwa Serikali imeamua kuleta Mapinduzi ya Kilimo ili kupunguza taatizo la mfumko wa bei. Kwa nini matayarisho ya upatikanaji wa pembejeo hayafanyiki mapema yaani kabla ya kuanza kwa msimu wa kilimo.

c) Je, ni wakulima wangapi wamenufaika na kilimo cha matrekta Unguja na Pemba na tani ngapi za mbolea na mbegu zimeingia Zanzibar katika msimu wa kilimo mwaka huu.

**Mhe. Waziri wa Kilimo na Maliasili Alijibu:**

Mhe. Spika, kabla kumjibu Mhe. Mwakilishi Mhe. Jaku maswali yake kwanza naomba nitoe maelezo kama ifuatavyo:-

Mara baada ya uzinduzi wa kilimo cha mpunga msimu wa 2011/2012 tulibahatika kupata mvua za vuli ambazo zilinyesha mfululizo kwa muda wa siku 60. Hali hii ilisababisha mabonde mengi kujaa maji na kusababisha matrekta mengi kushindwa kuingizwa mabondeni na hivyo kusitisha utoaji huduma za matrekta kwa muda wa miezi karibu miwili. Baada ya mvua za vuli kumalizika na hali ya mabonde iliporuhusu uchimbaji, wakulima walijitokeza kwa wingi kuhitaji huduma za matrekta kila mmoja akikimbilia kuwahi msimu. Hata hivyo kutokana na idadi ya matrekta yaliyokuwepo haikuwa rahisi kuwapatia huduma wakulima wote kwa wakati mmoja. Wizara kwa kulitambua hilo ilichukua juhudi ya kuongeza matrekta 10 mapya ambayo yalisaidia sana kutoa huduma hii na kuweza kufikia asilimia 96 ya lengo lililowekwa Unguja na Pemba.

Mhe. Spika, kwa upande wa pembejeo za kilimo, Wizara ilijiandaa vya kutosha katika suala la mbegu ambapo kwa mara ya kwanza tuliweza kutoa tani 322 ya mbegu bora ya mpunga msimu huu wa mwaka 2012 ikilinganishwa na tani 124 mwaka 2011 na tani 55 mwaka 2010. Kwa jumla hakukuwa na malalamiko makubwa juu ya upatikanaji wa mbegu za mpunga mwaka huu. Aidha maandalizi ya pembejeo za mbolea na dawa ya kuulia magugu yalifanywa mapema kwa kuagiza lita 20,000 za dawa ya magugu ikilinganishwa na lita 18,000 mwaka 2011 na tani 590 za mbolea mwaka 2011.

Mhe. Spika, napenda kuchukua fursa hii kukiri kwamba pembejeo za mbolea na dawa ya kuulia magugu hazikuweza kutosheleza mahitaji ya wakulima. Mwaka huu kutokana na kuwa wakulima wengi wamehamasika na kuitikia wito wa serikali wa kuendeleza kilimo cha mpunga hasa baada ya mpango wa ruzuku iliyotolewa na serikali. Maandalizi yaliyofanywa na makisio ya wingi wa pembejeo hizi yalizingatia zaidi uzoefu wa mahitaji ya pembejeo hizi kwa miaka iliyopita. Wizara ya Kilimo na Maliasili inaupokea ushauri wa kuanza mapema kwa matayarisho ya ununuzi wa pembejeo na imejipanga kuhakikisha kuwa msimu ujao tatizo hilo halitatokea tena.

Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo machache sasa naomba niyajibu maswali ya Mhe. Mjumbe kama hivi ifuatavyo:-

a) Mhe. Spika, ni kweli kuwa wakulima wengi wamejitokeza msimu huu kwa kilimo cha mpunga na hali hii imetokana na wakulima kuhamasika baada ya serikali kutangaza ruzuku katika utoaji wa pembejeo na huduma za matrekta.

b) Mhe. Spika, kilichocheleweshа kilimo si utoaji wa pembejeo bali ni kuchelewa kwa huduma ya matrekta kutokana na mvua kubwa za vuli zilizonyesha mwaka huu na kusababisha maeneo mengi ya mabonde kutuwama maji na hivyo kucheleweshа ukulima. Kwa ujumla hali hii kwa kiasi kikubwa imesababishwa na mabadiliko ya hali ya hewa na tabia ya nchi. Hali hii pia imetokea wakati wa msimu wa masika ambapo mvua zimekuwa chache na kwa kiwango cha chini sana hali ambayo haijtokea kwa miaka mingi iliyopita.

c) Mhe. Spika, serikali imekusudia kuleta Mapinduzi ya Kilimo na Mpango huo umeanza kutekelezwa kuanzia Bajeti ya mwaka 2011/12, hususan katika utekelezaji programu ya kuendeleza kilimo cha mpunga na upandaji wa mikarafuu. Wizara ya Kilimo inakubaliana na ushauri uliotolewa na Mwakilishi na kwa kushirikiana na Wizara ya Fedha itahakikisha kuwa upatikanaji wa pembejeo na huduma ya matrekta kwa ajili ya kilimo cha mpunga, mikarafuu na mazao mengine ya chakula na biashara kinafanyika kwa wakati.

Kuhusu wakulima wangapi walionufaika na huduma za matrekta, swali hili nalijibu kwa kutumia ekari zilizolimwa. Kwa upande wa Pemba lengo la kulima kwa trekta lilikuwa ekari 2,700, lakini zilizolimwa ni ekari 4,430 sawa na asilimia 217 na kwa Unguja lengo lilikuwa kulima ekari 15,400 lakini zilizolimwa ni ekari 13,155 sawa na asilimia 85.4. Kwa ujumla lengo la la kilimo cha mpunga kwa kutumia matrekta ya mkono Unguja na Pemba mwaka ilikuwa ekari 33,000 na utekelezaji umefikia 31,800 sawa na asilimia 96.7 ya lengo.

**Mhe. Jaku Hashim Ayoub:** Mhe. Spika, kwanza nimpongeze Mhe. Waziri kwa majibu marefu sana aliyoyatoa na katika swali la msingi alisema Mhe. Waziri kuwa kuna maeneo yamejaa maji, lakini eneo la Muyuni halikujaa maji na trekta limekuja likaburuga na kuna sehemu likaacha. Wananchi wakawa wanahaha na kuhangaika na trekta lile halikuja tena, ni sababu gani ya kunyimwa haki ile na katika watu walioitikia wito ni wananchi wa Muyuni na Waziri wa Nchi (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi ni shahidi wa hilo aliuona mpunga jinsi ulivyonawiri.

Je, Mhe. Waziri utakuwa tayari wananchi wale hivi sasa kuwapatia trekta likabaki pale pale kuitikia kilimo chengine baada ya kuvuna mpunga huo walime kunde.

**Mhe. Waziri wa Kilimo na Maliasili:** Mhe. Spika, simsikii anazungumza nini.

**Mhe. Spika:** Rudia swali kidogo Mhe. Mjumbe.

**Mhe. Jaku Hashim Ayoub:** Ahsante Mhe. Spika, kwanza nimshukuru Mhe. Waziri kwa majibu marefu sana aliyoyatoa na ya ufasaha kabisa katika swali la msingi alipokuwa akijibu, nikushukuru sana. Alipokuwa akijibu swali la msingi alisema kuna maeneo mengi yalijaa maji matrekta hayakuweza kufika, lakini eneo la Muyuni halikujaa maji lilikuja trekta likaburuga na kuna eneo likaacha kabisa halikufanya kazi. Wananchi wale wakaendelea kuteseka na kuhangaika lile eneo mpaka leo halikuburugwa. Na katika wananchi walioitikia wito wa kilimo cha mpunga ni wananchi wa Muyuni, Mhe. Rais alikuwa shahidi wa hilo katika ziara yake aliyoifanya na Waziri wa Nchi (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi alishuhudia. Wananchi wale hivi sasa wameshaanza kuvuna mpunga huo na sasa wanataka kuguruga tena konde hizo kwa kupanda kunde.

Je, Mhe. Waziri utakuwa tayari kuwakabidhi trekta walitumie pale na likabaki pale pale, kama itawezekana hata kama ikawa ni mali yao.

**Mhe. Waziri wa Kilimo na Maliasili:** Mhe. Spika, kuhusiana na sehemu ya Muyuni kule mvua hazikupiga kwa wingi kama sehemu nyengine. Kwa hivyo, suala hilo nililozungumza hapo ni kwamba wao ndio waliokuwa wamepata bahati kulima mapema na kupanda mapema na kukiuka yale malengo yaliyokuwepo. Kwa sehemu nyengine ni suala la maji au mvua lakini kwa sehemu ya Muyuni kutokana na hali ya hewa ilivyokuwa wao waliwahi mapema na suala hilo halikutokea hivyo ambavyo unafikiria.

**Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi:** Ahsante sana Mhe. Spika, kunipa nafasi kuuliza swali moja la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri na maelezo marefu sana lakini atakubaliana nami kwamba wako baadhi ya wakulima mazao yao yameharibika kutokana na upepo na wadudu wanaoitwa nyevule. Je, Mhe. Waziri ana wito gani kwa wakulima hao.

**Mhe. Waziri wa Kilimo na Maliasili:** Mhe. Spika, kwa ziara ambayo itafanywa na waziri kwa kipindi kijacho ningelimuomba Mhe. Mwakilishi awe karibu ili tuweze kutatua hilo tatizo analolisema.

**Mhe. Bikame Yussuf Hamad:** Ahsante Mhe. Spika, kwa kunipa fursa hii ya kuweza kumuuliza Mhe. Waziri swali moja dogo la nyongeza. Kwa kuwa serikali imetoa wito wa kuleta Mpinduzi ya Kilimo na kwa kuwa serikali sasa hivi imeshajipanga kuleta mbolea nyingi kwa ajili ya kuwa wakulima walikosa mbolea kipindi kilichopita, na kwa kuwa wataalamu wa kilimo wanasema tunapotumia mbolea nyingi katika ardhi basi inaweza kuleta matatizo kutokana na sisi huwa tunatumia maji ya kunywa na matumizi mengine.

Je, serikali imejipanga vipi na kutuletea mbolea m-badala ili wakulima wetu waweze kutumia mbolea hizo na kuepukana na mbolea za kemikali zilizo nyingi.

**Mhe. Waziri wa Kilimo na Maliasili:** Mhe. Spika, suala moja na kwamba sehemu ya uletaji mbolea kitu kimoja ambacho kimefanywa sana na serikali kwanza Mapinduzi ya Kilimo ni pamoja na uongozaji ambao matrekta yaliyokuwa yameongezwa katika kipindi hiki kidogo ambapo matrekta hayo tunatarajia kwa msimu ujao ni karibu matrekta 38 yatatumika kuongeza Mapinduzi ya Kilimo.

Pili ni kweli utumiaji wa mbolea kwa muda mrefu kunahatarisha kima cha maji cha chini kuchanganya sumu katika ulimaji huo. Kwa vyovyote vile katika suala la kuongeza kilimo ni vizuri kuwa na mbolea safi na ambayo haileti madhara. Kwa hivyo, katika kushughulikia sana suala hili kwa sasa Mapinduzi ya Kilimo sio utumiaji peke yake wa dawa ambazo zitatumika kwa suala zima la kilimo cha mpunga.

**Nam. 120**

**Ukosefu wa Uzio katika Hospitali ya Mkoani**

**Mhe. Asha Abdu Haji** – Aliuliza:-

Ili wagonjwa wapate utulivu wa kutosha, kuna haja ya kuwepo usimamizi mzuri wa uwangalizi wa wagonjwa. Katika kufanikisha suala hili Hospitali ya Mkoani inakabiliwa na changamoto ya kukosekana kwa uzio katika eneo lao hali ambayo inakwamisha jitihada zao.

Je, Mhe. Waziri tatizo hili litachukuliwa hatua gani ili kuepusha kuathiri shughuli za hospitali.

**Mhe. Naibu Waziri wa Afya** – Alijibu:-

Mhe. Spika, Kwa heshima yako naomba uniruhusu nimjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 120 kama ifuatavyo:

Mhe. Spika, ni matumaini yangu kwamba wawakilishi au mwakilishi kama anaifahamu vizuri hiyo Hospitali ya Abdalla Mzee Mkoani ilipojengwa ilikuwa na uzio. Kwa bahati mbaya wananchi wanaoishi mzunguko wa eneo hilo kwa namna moja au nyengine wameuharibu uzio huu. Hata hivyo, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kupitia Wizara ya Afya na Serikali ya Jamhuri ya Watu wa China wameshakubaliana kuijenga upya hospitali hiyo ukiwemo na uzio.

**Mhe. Asha Abdu Haji:** Ahsante sana Mhe. Spika, kwa kunipa fursa hii ya kuuliza swali la nyongeza. Ni lini tutarajie hospitali hiyo kufanyiwa matengenezo na hatimaye uzio kujengwa.

**Mhe. Naibu Waziri wa Afya:** Mhe. Spika, makubaliano ya serikali na watu wa China yameshafikiwa, hivi sasa Balozi amekwenda China lakini tunategemea kwamba mwezi wa Septemba atakuja pamoja na *technical team* kuja kufanya makisio na jinsi ya utaratibu wa kujenga hospitali hiyo.

**Nam. 140**

**Ujenzi wa Nyumba za Watoto Yatima Pemba**

**Mhe. Viwe Khamis Abdalla** – Aliuliza:-

Katika Kampeni zake Mhe. Rais wetu aliahidi kujenga nyumba za watoto yatima huko kisiwani Pemba. Je, Mhe. Waziri tokea kutolewa kwa ahadi hiyo ni hatua gani zilizochukuliwa.

**Mhe. Waziri wa Ustawi wa Jamii, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto** – Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Viwe Khamis Abdalla swali lake Nam. 140 kama hivi ifuatavyo:

Mhe. Spika, katika kutekeleza ahadi ya Mhe. Rais Dr. Ali Mohammed Shein aliyoitoa katika kampeni zake za kujenga nyumba ya kulelea watoto huko Pemba, wizara inalijua suala hilo na imeshaanza kulifanyia kazi. Hatua ya ujenzi itaanza wakati wowote wa kifedha utapopatikana.

**Mhe. Viwe Khamis Abdalla:** Nakushukuru Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kumuuliza swali dogo la nyongeza. Kwa kuwa Kisiwani Pemba kuna Mikoa miwili na wilaya zake nne. Je, Mhe. Waziri nyumba hizo za watoto yatima zitajengwa wilaya gani ili kuepusha usumbufu wa watoto wetu.

**Mhe. Waziri wa Ustawi wa Jamii, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto:** Mhe. Spika, tunategemea sana kujenga kituo hiki katikati ya Mikoa miwili baina ya Kusini na Kaskazini yaani Chake Chake.

**Mhe. Makame Mshimba Mbarouk:** Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi kuweza kunipa uwezo wa kuweza kumuuliza Mhe. Waziri swali la nyongeza. Mhe. Waziri katika jibu lako mama umesema kuwa wakati wowote jengo hilo litaweza kujengwa. Je, Mhe. Waziri ni kiasi gani jengo hilo litagharimu.

**Mhe. Waziri wa Ustawi wa Jamii, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto:** Mhe. Spika, kiasi cha fedha kitakachogharimu kwa sasa hivi siwezi kujibu, kwa sababu kuna kazi nyingi zinazotakiwa kufanywa mpaka kufikia nafasi ile ya kulijenga jengo lenyewe. Lakini ikiwa tayari nitamjibu nitamwambia ni kiasi gani kinachotakiwa.

**Mhe. Subeit Khamis Faki:** Nakushukuru sana Mhe. Spika, kunipa na mimi fursa nimuulize Mhe. Waziri swali moja la nyongeza. Wakati Mhe. Waziri alipojibu alikiri kuwa ahadi hii ilitolewa na Rais wakati wa kampeni na kwa kuwa sasa hivi ni bajeti ya pili hii ya serikali tangu kuingia madarakani serikali hii ya Awamu ya Saba. Sasa napenda kumuuliza kwamba je, katika bajeti hii ya serikali inayoendelea imeandaliwa kiasi gani cha fedha ili kutekeleza ahadi hiyo ya Rais.

Pili, baada ya kusema kwamba itajengwa katikati baina ya Mikoa miwili ya Pemba. Je, kiwanja hicho kitakachojengwa kimenunuliwa eneo gani na kiasi gani cha fedha.

**Mhe. Waziri wa Ustawi wa Jamii, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto:** Mhe. Spika, kwanza katika bajeti hii nataka nimwambie kwamba haimo, kiasi gani ambacho tutatumia hatukutia katika bajeti hii. Lakini ninachotaka kumhakikishia kwamba jengo litajengwa na sasa hivi tunahangaika huku na kule ili jengo hili lijengwe kabla ya kumaliza miaka yetu mitano ya uongozi. Hilo la kwanza.

La pili Mhe. Spika, kiwanja siwezi kumwambia kimenunuliwa kiasi gani, lakini kiwanja kipo tayari namhakikishia Mhe. Mjumbe.

**Nam. 94**

**Baraza la Michezo la Taifa**

**Mhe. Jaku Hashim Ayoub** - Aliuliza:-

Baraza la Michezo la Taifa *BTMK* Zanzibar kazi yake kubwa ni kusimamia Sheria ya vyama vya michezo ikiwemo kuhakikisha kila chama kinakuwa na uongozi wa kuchaguliwa Kikatiba.

(a) Kwa nini Chama cha Mpira wa *Netball* (CHANEZA) hakijafanya Uchaguzi kwa muda mrefu wa viongozi wake.

(b) Kwa nini chama hicho kinaendelea kufanya shughuli zake kama kawaida na viongozi ambao wamepoteza sifa kutokana na chama hicho kutofanya uchaguzi kwa zaidi ya miaka 10.

(c) Kukosekana kwa uongozi kunasaidia vipi maendeleo ya chama hicho.

**Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo** - Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake nambari 94 lenye kifungu (a), (b), na (c) kama ifuatavyo;-

Mhe. Spika, nakubaliana na Mhe. Mwakilishi kwamba Baraza la Michezo la Taifa Zanzibar (BMTZ) kazi yake kubwa ni kusimamia Sheria za Vyama vya Michezo ikiwemo kuhakikisha kila chama kinakuwa na uongozi wa kuchaguliwa kikatiba.

a) Ni kweli Chama cha Netibali (CHANEZA) hakijafanya uchaguzi wa viongozi wake kwa muda mrefu kutokana na wanachama wa chama hicho kushindwa kujitokeza kugombea nafasi za uongozi kila uchaguzi unapotayarishwa.

b) Viongozi wa Chama hicho cha CHANEZA wanendelea kufanya kazi kama kawaida wakichukuliwa kama ni viongozi wa mpito ili kusimamia wananchi wetu wanaoendeleza kucheza mpira wa *netball* hapa Zanzibar, vyenginevyo kingekosa usimamizi na kusababisha kupoteza umaarufu wake.

c) Kukosekana na uongozi wa kuchaguliwa hakusaidii sana maendeleo ya chama hicho kwani licha ya kuonekana mchezo huo kupendwa na wanamichezo wengi, lakini umadhubuti wa uwajibikaji hupungua na ndio maana ofisi ya usajili ya vyama vya michezo ikafikia kuchukua hatua ya kudhamiria kufuta usajili wa chama hicho ikiwa itashindwa kufanya uchaguzi baada ya miezi mitatu.

**Mhe. Jaku Hashim Ayoub:** Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri wizara yake itachukua hatua gani kuwaelimisha kuchukua fomu za uchaguzi ili mchezo huo usije ukaporomoka na lini utatangaza tarehe ya uchaguzi.

Pili, kwa kuwa hakuna uongozi wa kudumu watu wanafanya kazi kwa hiari kuna hatari ya haraka sana mchezo huu kuporomoka. Je, utachukua hatua gani.

**Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo:** Nakushukuru Mhe. Spika, wizara yangu kupitia Baraza la Michezo jukumu lake kubwa ni kuhakikisha kwamba vilabu mbali mbali vya michezo vinaendesha shughuli zake kwa mujibu wa katiba zao. Na pale ambapo katiba zao zimeshindwa kutekelezwa basi mrajis wa michezo anayefanya kazi ndani ya Baraza ni kuwakumbusha kwamba wanatakiwa kusimamia katiba zao ikiwemo kufanya chaguzi za kawaida za vilabu vyao. Sasa Baraza la Michezo linatoa taaluma na mrajis wa michezo anakumbusha, lakini pale ambapo vinashindwa basi kwa mujibu wa sheria mrajis anachofanya ni kufuta usajili wa chama hicho.

Kwa hivyo, CHANEZA ina tatizo hilo na imeshapewa *ultimatum* ya muda wa miezi mitatu kuanzia tarehe 30 mwezi uliopita baada ya hapo kama itashindwa kusimamia katiba yake wizara kupitia Mrajis wa Michezo itakuwa haina chaguo isipokuwa kukifuta chama hicho. Kwa hivyo hiki ndicho kinachoendelea Mhe. Spika.

**Mhe. Farida Amour Mohamded:** Nakushukuru Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza. Mhe. Naibu Waziri katika majibu yake mama alizungumza kwamba hawa wameshindwa kufanya uchaguzi wa kudumu. Sasa Mhe. Naibu Waziri kama wewe ni mwanamke na Mhe. Rais kaleta uteuzi wako kwenye mambo ya michezo hakukosea. Je, wewe utawasaidiaje wanawake wa chama hiki kabla hawajafutiwa usajili wao wakati mwenyewe umekiri kuwa watu wanaupenda sana mchezo huo.

**Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo:** Mhe. Spika, ni kweli na nakupongeza sana kuweza kuniuliza swali hilo. Kwa sababu nikiwa Naibu Waziri mwanamke na Mwenyekiti wa CHANEZA ni mwanamke tutashirikiana ili kukaa na wanawake wenzetu waweze kufanya uchaguzi haraka ili wasije wakafutiwa usajili wao.

**Mhe. Salim Nassor Ali:** Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Mchezo wa *Netball* ni mchezo ambao unafuatiliwa na kupendwa hapa Zanzíbar ukiongozwa na Mpira wa Miguu. Mchezo huu hivi sasa unachezwa hasa na wanaume na hupendwa pia na wanaume akiwemo Mzee wangu Mhe. Ali Juma Shamuhuna ni mpenzi sana wa mpira huu wa *Netball*. Mhe. Waziri katika majibu yake amesema kwamba kweli chama hiki kimejipanga kufanya uchaguzi, swali langu ni kwamba. Mchezo huu katika Wilaya zote za Unguja ni wilaya gani ambayo haina uongozi kwa Unguja na Pemba.

Pili, wizara ina mikakati gani kuhakikisha kwamba mchezo huu unaenea wilaya zote za Unguja na Pemba.

**Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo:** Mhe. Spika, taarifa tuliyonayo ni kwamba hivi sasa karibu Wilaya zote zina uongozi wa Chama hiki cha Mpira wa Mikono CHANEZA. Sasa kama alivyosema mwenyewe kwamba hivi sasa sio lazima tu wanawake ambao wanalazimika kucheza mpira huu hata wanaume. Wizara jukumu lake ni kushirikiana na wadau wa michezo kuona kwamba michezo inaimarika, wizara sisi tuko tayari kushirikiana na wadau wote hata Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi ambao wametajwa humu Mzee wetu huyu Mhe. Ali Juma Shamuhuna lakini hata yeye mwenyewe pia Mhe. Salim Nassor Ali ni mdau mzuri wa michezo.

Kwa hivyo, ni vizuri turudi kwenye wilaya zetu tukashirikiane na vyama hivi kuviongezea nguvu ili viimarishe mchezo huu vifanye uchaguzi, kwa pamoja basi tushirikiane na chama na Baraza la Michezo tuhakikishe kwamba kabla ya miezi mitatu uchaguzi umefanyika, kwa sababu *ultimatum* tupo makini na hiyo na *serious*, vyenginevyo sisi sote Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi baadae tutalaumiwa kwamba chama hiki kimefutwa.

Kwa hivyo ni vizuri wadau wa michezo ambao ni Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi ambao wametoka katika wilaya mbali mbali, tushirikiane na viongozi waliopo wilayani kuona kwamba mchezo huu unaendelea kuimarika, na ni kweli kwamba una wadau wengi na wapenzi wengi katika nchi yetu. Kwa hivyo tushirikiane kwa pamoja.

**UTARATIBU**

**Mhe. Ismail Jussa Ladhu:** Ninakushukuru Mhe. Spika, kwa kunipa fursa hii na muongozo wangu unahusu Kanuni ya 44.
Mhe. Spika, Kanuni hii inahusu taarifa ya serikali na ninaomba kuitumia hii kutumia kiti chako au kupitia kiti chako kuomba suala dogo kwa serikali kwa leo. Mhe. Spika, katika vyombo vya habari tangu jana hadi leo, kumetawala suala zito ambalo limeihusisha Zanzibar. Imeripotiwa katika gazeti la Citizen la jana katika habari inayosema, “Foreign Minister Bernard Membe described the news as shocking, strange, and irregular” .

Lakini habari yenyewe inasema, *Iran tankers adopt Tanzania flag to avoid embargo*. Katika taarifa hiyo Mhe. Spika, imehusishwa Zanzibar, kwa sababu labda ya Wajumbe niseme kwamba suala hili linahusu tuhuma kwamba kuna meli za mafuta za Iran katika kukwepa vikwazo vya kiuchumi vimeamua kutumia bendera ya Tanzania katika meli zao ili zisipate matatizo.

Lakini katika taarifa hii kwa sababu Tanzania hawana utaratibu wa *open registration*, imetajwa Zanzibar kama ndio eneo ambapo meli hizi zimepatiwa leseni hiyo. Sasa suala hili linaonekana lina utata mwingi na kuonekana kama vile Mhe. Spika, kuna mpango wa kutaka kuiharibia na kuipaka matope Zanzibar kwa suala hili, kwa sababu tu utaratibu wake tofauti, sisi tumeamua kuwa na *open registration*.

Sasa nilikuwa naomba tu Mhe. Spika, kwa Kanuni ya 44 si kwa leo lakini angalau kesho basi serikali ingetuandalia taarifa juu ya suala hili ili kupitia chombo hiki cha wananchi, suala hili likawa *cleared* na tukajisafisha na tuhuma hizi ambazo sasa zinaonekana zinaingia katika vyombo vya habari vya kimataifa na vinaweza vikaleta athari kubwa sana kwa Zanzibar na kwa uchumi.

Naomba Mhe. Spika, kutupa muongozo kuhusu suala hili.

**Mhe. Spika**: Waheshimiwa Wajumbe ni jambo zuri na ni jambo la kawaida kunapotokea jambo kubwa ndani ya nchi au kutoka nje kutaka kuingia ndani ya nchi au habari za kupotosha kwa ajili ya nchi yetu au dhidi ya nchi yetu, ni vizuri serikali ikalifanyia kazi na ikaweza kutoa taarifa rasmi ama kwa kupitia chombo hiki au hata kwa njia ya redio au televisheni.

Utaratibu huu serikali huwa inafanya hasa kwenye maadhimisho ya siku mbali mbali duniani, huwa taarifa zinatoka za serikali juu ya mambo mbali mbali juu ya taarifa zile na kama kuna jambo jengine lolote.

Ninakumbuka tu hivi karibuni tu Mhe. Mohamed Aboud Mohamed ametoa taarifa baada ya kutokea tatizo kubwa la vurumai katika nchi yetu, alitoa kwenye vyombo vya habari na pia akaja akatoa taarifa hapa na hasa katika kipindi cha maswali na majibu, na hata wakati wa bajeti yake.

Mimi ninadhani serikali wacha iangalie suala hilo, ili tuone utaratibu wa kuweza kutoa taarifa rasmi inayohusu jambo hili kama kuna dalili za kuipaka matope nchi yetu, basi kuondoa hilo tatizo. Kwa sababu ni kweli linaweza likaathiri kwa kiasi fulani harakati zetu za kiuchumi kupitia masuala ya kitalii.

Kwa hivyo, serikali tuone inalifanyia kazi suala hili.

**Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais:** Mhe. Spika, kwanza ninakushukuru kwa kunipa nafasi lakini pia nimshukuru Mhe. Jussa kwa kuwa makini na kufuatilia mambo hasa kwenye vyombo hivi vya habari. Hata mimi niliiona jana na bahati nzuri niliwatafuta watendaji wangu na kuwaambia walishughulikie jambo hili, na bado lipo katika ngazi ya wataalamu hawajanipa taarifa rasmi.

Lakini kwa kuwa serikali inafanya kazi kwa pamoja, naomba muda tuwasiliane na wenzetu wa Wizara ya Mawasiliano, nina hakika watendaji wangu watakuwa wamefanya kazi hiyo kwa sababu tangu jana nimewaachia.

Ninawahakikishia Wajumbe wa Baraza lako hili tunaweza tukatoa taarifa vizuri zaidi kwa kesho tu kueleza taarifa kamili juu ya jambo hili. Ahsante sana Mhe. Spika.

**Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano:** Mhe. Spika, na mimi nikushukuru sana na pia nimshukuru Mhe. Jussa kwa hili ambalo amelieleza kwenye Baraza lako tukufu.

Mhe. Spika, hata kabla ya Mhe. Jussa tulileta hapa Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano kwa kupitia Mamlaka ya Usafiri Baharini wameshaanza kulifanyia kazi suala hili. Naomba niliarifu Baraza lako tukufu kwa kupitia wewe kwamba tutashirikiana na Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais ili tulete taarifa rasmi ya serikali kuhusu jambo hili.

Lakini kwa taarifa za awali tu ni kwamba hatuna kumbukumbu si hapa Zanzibar wala ma-*agents* wetu waliopo Dubai ambao wanasajili meli *open registry* kwamba meli zilizotajwa tumezisajili sisi. Lakini kama nilivyosema hizo ni taarifa za awali lakini taarifa kamilifu tunaomba tuiwasilishe kesho baada ya kuifanyia kazi.

Ninakushukuru sana Mhe. Spika.

**Mhe. Hamza Hassan Juma:** Mhe. Spika, nitatumia haki yangu ya Kanuni kifungu cha 50 (4) (h) lakini hilo suala linataka muongozo wako. Kutokana na mijadala yetu humu Barazani kuna baadhi ya Waheshimiwa wanarejearejea sana kuwauliza Manaibu Mawaziri maswali wakati wanapojibu maswali.

Na wakati wanapojibu maswali wanajibu maswali yale kwa niaba ya Waziri, sasa tulikuwa tunataka muongozo wako. Jee, anapoulizwa Naibu Waziri inakuwa ni sahihi au aulizwe Waziri, Naibu Waziri yeye ndio ajibu.

**Mhe. Spika**: Sina hakika kama umekusudia katika maswali ya nyongeza. Kwenye maswali ya nyongeza kama hapa alisimama Mhe. Naibu Waziri, muulizaji wa swali la nyongeza huwa yule aliyepo, ni utamaduni wetu wa kawaida.

Lakini pia katika maswali mama kwa kawaida inapaswa kwenye Wizara. Wizara msimamizi wake mkuu ni Waziri. Kwa hivyo mimi huwa ninamwita Waziri. Kama wizara ile ina Naibu Waziri utamaduni wetu wa muda mrefu tangu tumeanza vyombo hivi wizara yenye Naibu Waziri basi Naibu Waziri huwa anajibu, pale panapohitajika majibu ya nyongeza Waziri huwa anasimama hupewa nafasi akajibu.

Kwa hivyo ninadhani ni utamaduni na mambo ambayo tumeyafuata muda mrefu sana. Lakini kimsingi mambo yanayohusu wizara, kwa kawaida Waziri ndiye mwenye dhamana ya wizara hiyo na maswali na hoja zote zinategemewa Waziri ndiye muhusika. Sasa kama kuna Naibu Waziri huwa wanasaidiana, kwa upande wa maswali Naibu Waziri anatangulia kujibu, kama kuna nyongeza au kuna haja ya kuongeza majibu au kama kidogo jambo zito pengine Mhe. Naibu Waziri hana taarifa nalo, basi Waziri huwa anajibu.

Lakini kwa upande wa hoja hii tumekubaliana ndani ya Kanuni yetu moja kwa moja kwamba Waziri ndiye awe na dhamana ya kujibu au kutoa hoja hiyo. Kama hayupo hamzuii. Hivyo ndivyo tumekubaliana katika utaratibu wetu.

Basi ninadhani baada ya hapo tuendelee, maana muda wetu ni mfupi na hoja hii ambayo iliyowasilishwa jana tunategemea jioni ijumuishwe na Mhe. Waziri. Kwa hivyo niwaombe sana Waheshimiwa Wajumbe tupo nyuma kidogo ya ratiba yetu na ilikuwa hivyo sababu ya umuhimu, si kwa sababu ya jambo lolote, umuhimu wa shughuli tuliyoimaliza ya Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais tulimmegea muda kidogo na tukawa tupo nyuma kwa kiasi fulani.

Niwaombe basi Waheshimiwa Wajumbe katika kuendelea kuchangia tupange *points* zetu vizuri, tupunguze kurearejea kama Kanuni zinavyoelekeza, lakini tuwe tunasema yale mambo yanayohusu jambo liliopo mezani, tusitoke nje ya mipaka na ndivyo taratibu zetu za Kanuni zinatuelekeza hivyo.

**HOJA ZA SERIKALI**

**Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha - Wizara ya Nchi Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais kwa mwaka wa fedha 2012/2013**

*(Majadiliano yanaendelea)*

**Mhe. Suleiman Hemed Khamis:** Mhe. Spika, ninakushukuru na mimi kwa kunipa nafasi ya kuweza kutoa mchango wangu katika hotuba ya Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais.

Mhe. Spika, katika masuala ambayo nimejitayarisha la kwanza ambalo ninataka kulizungmzia ni juu ya masuala ya dawa za kulevya. Tunafahamu Idara ina juhudi kubwa sana ya kutimiza majukumu yake. Inatoa taaluma, huduma za tiba, ushauri nasaha na vile vile inajiandaa mara kwa mara kwa semina mbali mbali.

Lakini sasa tukizungumzia hili suala lenyewe la dawa za kulevya ambapo tunajua kwamba dawa hizi zinaathiri vijana wetu. Hawa kama tunavyosema ni vijana nguvu kazi na bado masuala haya yanaendelea, vijana wetu wanaathirika na idadi ya vijana inazidi kuongezeka.

Sasa labda tu nimuulize Mhe. Waziri katika suala hili la dawa za kulevya, wizara yake imejitahidi kiasi gani kudhibiti dawa za kulevya Zanzibar. Kwa sababu ni lazima tuweze kupata taarifa awali yake ilivyokuwa na hivi sasa tulivyo, kama labda wizara imefanya jitihada kubwa ya kupunguza uingiaji wa dawa za kulevya Zanzibar.

Au vile vile Wizara ilikuwa ituarifu kwamba biashara hii bado inaendelea na tumeshindwa bado kuidhibiti. Lakini vile vile tunataka kujua kwa waziri kwamba kwa kiasi gani wale ambao waliopewa dhamana, bila shaka hii kazi wamepewa watu dhamana maalum ya kufuatilia masuala haya. Tunataka tujue dhamana yao waliyopewa wameweza kudhibiti kiasi gani.

Vile vile tulitaka tujue kama taarifa au tupate taarifa za kutosha kuhusu masuala haya ya dawa za kulevya. Mhe. Spika, kwa taarifa tulizonazo ni kwamba inasadikiwa maeneo makubwa ya biashara hii ni bandarini pamoja na uwanja wa ndege.

Lakini tusisahau kwamba nchi yetu ni visiwa; kuna kisiwa cha Unguja na Pemba. Uingiaji wa dawa sio lazima bandarini ambapo meli kubwa zinaingia kutoka kila mwahala na uwanja wa ndege, lakini kuna maeneo mengine inasadikiwa dawa hizi zinapita. Kwa hivyo tulitaka tujue vile vile kwamba jee taarifa zikoje katika maeneo mengine, sana yanaaminika kwenye bandari na uwanja wa ndege lakini jee maeneo mengine ambayo ni chanzo vile vile cha kuingiza dawa hizi. Jee jitihada gani zimefanyika au kufanya utafiti na kujua kuna maeneo madogo madogo pia dawa hizi zinaingia, kwa sababu hivi ni visiwa na vimezungukwa na bahari, kwa hivyo meli au mashua au chombo chochote kinaweza kuingia mahali popote na wakati wowote.

Jambo jengine katika masuala haya tunataka kujua hiki choo kilichotaka kupelekwa uwanja wa ndege kule kwa ajili ya kuchunguzwa watu hawa, kwa nini mpaka leo choo hiki hakijajengwa? Ni nini sababu au kuna matatizo gani yaliyojitokeza mpaka hivi sasa. Vijana wetu hawa ambao ndio nguvu kazi tunawahitajia katika kulitumia taifa hili, lakini inaonesha bado udhibiti wa vijana wetu wa hawa wanaotumia dawa za kulevya inaonekana ni vijana wanaendelea na kutoa taarifa mbali mbali kwamba tunawasaidia hivi, lakini kwa uhakika hawa vijana wenyewe hasa tunawafanya nini mpaka leo, tuwaachilie hivi hivi waendelee au tuwadhibiti katika kuweka mahala maalum.

Kuna suala jengine vile vile tunaweza tukapata Ripoti kutoka kwa watu wengine mbali mbali ya Polisi na wao wana jitihada ya kutafuta watu hao wanaoingiza dawa za kulevya na hao wanaotumia, lakini jee Polisi Jamii tumewashirikisha kiasi gani watu hawa katika kutusaidia.

Kwa kuwa vijana waliokuwa wameshaathirika na ambao wameacha kutumia dawa za kulevya, lakini miongoni mwao ni wanawake na wengine wana watoto. Jee wizara yako ina utaratibu gani wa kuwasaidia hawa vijana katika kupata ajira. Kwa hivyo tunataka kujua serikali hapa imeandaa utaratibu gani katika kuwasaidia hawa vijana, wanalalamika mara nyingi kuwa wapo na hawapati ajira au hawakudhibitiwa kwa namna moja au nyengine, wanaweza kurudia katika kazi yao ile ya asili ya kuendelea na dawa za kulevya.

Mhe. Spika, nchi yetu imeathirika sana na suala hili na lazima serikali ichukue jitihada na bidii kubwa sana kuhakikisha kwamba vijana wetu ambao ndio nguvu kazi ya baadae wasiathirike na dawa hizi za kulevya.
Mhe. Spika, baada ya kuzungumzia suala hili la dawa za kulevya, nilitaka sasa hivi niingie katika sehemu nyengine ambazo kwenye suala zima la athari za mazingira. Mhe. Spika, kwa kweli wizara hii ina kazi ngumu na kubwa sana.

Hali ya nchi yetu inaonekana inavyoathirika siku hadi siku. Tulitaka kujua tu katika suala hili, jee upo mfumo sahihi wa utawala. Ili nchi iweze kunufaika ili nchi iweze kuwa na mazingira mazuri kwa sababu tushajua kuwa mazingira yanaathirika. Jee, ili nchi iweze kunufaika na kuwa katika mazingira mazuri ya utekelezaji wa hali hii, jee kuna sera maalum ambazo zimeekwa au hakuna sera. Kama zipo sera za zamani, jee munahisi kutokana na hali ya sasa ni kwa sababu ya kubadilisha sera zilizopo. Mhe. Spika, tunataka kujua vile vile kujua mfumo wa kisheria uliopo hivi sasa unatosheleza au tunahitaji kuweka mfumo mwengine wa kisheria kutokana na hali hii.

Jambo jengine Mhe. Spika, ni kiasi gani haki za jamii zimezingatiwa kuhusu suala la uchumi. Suala jengine ambalo lililojitokeza kwa mazungumzo ya mara kwa mara, inaonesha kuwa bado suala zima la ukataji wa miti unaendelea ambao hauridhishi. Kwani ukataji wa miti ovyo ni sababu tosha ya kuongeza hewa mkaa, uharibifu wa misitu ni suala jengine ambalo athari zake ni kubwa sana ni kuongezeka kwa joto nchini.

Hapana asiyejua katika maisha yetu tunayokwenda hivi sasa hali ya joto katika nchi yetu imeongezeka si mchana si usiku. Hali hii imeathiri sehemu kadhaa wa kadhaa. Sasa wizara hii ndipo niliposema ina kazi kubwa sana. Tuone kama ni hali gani ya kilimo kama hivi sasa inaathirika. Kilimo kinaweza kuathirika kutokana na jua kali.

Tumeelezwa hapa kuna maeneo yasiyopungua 60 yameathirika kwa maji ya chumvi. Hilo ni moja katika kazi kubwa sana ya wizara hii. Kama hali ndio hii tuangalie kima cha maji ya bahari tumeambiwa kimeongezeka, na kama kima cha maji kimeongezeka ina maana visima vingi vilivyokuwa karibu na bahari maji ya chumvi yataingia kwa wingi.

Mhe. Spika, ikifika kipindi cha ukame tunaamini kwamba visima vyetu tulivyo navyo ambavyo tunavitegemea ikiwa visima vya *drill* vya kupata maji ambayo yenye kima kikubwa cha chini ya ardhi au visima vya kawaida

tunavyovitumia majumbani kutokana na jua kali na joto jingi. Hii inaonesha kwamba maji yataanza kupungua kwenye visima.

Mhe. Spika, kwa hivyo kuongezeka kwa joto la bahari, joto hili halipo nchi kavu tu lakini hata katika bahari ambayo yote ni sehemu ya mazingira ya bahari ambapo tunaamini joto likiongezeka samaki wanaanza kukimbia, matumbawe yanaharibika baharini, majani ya wanyama hawa yanapotea, mazalio ya samaki vile vile yanaharibika. Kwa hivyo viumbe hai vinapata taabu na kukimbia. Hii yote ni kuonesha hali halisi ya hali ya tabia nchi ilivyokuwa imeshabadilika.

Mhe. Spika, tukiangalia ikiwa hali ni namna hiyo samaki wanakimbia, ina maana hata watu wetu wanaovua samaki watapata shida katika kupata samaki kwa wingi, kwa sababu samaki wanakimbia wanakwenda bahari kuu. Kwa hivyo hili ni moja katika tatizo vile vile.

Mhe. Spika, tunaona fukwe zetu zilivyokuwa zimeharibika kwa kima cha maji kupanda juu. Miti mingi inaanguka na maji ya chumvi yameanza kuhujumu sehemu za kilimo. Maji yameingia ndani.

Unguja na Pemba kwenye ufukwe wa bahari, ukiangalia katika visiwa viwili; kisiwa cha Unguja kimaumbile ni tofauti na kisiwa cha Pemba kimaumbile. Kisiwa cha Unguja *coastline* yake ya baharini au ufukwe wa bahari umekwenda vizuri. Hauna mambo ya kuingia ndani na kutoka nje sana, lakini ukiangalia kisiwa cha Pemba *geographically* utakuta kisiwa cha Pemba kina *in and out handlines* ambayo yanaingia maji ya chumvi ndani sana. Kwa hivyo hizo ni moja katika athari kubwa sana, kuangalia mazingira ya kisiwa cha Pemba na mazingira ya kisiwa cha Unguja.

Mhe. Spika, hii hali inavyoonesha ni kwamba hata mwisho maeneo yetu ya makaazi yanaweza kuathirika kwa maji ya chumvi. Tuangalie kwa nchi za wenzetu kama ni Holland unakuta usawa wa bahari na ardhi yenyewe ni sawa sawa. Kwa hivyo wao wanatengeneza mazingira ya kuishi kwa kutembea na vyombo ndani ya maji yale na kufika katika maeneo yao ya makaazi.

Lakini sisi kwa mazingira ya kisiwa chetu, sehemu ambazo ardhi ni sawa sawa na usawa wa bahari matumainio ya maji ya chumvi yataingia kwa wingi. Sisi wengi tunaoishi katika visiwa hivi tunategemea ardhi kwa ajili ya Kilimo. Sasa haya yote niliyokuwa nimeyazungumza, uhaba wa mvua, athari ambayo inapatikana katika kilimo wakati wa jua kali uzalishaji unakuwa mdogo, maji ya chumvi kuingia ndani ya kisima, maji ya chumvi kuharibu fukwe na miti kuanguka mpaka katika maeneo ambayo watu walikuwa wanaishi, hata makaburi nayo yanachukuliwa na maji. Kwa hivyo hili ni suala zito na gumu sana.

**Mhe. Spika:** Mhe. Mjumbe una dakika tatu.

**Mhe. Suleiman Hemed Khamis:** Mimi ninataka nimuulize Mhe. Waziri, kati ya haya yote je, ni jitihada gani ambayo Wizara yako imechukua kulisaidia taifa hili.

Suala jengine Mhe. Spika, ambalo nataka nimalizie la mwisho, ni suala la watu wenye ulemavu. Tumeambiwa hapa kwamba usajili umefanyika na tuna watu hawapungui 6,445, lakini hatukupata uchambuzi wa watu hawa, hawa ni kwa kijumla hatukuambiwa miongoni mwa hawa 6,445 wanaume ni wangapi na wanawake ni wangapi na watoto ni wangapi. Hapa asili ya kutaka kujua idadi hii, ni kutaka kuwachambua hawa watu kwa sababu wametajwa kiujumla, miongoni mwao pengine kuna watoto na wameathirika kimaumbile. Kuna wengine ambao wanahitaji kuchukuliwa hatua za kiserikali, kwa sababu ni wadogo labda wanahitaji kupata elimu, na elimu yao wataipata vipi hawa ambao wana ulemavu na hawa watu wa kati na kati je wanakwenda vipi.

Kwa hivyo, hizi haki za walemavu katika sheria zikoje. Mikataba ya kimataifa kwa mfano inawasaidiaje walemavu, kwa sababu wao wana imani sana na watu wenye ulemavu. Je, hii mikataba ambayo tunasikia kuna sheria, kuna mambo kadhaa inawasaidia kwa kiasi gani walemavu. Tumeambiwa hapa kuna jumuia kiasi tisa za walemavu na wanapata ruzuku. Je, wanapata ruzuku ya namna gani, kwa mfano wanasaidiwa vifaa, ok zaidi ya hilo ni lipi jengine. Umeshamsaidia yeye kuweza kutembea je, huyu mlemavu hataki kula, tunamsaidia vipi kwani hataki elimu, tunawasaidia vipi katika elimu.

Kwa hivyo, kutokana na idadi hii basi ningeshauri kwamba paandaliwe utaratibu maalum kwa hawa kuweza kuwagawa na tukawajua. Wangapi wanastahili kwenda skuli, na aina gani ya skuli ambayo walemavu hawa wanahitaji kupelekwa, halafu tuweze kujua kama kuna vijana wenye uwezo wa kufanya kazi je, tumewaandalia kazi gani vijana hawa ya kuwapa, kwa sababu tunawaona wanazunguka ndani ya miji hii, kigari amepata lakini bado anaendelea kuzunguka katika mji kuombaomba, hii ombaomba itaendelea mpaka lini kwa walemavu. Tunataka tusiwaone walemavu ndani ya miji kwenye vigari vyao wanaomba. Hawa ni watu ambao wana uwezo, mikono yao ni mizima, hivyo watafutiwe kazi za kuweza kufanya, hata kama ni kazi za kupaka rangi, kusuka mikeka, kutengeneza kamba na mambo mengine. Kwa hivyo, utaratibu uweze kuandaliwa kwa ajili ya maisha yao.

Mhe. Spika, naheshimu wakati wako na ninakushukuru kwa kunipatia nafasi, ahsante sana.

**Mhe. Bikame Yussuf Hamad:** Ahsante Mhe. Spika. Kwanza sina budi kuchukua fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia kukutana hapa tukiwa ndani ya hali ya uzima na afya njema. Tunamuomba Mwenyezi Mungu kama kuna wenzetu wana matatizo, basi *Inshaallah* Mwenyezi Mungu awatatulie matatizo yao na awape wepesi ili mara nyengine tushirikiane.

Mhe. Spika, pia nataka nichukue fursa hii ya kumpongeza Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais, pamoja na watendaji wao wote, kwa kutuletea hotuba ya kitabu hiki cha bajeti ya wizara yao hii.

Vile vile napenda nichukue fursa hii Mhe. Spika, niipongeze wizara hii kwa juhudi zao kubwa walizozifanya katika kuondoa matumizi ya utumiaji wa mifuko ya plastiki, naona kwa kiasi fulani wamefanikiwa kwa suala hili.

Mhe. Spika, nianze mchango wangu kwa kuzungumzia suala la mazingira, lakini pia na dawa za kulevya. Mhe. Spika, Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais, ina majukumu makubwa kama alivyotangulia Mhe. Suleiman Hemed kulizungumzia, kuwa ina majukumu makubwa ambayo yanaikabili nchi yetu. Kwa sababu ukizungumzia dawa za kulevya, watu hawanyanyukii moja kwa moja kwenye dawa za kulevya. Lakini hunyanyukia watoto wadogo kuanza mambo ya uvutaji wa sigara na bangi, ndio hatimaye hupelekea katika mwelekeo huo wa kuelekea katika dawa za kulevya.

Mhe. Spika, mimi ningemuomba Mhe. Waziri kwa hili. Kuna hivi vitengo vya polisi jamii, basi ningemuomba Mhe. Waziri vitengo hivi ashirikiane navyo kikamilifu. Kwa sababu polisi jamii ukienda katika mazingira, kama ukataji wa miti, basi polisi jamii aliyeko kwenye shehia, ndiye atakayejua katika maeneo ya mwituni nani anayefanya vitendo hivyo. Ikiwa ni dawa za kulevya vile vile, ni mtoto gani pengine anayeanza kunyanyukia kuvuta sigara, na pengine hajafikia kiwango na pia ni watoto gani ambao wanaanza kujishirikisha na masuala ya uvutaji wa bangi.

Kwa hivyo, ndio nikataka kumuomba Mhe. Waziri katika masuala yake haya, basi namuomba sana. Ingawa anasema kuna kamati wameshaunda katika shehia na wilaya. Lakini pamoja na kamati hizo, mimi ningekuomba kwa kupitia vitengo hivi vya polisi jamii, basi uwe navyo bega kwa bega. Kwa sababu kuna mifano mizuri hasa katika vijiji vyetu, maeneo ya vijijini. Kuna mifano mizuri inayojitokeza sasa hivi, watoto wengi wamepungua zinapofika skukuu hutembea mpaka saa 5:00 za usiku, lakini hata kwenye mabanda ya video, watoto wamepungua sana kwenda katika mabanda ya video, kwa kupitia vitengo hivi vya polisi jamii.

Kwa hivyo, ningekuomba Mhe. Waziri ushirikiane na vitengo hivi, tena usijekutafuta vitengo hivi ukatafute wale ukasema pengine wanataka wale watu wasomi. Mtafute yule anayekwenda pwani na yule anayekwenda maporini kuchunga, basi yule ndiye atakayeona mazingira yanaharibiwa vipi, anayekwenda pwani ndiye atakayeona mikoko inakatwa vipi, na watu wa aina hii ndio utapata taarifa zao nzuri. Kwa hivyo, katika masuala haya Mhe. Waziri ningekuomba sana uvitizame hivi vitengo vya polisi jamii. Kama kuna shehia ambazo hawajaunda vitengo hivi vya polisi jamii, kwa sababu kuna vijiji vyengine hawataki kushiriki kuunda vitengo hivi, kwa sababu wanaona wanafanyiwa kero. Lakini vitengo hivi ni vizuri sana, na katika vijiji vyetu vingi vimeshaonesha mfano mzuri wa upunguaji wa mambo kadhaa ambayo sio ya msingi.

Vile vile Mhe. Waziri kuna hiki kitengo maalum cha polisi kinachopambana na dawa za kulevya, ambacho kiko pale uwanja wa ndege na bandarini. Lakini Mhe. Spika, pia kuna bandari zetu ndogo ndogo, hivyo kwa kupitia hawa KMKM ningekuomba Mhe. Waziri na hawa nao muwaangalie vizuri sana, ili wafanye kazi zao vizuri na waweze kuepukana na kuchukua rushwa. Mhe. Waziri unapowafanyia bajeti yao vizuri na mkawa na mashirikiano mazuri, na wao basi pia watakuwa ni mfano mzuri wa kutafuta masuala haya yanayohusiana na dawa za kulevya.

Mhe. Spika, niende katika suala zima la watu wenye ulemavu. Suala hili ni muhimu sana na wao wakiwa ni binadamu kama binadamu wengine wanatakiwa wapatiwe haki na fursa katika wajibu wao. Mhe. Spika, kuna suala zima ambalo bado hapa Zanzibar kuna majengo mengi hayakidhi haja kwa watu wenye ulemavu, na suala hili husemwa mara kwa mara humu Barazani, lakini tunaona halipatiwi ufumbuzi. Kwa hivyo, Mhe. Waziri tunakuomba hili suala zima la watu wenye ulemavu na majengo yetu tunayojenga, likiwemo hata hili la Baraza la Wawakilishi, hayakidhi haja. Kuna watu wengine huendea matako, na kuna watu wengine wana maumbile mbali mbali Mwenyezi Mungu aliyowajaalia. Kwa hivyo, hili nalo lizingatiwe, sio mtu ana haja ya ofisi gani basi apande magazi mpaka umuone roho inamtoka, sio jambo zuri hilo. Kwa hivyo, tunaziomba wizara ambazo ni za serikali na majengo yao hayana *lift*, basi wizara zile zilazimishwe kujenga *lift*, ili wale watu wenye ulemavu na wao wapate fursa ya kwenda katika wizara zao.

Mhe. Spika, watu hawa wenye ulemavu, serikali ina kitengo hiki cha wazee wale ambao hawajiwezi, serikali imechukua juhudi ya kuwawekea pahali ili kuweza kuwahifadhi wazee wale katika mazingira mazuri. Mhe. Waziri kuna ulemavu wa kila aina, kuna ulemavu mwengine mfano wake ni kama uzee, hawajiwezi. Kwa nini wizara yako haifanyi mpango wa kutafuta wale wazee ambao hawajiwezi kuwaweka pahali pamoja, katika misingi ya kuwasaidia na wao na kuna ulemavu mwengine hawezi kufanya chochote. Kwa hivyo, na hili Mhe. Waziri nalo ulione kwamba kuna walemavu wa aina hiyo ambao hawawezi chochote, kwa hivyo muweze kuwaweka pahala pazuri na kuwapatia angalau chochote.

Jengine Mhe. Spika, ni suala zima la ukimwi ambalo ni moja kati ya majukumu ya Wizara hii, na ndio Wizara mama ambayo jukumu lake hilo moja. Ingawa suala hili la ukimwi liko katika kila wizara, lakini wizara hii ndio wizara mama ya kushughulikia masuala mazima ya ukimwi na maambukizi yake. Sasa kwa nini Mhe. Waziri mimi sijaona katika hiki kitabu, pengine tathmini ya suala hili zima la ukimwi ukatueleza, kuna wilaya gani, kuna shehia gani, ambayo pengine yameongezeka matatizo haya. Kwa sababu wengine sio waangaliaji wa TV, na wala sio wasikilizaji wa redio, lakini kwa kupitia Baraza hili, watu wengi wanahamasika kufuatilia kusikiliza hivi vikao. Sasa ungetupa tathmini, na ile tathmini inapotoka basi watu itawasaidia wakajua kumbe pahala fulani ndio mambo haya yalioko, basi anaanza kujenga hofu na akawa na tahadhari kubwa, lakini pia tukapata tathmini ya kuwa hili suala linaongezeka, hili suala la ukimwi linapungua katika asilimia ngapi. Wewe ndio Wizara yako ya kuweza kutupa tathmini hii ili tukaweza kujua nini cha kufanya.

Mhe. Spika, kwa hayo machache na kwa niaba ya wanawake wenzangu wa Wilaya ya Micheweni, naunga mkono hotuba hii kwa asilimia mia kwa mia.

**Mhe. Amina Iddi Mabrouk:** Ahsante sana Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi ili na mimi niwe mmoja wapo wa kuweza kuchangia hotuba ya Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais.

Awali ya yote kwanza nichukue fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu ambaye amenijaalia kusimama hapa mbele ya Baraza lako tukufu nikiwa mzima na afya njema. Pia nichukue nafasi hii kwa dhati kabisa kumpongeza Mhe. Waziri hasa kwa vile mwanamke mwenzangu kwa kuweza kutekeleza majukumu yake, naamini kwamba kumbe wanawake tukiwezeshwa tunaweza. Pia akinamama sisi kwa kweli huwa makini na waangalifu sana katika kutekeleza majukumu yetu.

Vile vile Mhe. Mwenyekiti, niwapongeze watendaji wake ambao wameandaa hotuba hii, naamini kwamba kama ikitekelezwa kama yalivyoandikwa humu katika kitabu hiki, basi naamini kwamba nchi yetu itapiga hatua kubwa ya maendeleo. Baada ya pongezi hizo Mhe. Spika, sasa niingie katika kitabu hiki cha Mhe. Waziri.

Mhe. Spika, nianze katika ukurasa wa 16. Mhe. Spika, mimi nachukua nafasi hii ya dhati kabisa kuipongeza serikali kwa kuweza kudhibiti mifuko ya plastiki. Kwa kweli siku za nyuma ilikuwa kama utakwenda katika masoko yetu, basi kuna watu wachache ambao walikuwa wanauza mifuko hii kwa kinyemela. Lakini sasa hivi serikali yetu imeweza kufuatilia na kuhakikisha kwamba inazuia kwa kiwango kikubwa uingiaji wa mifuko hii ya plastiki. Hata kama utapita njiani zamani ulikuwa unaikuta mifuko hii ya plastiki inapeperushwa na upepo. Lakini sasa hivi unaweza kwenda hatua nyingi hukutani na mifuko ya plastiki.

Mhe. Spika, bado lipo tatizo kubwa ambalo serikali yetu haijaweza kudhibiti, tatizo hilo ni uchimbaji wa mchanga. Uchimbaji huu wa mchanga bado ni tatizo kubwa katika nchi yetu na kama Mhe. Waziri utapita katika maeneo ya

makaburini pale Mwanakwerekwe, kwa kweli hakupitiki. Mhe. Spika, makaburi karibu yatafufuliwa maiti kwa sababu ya uchimbaji wa mchanga, na tunaamini kwamba uchimbaji wa mchanga ni tatizo kubwa la uharibifu wa mazingira yetu. Mhe. Spika, namuomba Mhe. Waziri na ninakuamini sana, hivyo tatizo hili la uchimbaji wa mchanga ufanye kazi maalum ya kudhibiti uchimbaji wa mchanga katika taifa letu.

Mhe. Spika, nikiendelea nije katika ukurasa wa 24. Mimi binafsi nichukue nafasi hii ya dhati kuipongeza serikali yetu, kwa namna ilivyochukua hatua ya kusajili watu wenye ulemavu. Kitabu hiki kimetuambia kwamba katika mikoa miwili ya Pemba imeweza kusajili watu wenye ulemavu 6,445. Kati ya hao wanaume ni 3,556 na wanawake ni 2,878.

Mhe. Spika, serikali imepiga hatua kubwa na kujua takwimu sahihi itasaidia serikali kupanga mipango yake vizuri ya maendeleo. Hata hivyo, namuomba Mhe. Waziri atakapokuja kufanya majumuisho, basi atuambie takwimu ya Unguja katika mikoa yetu hii ya Unguja ina takwimu ya watu wenye ulemavu wangapi.

Pia namuomba Mhe. Waziri na serikali kwa ujumla ihamasishe jamii, kwa sababu bado jamii yetu iko nyuma kwa baadhi ya wananchi, hususan kinamama wenzangu ambao wanawaficha watoto wenye ulemavu. Mimi namuomba Mhe. Waziri atumie vyombo tofauti vya habari, ili kuwaelimisha wananchi kujua kwamba mtoto mwenye ulemavu sio sahihi kumficha ndani. Mimi nachukua fursa hii kuipongeza serikali na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, kwa kuona kwamba sasa ipo haja kwa watoto wenye ulemavu tofauti kuwapatia elimu.

Mhe. Spika, naamini mtoto unapomtoa akienda kujumuika na wenziwe, basi hata ile akili yake inakua vizuri. Lakini unapomuweka ndani ukamficha, kwa kweli mtoto yule unazidi wa 27. Mimi binafsi naomba nichukue nafasi hii kwanza kuipongeza serikali kwa jitihada zake ambazo inazichukua za kutafuta mbinu mbadala za kuwatibu vijana wetu hawa ambao tayari wameathirika na dawa za kulevya.

Hata hivyo, Mhe. Spika, serikali naiona inatumia nguvu kubwa katika kutibu vijana wetu ambao tayari wameathirika na dawa za kulevya, lakini bado haitumii nguvu kubwa katika kudhibiti uingiaji wa dawa za kulevya. Mhe. Spika, kwa kweli tatizo hili la uingizwaji wa dawa za kulevya lipo kubwa na linaendelea kuongezeka.
Mhe. Spika, njia kubwa ambazo dawa hizi zinaingizwa ni njia mbili. Njia ya kwanza ni uwanja wa ndege na bandarini. Sasa mimi namuomba Mhe. Waziri na nimpongeze sana, kwa sababu hivi juzi alijibu swali linalohusiana na dawa za kulevya na akatuthibitishia kwamba Zanzibar tumepata choo, ambacho mtu anapopita uwanja wa ndege na halafu taasisi zinazohusika na dawa hizo kama zikiwa zinamshuku mtu kuwa kabeba dawa za kulevya, basi choo kile kinaweza kusaidia kwa kumpeleka mtu yule.

Mhe. Spika, lakini kwa masikitiko makubwa Mhe. Waziri alisema kwamba taarifa zile yeye binafsi anaona kwamba kinachelewa kutiwa choo kile na aliiandikia barua Wizara ya Makamo wa Pili wa Rais. Mimi naipongeza Wizara hii ya Makamo wa Pili wa Rais, kwa sababu Mhe. Waziri wa Makamo wa Kwanza wa Rais alisema kwamba alijibiwa na Waziri wa Makamo wa Pili wa Rais kwamba yeye aliiandikia barua polisi na mpaka hivi sasa polisi haijatoa jibu. Kwa hivyo, Mhe. Spika, naomba nichukue fursa hii ili niwaombe hawa Mawaziri wawili washirikiane ili kuhakikisha kwamba choo kile kinawekwa pale panapostahiki.

Mhe. Spika, si hivyo tu, lakini njia hizi mbili ambazo nimezitaja awali ambazo zinapitisha hizi dawa za kulevya, inaonekana pia pengine hata yule mtu ambaye amebeba hizo dawa za kulevya, basi utaalamu wetu ni mdogo. Hatuna vyombo ambavyo ni vya kumtambua mtu yule kuwa amebeba. Kwa hivyo, naomba serikali tujitahidini ili kuhakikisha kwamba tunaweka vyombo vya kisasa ambavyo vinaweza kumtambua mtu ambaye amebeba dawa za kulevya.

Vile vile Mhe. Spika, niiombe serikali bado tatizo lipo la mahakama zetu, kwa sababu wakati mwengine mtu anakamatwa na dawa za kulevya wazi wazi, lakini kesi inapopelekwa mahakamani baada ya muda ushahidi unakuwa haupatikani. Mimi naipongeza Idara yetu hii ya Mkemia Mkuu, kwa kweli inafanya kazi vizuri na dawa zile zinapopelekwa kule zinapimwa na matokeo yake Idara hii ya Mkemia Mkuu inapeleka, lakini hatimaye na kwa masikitiko makubwa inaonekana kwamba kesi ile inapokwenda mara siku ya pili unapelekwa unga mwingine ukapimwe, wakati awali umeshapelekwa unga ule na majibu yameshatoka. Kwa hivyo, naiomba serikali labda tutafute mbinu mbadala ya kuhakikisha kwamba hizi kesi zinakwenda haraka. Mkemia Mkuu keshapima na keshatoa jawabu, naomba basi isiwe kurejea rejea unga ule kupelekwa kupimwa, hii ndiyo inayosababisha kwamba

unga ule baadae unaambiwa sio unga halisi wa dawa za kulevya, unaambiwa ni unga wa muhogo. Kwa hivyo, naiomba serikali kudhibiti uingizwaji wa dawa za kulevya.

Pia Mhe. Spika, vijana wetu hawa wameathirika kwa kiasi kikubwa na dawa za kulevya. Waheshimiwa Wawakilishi kama tutafanya ziara kwa kupitia Mlandege na Miembeni, kwa kweli vijana tutawakuta wanayoyoma na wameshaathirika na dawa za kulevya. Kwa hivyo, naomba tuchukue jitihada hii, ili kuhakikisha kwamba dawa hizi haziingizwi nchini.

Mhe. Spika, mimi nichukue fursa hii kupongeza hawa walioianzisha *sober houses*. Mhe. Spika, kwa kweli *sober houses* imetusaidia sana vijana wetu kwa kuhakikisha kwamba wanawachukua vijana hawa na kuwaponyesha. Mhe. Spika, mimi naiomba serikali kwamba pamoja na kuwepo kwa hizi taasisi binafsi ambazo zimejitolea kuanzisha *sober houses*, lakini kama serikali tuna wajibu mkubwa na sisi kuanzisha *sober houses* yetu, kama serikali za nchi jirani zilivyofanya. Naamini kufanya hivi kwa kweli itawasaidia sana wale vijana ambao pengine familia zao hazina uwezo, hivyo tuhakikishe kwamba tunawanasua katika tatizo hili.

Mhe. Spika, niendelee na mchango wangu niende katika Idara ya mazingira. Mhe. Spika, Idara ya mazingira nilikuwa tayari nimeshaitaja. Kwa hivyo, kwa sababu nataka niuokoe muda wako naomba niseme kwamba naiunga mkono hotuba hii ya Mhe. Waziri wa Wizara ya Makamo wa Kwanza wa Rais kwa asilimia mia juu ya mia, ahsante sana Mhe. Spika.

**Mhe. Farida Amour Mohammed:** Ahsante Mhe. Spika, kwa kunipa fursa hii ya kuchangia machache katika hotuba ya Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais.

Mhe. Spika, kwanza naomba nimpongeze Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais, pamoja na watendaji wake kwa jinsi walivyoitoa hotuba yao nzuri na yenye kuleta matumaini kwa wananchi wa Zanzibar.

Mhe. Spika, nianze mchango wangu moja kwa moja kwenye suala la mazingira. Mhe. Spika, uharibifu wa mazingira umeenea ndani ya Zanzibar yetu hii, kwenye ukataji wa miti, uchimbaji wa mchanga na ukataji wa matofali. Katika ukataji wa matofali na uchimbaji wa mchanga, tayari watu hao wachimbaji wameshapewa maelekezo mazuri, baada ya kuchimba wafukie yale maeneo yake ili yajirudi katika hali yake ya kawaida.

Mhe. Spika, kwenye suala la bahari, kuna watu wanakata mikoko kwa ajili ya kufanya kuni. Lakini wakati huo huo kuna wananchi wetu wamejitolea kwa nguvu zao zote kupanda mikoko kwa ajili ya kulinda mazingira yetu yasichafuke. Kwa hivyo, hapa nataka nimuombe Mhe. Waziri kwamba watu wale waliojitolea kufanya kazi katika mazingira magumu, na ambao ni wanawake kwenye kupanda mikoko na ni wanawake ambao wako katika Wilaya ya Wete ndani ya Jimbo la Mtambwe, huwa wanafanya kazi katika mazingira magumu na hawajawahi kumuona kiongozi kwenda kuwatembelea, na kuwapa nguvu tu kidogo na moyo wa kufanya ile kazi, kwa sababu ile kazi wanaifanya ni kubwa na ni nzuri. Mimi mwenyewe binafsi nilishawahi kwenda kuwaona. Kwa hivyo, nakuomba Mhe. Waziri katika hili uwaone wanawake wale katika Jimbo la Mtambwe wanaojishughulisha na kupanda mikoko, ili kuhifadhi mazingira yetu ya bahari. *(Makofi)*

Nikiendelea na mchango wangu sasa nizungumzie kuhusu suala la UKIMWI. Mhe. Spika, serikali inatumia fedha nyingi sana katika nyanja na taasisi zote kwenye mambo ya UKIMWI. Kwa kweli bajeti zote za serikali zinazokuja hapa Baraza la Wawakilishi kuna kifungu cha UKIMWI na kila pahala inaonesha fedha nyingi sana zinatumika kwa ajili ya UKIMWI.

Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Spika katika kutumika fedha hizi nyingi sana katika masuala ya UKIMWI, tujue ni kiasi gani cha watu waliopatikana katika hali ya kupungua kwa UKIMWI, maana yake isiwe fedha nyingi zinatumika kwa mambo mengine, lakini ukitizama UKIMWI bado unaendelea.

Mhe. Spika, mambo ya kuwaweka watu wetu wenye UKIMWI kudhalilisha, kutengwa na kuwekwa sehemu ya peke yao ile imeondoka na tunakwenda nao vizuri. Lakini tunataka tupate tathmini ya huu UKIMWI umepungua kiasi gani baada ya muda mrefu serikali, taasisi binafsi pamoja na wafadhili na wahisani kutoa fedha nyingi kwa ajili ya kusaidia Kitengo cha UKIMWI.

Vile vile naomba nizungumzie kuhusu suala la watu wenye ulemavu. Mhe. Spika, walemavu kama wenzangu walivyotangulia kwamba miundombinu ya walemavu bado haijakamilika vizuri, kwa sababu taasisi nyingi walemavu wanashindwa kuingia kwenye maeneo.

Mhe. Spika, kuna walemavu wa aina nyingi Mhe. Waziri. Kwa mfano, kuna walemavu wengine hawajiwezi na wala hawatoki na wale wazazi wao ndio wanaokuwa ni walemavu. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Spika kwenye tathmini yake ya kupita na kusajili walemavu, kuna maeneo mengine kama vile vijiji ndani sana hawajasikia. Vile vile kuna wazazi wengine kutokana na hali ya wale watoto wao ya ulemavu walivyo wanaona tabu wao wenyewe hata kuwapeleka.

Mhe. Waziri namuomba sana kupitia kwako Mhe. Spika, kwamba ashirikiane na taasisi husika zilizomo vijijini ndani ya shehia wakiwemo Masheha, Madiwani kwa ajili ya kufanya tathmini na kuweza kusajili hasa na kujua ni walemavu wangapi na wa aina gani waliomo katika maeneo, kwa sababu bado wamo wengi.

Mhe. Spika, katika walemavu hao bado kuna udhalilishaji. Lakini naipongeza sana serikali kwa sababu ya kuwalea walemavu. Kwa kweli bado kuna wenzetu ambao ni makatili wanawadhalilisha sana walemavu tena watoto. Kwa mfano, unaweza kumkuta mtoto mwenye ulemavu anadhalilishwa kwa kubakwa, lakini baadae kesi ile itakapokwenda Kituo cha Polisi au Mahakamani utaambiwa lazima upatikane ushahidi wa papo kwa papo na wala sirahisi kupatikana ushahidi wa aina hiyo Mhe. Spika.

Kutokana na hali hiyo, naiomba serikali ijipange vizuri, kwa sababu yule ni mlemavu ameshabakwa masikini ya Mungu na wala hajui pa kwenda na yule mbakaji tayari ameshakimbia, ametafuta sehemu nyengine ya kujificha, halafu yeye inabakia kesi ya kwenda na kurudishwa na matokeo yake haifikii pahala, hiyo ni idhilali kuwa kwa wenzetu walemavu.

Mhe. Spika, walemavu ni binadamu kama sisi na leo ni mlemavu yeye na kesho hujui Mwenyezi Mungu atakuweka vipi, kwa sababu kuna ulemavu wa kuzaliwa na mwengine wa kupata ajali, kwa hiyo lazima tuwaenzi sana hawa wenzetu walemavu, ili wapungue nahii idhilali waliyonayo. *(Makofi)*

Mhe. Spika, katika Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais Pemba, nataka nitoe masikitiko yangu kidogo. Katika kuwaenzi Viongozi wetu Wakuu wa Kitaifa, kule Pemba Mhe. Makamu wa Kwanza wa Rais hata nyumba ya kukaa hana inayotokana na serikali.

Vile vile halafu Afisa Mdhamini wetu katika Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais kwa kushuhudia kwa macho yangu nikiingia katika ziara zile kwa baadhi ya siku anaingia jikoni mwenyewe kupika, yaani hana watu maalum waliotengwa kama hawa wamepangwa katika Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais.

Sambamba na hilo hata dereva ambaye yupo maalum kwa ajili ya Makamu wa Kwanza wa Rais kwa Pemba haonekani. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri kupitia kwao Mhe. Spika, ajipange vizuri na alione kwamba Afisa Mdhamini wetu ambaye yupo Pemba ni mwanamke, lakini wapo watu wengi.

Hivyo ni vyema watafute watu maalum kwa ajili ya kutoa huduma wakati Mhe. Makamu wa Kwanza wa Rais anapoingia kule Pemba na isiwe Afisa Mdhamini mwenyewe baada ya kukaa na kusikiliza maoni, pengine mawazo na ikawa yeye ndiye kwanza aingie jikoni na baadae ndio afanye mengine na hiyo ni udhalilishaji kiasi fulani Mhe. Spika.

Mhe. Spika, katika dawa za kulevya na mimi naomba nizungumzie japo kidogo. Kwa kweli kuhusu dawa za kulevya serikali imefanyakazi nzuri ya kulinda na kuhifadhi dawa za kulevya, ili zisiingie na zinaingia kwa nyanja tofauti kama vile baharini, *Airport* na hizo ndizo nyanja kubwa wanazoziona ziko wazi.

Vile vile kuna vichochoroni, kuna vibandari vya vichochoroni Mhe. Spika dawa za kulevya bado zinaingia na dawa hizi zinawaathiri vijana wetu wengi, ambao ndio wanaopata tabu pamoja na kuathirika.

Lakini jambo la kusikitisha hatujawahi kupata taarifa rasmi kwamba yule anayesafirisha na kuingiza hapa nchi kukamatwa na kuhukumiwa pamoja na kuadhibiwa na kuona hasa huyu ameadhibiwa kutokana na kuleta dawa za kulevya, kwa sababu yule ndiye mwenye kupaswa kuhukumiwa. Sasa wale wengine wadogo wadogo wenye kuvuta

unga, ambao wao hawana uwezo wa kwenda nchi za nje na kununua au kuchukua kutoka huko ndio wanaoadhibiwa hapa.

Kwa hivyo, namuomba sana Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Spika pamoja na jitihada zake zote anazozifanya za kuzuia dawa za kulevya zisiingie nchini. Mhe. Spika, naomba japo siku moja tuambiwe kwamba huyu ameshahukumiwa kwa sababu ya kuingiza dawa za kulevya nchini na wale ndio maadui jamani, kwani wanatuumizia watoto wetu, wanakosa elimu pamoja na mambo mengine mbali mbali ya kijamii na wamekaa hawajui chochote.

Kwa kweli nawashukuru sana wale wenzetu walioamua kuweka zile *Sober Houses*. Lakini kwenye *Sober Houses* zile kuna changamoto nyingi, kwa sababu wale wanataka kutunzwa mule ndani, kama vile kuelimishwa na wameshakubali masikini ambao wale vijana wetu waliokubali kuacha dawa za kulevya, basi wanataka waenziwe sana yaani watunzwe.

Kwa hivyo, badala yake wale wakitoka nje wanakwenda kutafuta sehemu nyengine na dawa za kulevya mimi nasema ni kitandawili popote pale zinaingia Mhe. Spika. Kwa mfano, unaweza kuwakuta watu wako Gerezani wamefungwa, lakini mule ndani ya Gereza wanavuta bangi na wanakula unga wanaupata wapi na pale kuna ulinzi mkali. *(Makofi)*

Mhe. Spika, namuomba Mhe. Waziri katika hili lazima tuwe makini katika sekta pamoja na taasisi zote hasa katika vyombo vya ulinzi. Kwa kweli vyombo vya ulinzi viwe makini na visimamiwe katika kuhifadhi mambo haya.

Mhe. Spika, kwa vile mambo yote yameshazungumzwa sana na mambo yenyewe ni ya kujirudia ambayo ni masuala ya dawa za kulevya, UKIMWI na watu wenye ulemavu. Kwa hivyo, naomba kwa niaba ya wanawake wenzangu wa Wilaya ya Wete niunge mkono hotuba hii kwa asilimia mia moja. Ahsante sana Mhe. Spika. *(Makofi)*

**Mhe. Spika:** Mhe. Mjumbe, tunashukuru. Sasa naomba nimkaribishe Mhe. Saleh Nassor Juma na baadae tumkaribishe Mhe. Ismail Jussa Ladhu.

**Mhe. Saleh Nassor Juma:** Mhe. Spika, ahsante sana na mimi kunipatia fursa hii kuweza kutoa mchango wangu juu ya hoja hii iliopo mbele.

Awali ya yote hatuna budi kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa kuweza kutupa hii neema ya uhai na uwezo wa kutoka majumbani kwetu hadi hapa katika jengo hili tukufu. Kwa kweli hii ni hazina kubwa aliyotujaalia Mwenyezi Mungu na kwa vyovyote vile hatuna budi kumshukuru.

Nadhani kwa niaba ya wapiga kura wa Jimbo la Wawi nitakuwa mchache wa shukurani kama sikutumia fursa hii Mhe. Spika kukushukuru wewe na sio tu kwa kunipa nafasi ya kuchangia hii hoja, vile vile kwa umakini na umahiri wako katika kusimamia hizi hoja tunazozijadili humu ndani. Mhe. Spika, wewe ni miongoni mwa Maspika machache sana tena ni adimu sana katika Maspika Kusini mwa Jangwa la Sahara walio na umakini mkubwa kama huu. *(Kicheko/Makofi)*

Mhe. Spika, katika hili niwaombe hawa jamaa wa Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar (*SUZA*) wakupe *Degree* ya Heshima ya Uzamivu (*PhD*) katika haya mambo ya Mabunge, tutawaomba sana hawa wakutunukie kitu hicho. *(Makofi)*

Baada ya dibaji hiyo sasa niende kwenye hoja iliopo mbele yetu.
Kwanza nianze kumpongeza Mhe. Waziri pamoja na jopo letu la wataalamu likiongozwa na Katibu wake Mkuu kwa kuweza kufikiria na kutuleta hii bajeti yao. Kwa kweli nachukua fursa hii kuipongeza serikali katika hili, ni bajeti ambayo kwa kiasi fulani nadhani huko mbele nitatoa msimamo ina mwelekeo gani. *(Makofi)*

Mhe. Spika, nianze kwenye ukurasa wa 9 kwenye ibara ya 35 Mhe. Spika, naomba kunukuu kidogo.

Kitabu cha hotuba ya bajeti ukurasa wa 9 ibara 35 inaeleza hivi:-

> "Mhe. Spika, Idara imeendelea kuratibu na kusimamia utekelezaji wa miradi mitatu ya maendeleo ukiwemo mradi wa kuangamiza kunguru weusi, mradi wa usimamizi wa maji machafu Msingini Kichungwani Pemba pamoja na mradi wa kuimarisha majengo ya viongozi".

Mhe. Spika, mimi kidogo nitazungumzia hii miradi miwili ya kuangamiza hawa kunguru weusi pamoja na ule mtaro wa maji machafu unaotoka Msingini hadi Kichungwani.

Kwa hivyo, nianze na huu mradi wa mtaro wa maji unaotoka Msingini mpaka Kichungwani. Kwa kweli katika hili niipongeze serikali sana, kabla ya mradi ule mitaa ya Msingini ilikuwa ni tatizo kubwa, pale ilikuwa ikikaribia mvua basi sote tunatafutana kwa sababu jinsi ya maji machafu yalivyokuwa yakisambaa katika majumba yetu.

Sasa serikali ilipoleta mradi ule pamoja na kwamba bado haujakamilika, lakini tunashukuru kwamba afya zetu zinatengemaa sana hususan katika kipindi cha mvua.

Mhe. Spika, wakati wa kipindi cha mvua katika mitaa ya Msingini miaka kama minne au mitano iliyopita nyuma, Hospitali ya Chake Chake na hata ile ya Vitongoji tunazijaza kwa maradhi ya matumbo. Kwa hivyo, hivi sasa tunashukuru *Alhamdulillah* sihaba na Mwenyezi Mungu awajaalie mumalizie huu mradi vizuri, ili afya izidi kunawirika. *(Makofi)*

Mhe. Spika, ni vyema serikali inapofanya jambo, basi ikaangalia na wakati ujao tufanye nini, tungefanya kitu kinachoitwa *two in one*, mbili katika moja na huku tukiweza kuyaimrisha mazingira yetu pia na yale maji ambayo wameyakusanya katika kila bwawa ambalo tayari wameshayafanyia *treatment* yale maji, nadhani kuyatupa baharini ni hasara kwa kiasi fulani. Kwa mfano, wenzetu katika nchi kama vile *UAE* na nchi nyengine, yale maji wakeshakuyafanyia *treatment* wanayatumia kwa matumizi mengine.

Hivi sasa serikali yetu imo katika *Poverty Reduction and Income Generating*. Sasa maji yale Mhe. Spika yaliyokwisha kuwa *treated* pale Kichungwani badala ya kuyatupa baharini. Nadhani vyema wangeya-*store* na kuweka *Pumping Station* na kuyapeleka mwahala kama pale juu Gongomawe na huku sehemu za Simambili, ili akinamama wakaweza kujipandia mboga mboga na hata akinababa, basi ingesaidia sana maji yale yangeweza kupunguza umasikini pamoja na kuongeza kipato kwa wananchi.

Mhe. Spika, katika hili naishauri serikali kwamba ni vyema maji yale badala ya kuyamwaga baharini wanaya-*store* na kuya-*pump* katika maeneo mengine, ili tuweze kuongeza kipato na kupunguza umasikini. Vile vile nafikiri hata kwenye huu mpanga ambao nasema umefeli unaoitwa Mapinduzi ya Kilimo, basi maji yale yangesaidia kufanya masuala ya *irrigation*.

Kwa hivyo, naiomba sana serikali katika hili iangalie *long run* ya *project* hii *what is the next* kutoka pale baada ya mazingira nini kifuate na wala sio yale maji tuyamwage tu, isipokuwa tuyatafutie utaratibu mwengine. Hilo ni moja.

Mhe. Spika, nilisema kwamba nitazungumzia mambo mawili hili na lile la kuwaua kunguru weusi. Kwa kweli kunguru ni miongoni mwa viumbe alivyovileta Mwenyezi Mungu duniani, kunguru wamo katika mazingira yetu.

Wataalamu wanacho kitu wanakiita *ecosystem* na ndani ya *ecosystem* viumbe vinategemeana kwa mambo haya ya vyakula, wanaita *interdependence of food between living organism within the ecosystem*. Kwa hivyo, katika hali ya kutegemeana ndani ya *ecosystem* kuna kitu kinachoitwa *balance of nature or biological equilibrium*.

Mhe. Spika, unapokuja kusema kwamba unateketeza wewe *within the ecosystem* na kuchukua *species* moja ya mnyama na kutoka kunguru 408,000/= unawaondosha ndani ya *ecosystem*, hiyo ni *disturbance of biological equilibrium or balance of nature*. *(Makofi)*

Kwa kweli hata kama kunguru anayo madhara unapotumia *chemicals means* katika kumuondosha basi huo ni ukatili, kama vile gobole, mitego na halafu ukawapiga magongo na huo ni ukatili kwa viumbe.

Mhe. Spika, naomba kutoa ushauri katika hili tena ni *scientifically* kwamba ikiwa *population density* ya kunguru imekuwa kubwa ndani ya *ecosystem*, basi tumieni kitu kinachoitwa *predator prey relationship*, kwamba hawa

kunguru watafutiwe *natural enemy*, watafutieni maadui wao wa kimaumbile, ili waje wawale kwa ajili ya kuwapunguza ile *population* yao.

Kwa mfano, makonho kuna mnyama anayeitwa konho, yaani ni mnyama anayekula kunguru. Lakini Mhe. Spika, unakwenda kuchukua sumu na kumtilia kunguru anakufa kunguru. Sasa sumu ile itakapobururwa na maji na kwenye vyanzo vya maji na kufanya *environmental pollution* na maji yale yatanywewa na binadamu na viumbe vyengine, badala ya kwamba unatibu huku kumbe vile unatibua na sehemu nyengine. *(Makofi)*

Mhe. Spika, tunawaomba wataalamu watueleze baadaye kwamba sisi tulikuwa tukitumia *DDT* kwenye kilimo na tulikatazwa kwamba *DDT* inazalisha *pollution* na nini.

Sasa leo nimeambiwa kwamba zilikuwa zinahitajika na hapa itabidi Mhe. Waziri wakati atakapokuja naomba kupitia kwako Mhe. Spika, anipe maelezo ya kutosha katika hili, kwa sababu alisema kwamba mradi huu unahitaji shilingi milioni 50. Miongoni mwa shilingi milioni 50, zilizopatikana ni shilingi milioni 35, ni *seventy percent* ya *total estimate* imepatikana na zimetumika kwa ajili ya kununulia mitego 30 pamoja na kilo mbili za sumu kutoka New zealand.

Kwa hivyo, hizi shilingi milioni 35 nitahitaji maelezo kwamba zimetumika vipi, kwa kila mtego ni kiasi gani na na kilo moja ya sumu ni kiasi gani? Mhe. Spika, hapa ninahitaji, ili sisi tusipitishe hapa, kwa sababu kazi yetu Baraza Mhe. Spika sio kupitisha tu hizi Bajeti za Serikali na matumizi ya serikali, vile vile kuangalia matumizi mazuri ya fedha za walipakodi wa nchi hii na hiyo ndio *role* yetu pia. *(Makofi)*

Sasa leo unaponiambia shilingi milioni 35 umetengeneza mitego 30 pamoja na kununua kilo mbili za dawa kutoka New Zealand, bado sijafahamu vizuri tena naomba ufafanuzi wa kutosha Mhe. Spika, ili baadae nije niunge mkono hoja ya Mhe. Waziri. *(Makofi)*

Mhe. Spika, katika hili naishauri serikali kwamba kuua kunguru 408,000 kwa kutumia sumu ni kuharibu mazingira, kwa sababu munaua kunguru, lakini ile sumu itadhuru viumbe vyengine na hilo ni tatizo. Kwa hivyo, ninachoshauri hizi shilingi milioni 35 mungekwenda kununua makonho sehemu za Afrika Magharibi ambapo wanapatikana sana, ambao wanakula hawa kunguru na baadae wata-*balance* ile *ecosystem.*

Vile vile napenda kushauri jambo jengine kwamba hawa watu wa-*contact* wa wataalamu, kwa sababu tatizo la hawa kunguru kama ni *population density* inaongezeka, basi kuna dawa unaweza kutumia hawa wasizae na ku-balance *population density* kwa kuwawekea pengine *estrogen* wakawa wanakula wala hawafi na huku hawazai na akeshakupea atakufa basi na wale wanaendelea kuwepo. *(Makofi)*

Lakini kufanya ukatili wa kuua wanyama ni tatizo kubwa hata Mwenyezi Mungu katika hili, kwa sababu unapoua kunguru laki 4 ni tatizo na hata Mwenyezi Mungu atakuwa hayuko radhi. *(Makofi)*

Nikiendelea na mchango wangu sasa nizungumzie kuhusu suala la mazingira. Mhe. Spika, mazingira ikiwa tutatumia vizuri mazingira yetu, basi yatakuwa rafiki na sisi, lakini mazingira unapoyatumia vibaya basi yanakua adui wa binadamu. Kwa kweli hii nadhani ni tanbihi ambayo inahitajika sana Mhe. Spika kwa wananchi na hata serikali yetu iliopo madarakani, kwamba lazima tuyatumie vizuri mazingira yetu kwa ajili ya kuwa rafiki.

Mhe. Spika, inasikitisha kwamba serikali yenyewe ina muhali katika kusimamia masuala ya mazingira. Kwa mfano, inaona hapa mazingira yanaharibika, lakini serikali inakuwa na muhali. *(Makofi)*

Mhe. Spika, kama unalijua Jimbo la Wawi kuna kiwanda ambacho kimejengwa katikati ya mji wa Wawi kinaitwa Kiwanda cha Makonyo. Kwa kweli ukienda kuangalia *air pollution* iliopo kipindi hiki cha uzalishaji wa mafuta ya makonyo pale inasikitisha mno, tumepiga kelele zamani, sasa nadhani hata baadae tutaendelea kupiga kelele, lakini serikali itaendelea kuziba masikio.

Mhe. Spika, kile kiwanda pale ni tatizo mimi nadhani kwa sababu ametoka Mhe. Mohammed Aboud Mohammed pale labda wanaona ni muhali kumuondoshea. Nadhani Mhe. Mohammed Aboud Mohammed au Mheshimiwa

mwengine yeyote ambaye ni mzawa wa pale basi watusaidie kile kiwanda na yale majengo yabakie pale, lakini kiwanda watuwekee kule *countryside* ya kile kisiwa. Kwa mfano *Eastern Belt* kule Makaani na wala hakuna makaazi ya watu, kule wazalishe na yale ma-*godown* yao watatumia pale.

Lakini ninachokuhakikishia Mhe. Spika, kiwanda cha Makonyo hivi sasa ni tatizo na kinaathiri sana mazingira ya pale Wawi kiasi ambacho kama unaweka maji usiku kipindi cha uzalisha kwenye dumu na kuliacha wazi, basi ukija asubuhi maji yale yote yameshakuwa meusi na hilo ni tatizo. Sasa ikiwa maji ni hivyo, je yakiingia kwenye damu au ubongo wa binadamu itakuwaje Mhe. Spika, nadhani ni madhara.

Mhe. Spika, serikali hii ni sikivu na hizo awamu za mwanzo tulizishauri sana na kusema aaa! Pale panatoka muasisi panatoka Biti Fihimu na tukakiacha pale. Lakini naamini serikali hii itanisikiliza na kiwanda kile kukihamishia pengine na yale pale kutumia kama ma-*godown* yao.

Mhe. Spika, nafikiri serikali iwe makini katika kusimamia mazingira. Kwa kweli mambo ya tabia ya nchi, kwa mfano hivi sasa tuliambiwa juzi na jamaa wa MKUHUMI hapa katika semina waliyotupa MKUHUMI pale *Zanzibar Ocean View*, kwamba sasa maji ya chumvi yanaingia katika maeneo ya mashamba. Kutokana na hali hiyo, kuna hatari baadhi ya visiwa vikazama hapa na leo serikali badala ya kuwa *serious* katika kusimamia masuala haya ya mazingira naona inatoa maneno zaidi kuliko vitendo.

Kwa mfano, kama kuna sehemu ambayo mazingira yanaharibiwa au kuna taasisi ambayo inaharibu mazingira katika *rural area* kule Pemba ni sehemu ya vijijini. Kwa kweli vijijini tunaharibu mazingira sana na wataalamu wanasema tunafanya *poor cultivation means* na wala hatuna taaluma ya kilimo, tunakata misitu na kuchoma moto ndio tunalima, tunapanda zao moja tu hilo hilo, wanaita *monoculture*.

Tatizo liliopo ni kwamba serikali yetu haiko *serious*. Kwa mfano, juzi hapa nilipotembelea Chuo Kikuu cha Taifa Zanzibar (*SUZA*) walisema wanataka waanzishe *Department ya Agriculture Pemba Branch*, lakini bajeti yao au hawana uwezo na wamesema serikali na huu karibu ni mwaka wa tano bado hawajasikilizwa.

Vile vile *SUZA* wanataka kuanzisha *Degree* ya mwanzo katika masuala ya *Environmental Science*, lakini hawawezeshwi na serikali. Mhe Spika, kama wangeruhusiwa wale basi naamini ingekuwa ni chemchem ya kutoa wataalamu wa masuala ya mazingira na kuweza kunusuru haya mambo ya tabia ya nchi. Kwa mfano leo kwao Mhe. Haji Faki Shaali pale kisiwa chao karibu kiko hatarini nacho Kisiwa Panza kule.

Mhe. Spika, nadhani ni vyema serikali isikilize na iwaruhusu wale na kile chuo ni cha serikali na wawatengee bajeti, ili waweze kuanzisha *Department of Environment* na pamoja na *Faculty of Agriculture* kusudi kuweze kuepukana na haya mambo ya kuharibu masuala ya mazingira.

Mhe. Spika, nafikiri serikali katika hilo ingeliona na wala wasiwaone wataalamu kwamba ni watu wa kubabaisha, kwani wale ni wataalamu tena wanataaluma yao. Kwa kweli tumebahatika tumempata mtaalamu mzuri pale *Professor* Idirisa Rai anayo mambo mengi ya kutusaidia katika nchi hii, lakini tukilegalega atatukimbia yule, kwa sababu atatushauri serikali lakini hatumsikilizi, jamani *Professor* Rai atatukimbia msikilizeni na mpeni uwezo wa kuanzisha haya mambo kwa ajili ya kutusaidia nchi yetu.

**Mhe. Spika:** Mhe. Mjumbe, umebakiwa na dakika tatu.

**Mhe. Saleh Nassor Juma:** Mhe. Spika, nimalizie na suala la walemavu. Kwa kweli hivi sasa walemavu ni *International Issue*, ulimwengu mzima sasa una-*advocate disabilities* na sisi tumesaini Mkataba wa Haki za Binadamu, hawa ni binadamu sawa na binadamu yoyote katika nchi hii.
Sasa Mhe. Spika, Baraza lako linatakiwa liwe mfano wa kuwathamini walemavu, lakini hivi sasa akija mlemavu wa viungo hawezi kwenda sehemu ya Mshika Fedha mpaka aletewe chini, yaani hawezi kuipanda ile ngazi.

Mhe. Spika, nilidhani kwamba Baraza lako lingeweka kiti pale mbele kwa wale wanaotumia Lugha za Ishara. Kwa mfano, anaweza kuja hapa mtu ambaye ni kiziwi na kiti chake kiko wapi huyo mkalimani pale, yule wa kufahamisha kwa lugha za ishara na wala tusiwe *bias* katika mambo, kwa sababu Baraza lako Mhe. Spika linatakiwa liwe mfano. *(Makofi)*

Aidha Mhe. Spika, leo hii kama tutapata Mhe. Mwakilishi ambaye ni mlemavu wa macho nataka nikaoneshwe *braille mashine* imo ya kutayarishia *order papers* za kupapasa zile. Kwa hivyo, Mhe. Spika naomba katika hili ofisi yako iwe ya mfano katika kutunza na kuthamini mambo haya ya walemavu, ili serikali iige hapa na sisi tuwe darasa. *(Makofi)*

Kutokana na hali hiyo, ni matarajio yangu Mhe. Spika tukija katika Baraza lijalo wale watu wa Lugha za Ishara watakuwepo pamoja na *braille machine* japo *standby braille machine* itakuwepo pale. *(Makofi)*

Mhe. Spika, kwa heshima na taadhima mimi mwenyewe binafsi na kwa niaba ya wapiga kura wa Jimbo la Wawi naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**Mhe. Ismail Jussa Ladhu:** Mhe. Spika, naomba nianze kwa kumshukuru Mola wetu mtukufu kwa kutujaalia tena na tena kukutana hapa kujadili masuala yanayohusu maendeleo ya nchi yetu na watu wake. Nikushukuru wewe Mhe. Spika, kwa kunipatia nafasi hii kwa mara nyengine tena katika mfululizo wa mkutano wa bajeti kwa mwaka huu 2012/2013 na mimi nitoe maoni yangu mara hii kuhusiana na Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais. Mhe. Spika, niruhusu nimpongeze Mhe. Waziri kwa uwasilishaji fasaha wa hotuba yake alipokuwa akitusomea jana hapa. Baada ya utangulizi huo Mhe. Spika, sasa naomba nende moja kwa moja katika hotuba hii.

Naomba nianze na Idara ya Mipango Sera na Utafiti kwenye ukurasa wa 9 na wa 10 pale Mhe. Spika, pamezungumzwa mradi wa kuangamiza kunguru weusi. Hili Mhe. Spika, ninaomba Waziri akija anipatie maelezo kidogo atapokuja kufanya majumuisho. Mhe. Spika, kwa mujibu wa maelezo haya ni kwamba fedha ambayo imeingizwa ni shilingi 35,000,000 kati ya 50,000,000 zilizokuwa zimepangwa kama mchango wa Serikali kama asilimia 70. Lakini ukiangalia mafanikio ya mradi ni kwamba kunguru walioangamizwa ni 11,596 kati ya makadirio ya kuangamiza kunguru 408,000. Sasa hailingani kabisa ya asilimia 70 ya fedha iliyoingizwa halafu sijui kama inafika asilimia 5 hii kwamba kunguru 11,598 kati ya kunguru 408,000 haya Mhe. Spika, si matumizi mazuri ya fedha za walipa kodi wala haioneshi umakini katika mipango yetu. Nilikuwa naomba Waziri akija nipate maelezo.

Mhe. Spika, eneo la pili ambalo nataka nizungumzie katika Idara hii ukurasa wa 11 pale pamezunguzwa juu ya suala la Idara hii kuhusika kumpatia nyumba Mhe. Makamo wa Kwanza wa Rais. Mhe. Spika, naomba hili pia Waziri akija anipatie maelezo. Kuna maneno mengi yanasemwa kwamba katika kumkodia nyumba Makamo wa Kwanza wa Rais hakukuzingatiwa uwezo wa nchi yetu katika suala zima la fedha. Kuna taarifa hata katika magazeti zimechapishwa kwamba nyumba hii inalipiwa shilingi milioni 10 kwa mwezi. Makazi mapya ya Makamo wa Kwanza wa Rais mimi sina hakika Mhe. Spika, lakini kama hivyo ndivyo basi mimi sitakubali ku-*approve* tena fedha hii kwa mwezi kulipa shilingi milioni kumi, hata kama anakaa kiongozi wetu mmoja katika viongozi wetu wakubwa katika nchi hii. Kwa hivyo nilikuwa naomba Mhe. Waziri akija atupe ufafanuzi kwa nini wamemkodia Makamo wa Kwanza wa Rais nyumba ya thamani ya shilingi milioni kumi ikiwa taarifa hii ni sahihi.

Lakini vile vile Mhe. Spika, naomba pia Waziri akija anisaidie jengine. Hadi hivi sasa Makamo wa Kwanza anaposafiri kwenda hasa Dar es Salaam hana nyumba ya kukaa na hivyo anaishia kukaa hoteli. Na hoteli hiyo anayokaa kwa hadhi yake na wasaidizi wake sina takwimu lakini nina hakika inagharimu fedha nyingi. Sasa watu wengi wa Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais, pamoja na mahusiano mazuri na ndugu zetu wa damu, tumeshindwa kupatiwa nyumba, Serikali yenyewe kutafuta nyumba ya kumuweka Makamo wa Kwanza wa Rais hata ikabidi hadi hii leo anaendelea kutumia hoteli na hatuoni kwamba kwa namna hii tunazitafuna fedha za walipa kodi katika mambo ambayo tungeweza kuyanusuru kama tungelipata nyumba ya kukaa kwa gharama ndogo zaidi kuliko anotumia hivi sasa kwenda kukaa hoteli. Hili naomba pia naomba akija Mhe. Waziri anisaidie.

Mhe. Spika, eneo jengine ambalo pia naomba maelezo linahusu mpango wa Idara hii katika kujenga uwezo wa Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais. Hapa nimeona kwamba kuna mradi umeandikwa kupelekwa UNDP na ukasema tayari umeingizwa katika miaka miwili inayokuja chini ya mpango wa UNDAP. Halafu vile vile akasema kunapelekwa mradi mwengine Benki ya Dunia *World Bank* kwa suala hilo hilo la kujengewa uwezo. Sasa nikawa ninajiuliza kwamba kuna mahitaji makubwa kiasi hicho iwe *focus* Ofisi ya Makamo wa Kwanza katika miradi zaidi ijielekeze katika kujenga uwezo wa Ofisi tu, kuliko mambo mengine mazito ambayo yanasimamiwa na Ofisi hii kama inavyojulikana.

Mhe. Spika, la mwisho katika Idara hii ya Mipango, Sera na Utafiti katika ukurasa wa 13 wa hotuba ya Mhe. Waziri amezungumzia mpango ambao mwaka uliopita tulipiga kelele sana juu ya Serikali kuwa na kituo chake cha kuwahudumia walioathirika na dawa za kulevya. Na tumetajiwa hapa kwamba kuna mradi wa *construction of treatment inhabilitation centre*, hili Mhe. Spika, nilikuwa naomba nipatiwe maelezo kwa sababu umetajwa hapa lakini baadae huku mbele katika hotuba sikuona katika ile Tume ya Kupambana na Madawa ya Kulevya ukiwa umepatiwa maelezo ya kutosha. Sasa nilikuwa najiuliza hizi fedha ambazo zimetajwa katika ukurasa wa 13 hapa zinajumuisha fedha za ujenzi wa kituo hiki? Na je, kinategemewa kuwa cha ukubwa wa kiasi gani? Kuhudumia pengine waathirika wangapi na kinategemewa kugharimu kiasi gani katika ujenzi nilikuwa naomba hilo Mheshimiwa akija atupatie maelezo ya kutosha katika hilo.

Mhe. Spika, eneo jengine ambalo limenikwaza ni katika Idara ya Uendeshaji na Utumishi, ukurasa wa 15 hotuba ya Mhe. Waziri, Mhe. Spika, katika eneo hili pametajwa hapa katika *paragraph* ya 56 kwamba Idara imeweza kuhudumia safari 6 za nje na 17 za ndani kwa viongozi na watendaji katika kuimarisha utekelezaji majukumu ya Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais. Nilikuwa naomba Mhe. Waziri atusaidie *brake down* katika safari hizi alizozitaja hapa zilijumuisha nani na nani katika watendaji na viongozi wa Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais na ziligharimiwa na nani.

Na hilo aliuliza labda niliunganishe kabisa kwa sababu nikiangalia katika buku la *estimate* katika Idara hii hii kwa mwaka huu fedha za safari kama ilivyokuwa mwaka jana zinaendelea kuchukua sehemu kubwa ya bajeti. Mwaka huu kumetengwa katika Idara ya Uendeshaji na Utumishi milioni 71 mwaka jana zilikuwa milioni 95. Kwa hivyo nilikuwa naomba nisaidiwe tunafaidika nini katika suala hili. Na hasa ninaliuliza hili kwa sababu ninategemea ninapokwenda katika mikutano hii tunapata faida kama nchi. Lakini ziko taarifa Mhe. Spika, kwamba katika mkutano mmoja katika mikutano hiyo ambao Mhe. Waziri alishiriki Afrika Kusini mkutano kuhusu Mazingira. Waziri alipata fursa nzuri sana ya kuweza kukutana na Waziri anayehusika na mambo ya mazingira wa Qatar ambapo Zanzibar ingefaidika sana. Lakini bahati mbaya Waziri akauacha mkutano ule na akawahi ndege ya Makamo wa Rais ya Jamhuri ya Muungano iliporudi nyumbani. Sasa ninajiuliza tija ya safari hizi inaisaidia nini nchi yetu Mhe. Spika, ikiwa ile *priority* ambazo zitaisaidia nchi hatuzipati nilikuwa hili naomba Mhe. Waziri akija anipe maelezo.

Lakini vile vile Mhe. Spika, katika bajeti ukurasa wa 15 zimetajwa fedha ambazo zimetumika mwaka jana katika Idara ya Uendeshaji na Utumishi na katika hili kuna fungu ambalo mimi limenitia mashaka linalohusu mishahara. Nimesema kwamba ilitumia shilingi 445, 820,197 sawa na asilimia 141 kwa ajili ya mishahara lakini akatupa maelezo pale kwamba ongezeko hili limetokana na kuongezeka kwa mishahara naikubali. Lakini nimepata mashaka Mhe. Spika, kwa sababu ninapokuja kuangalia sasa ukurasa wa 16 fedha zinazoombwa kwa mwaka huu kwa Idara hiyo hiyo kwenye fungu la mishahara ni shilingi 361,695,000. Sasa unaona fungu hili badala ya kuongezeka kwa mwaka huu au kubakia pale pale limepungua. Sasa kama fungu la mwaka jana liliongezeka kiasi hiki kwa sababu ya kuongezeka kwa mishahara, tena kwa nini kwa Idara hiyo hiyo fungu mwaka huu linapungua kiasi hiki kwa milioni kama thaminini hivi. Nilikuwa hili naomba nipatiwe maelezo ya kutosheleza na ya kuridhisha Mhe. Spika.

Na hapo hapo niunganishe kabisa na suala moja ambalo naomba anipatie maelezo katika bajeti za Idara mbali mbali za ofisi hii kwamba mwaka jana tunajua kwamba mishahara iliongezwa na Serikali. Mwaka huu katika fungu la kila Idara kuna ongezeko kubwa sana katika *brake down* ya mishahara, mbali ya yale marekebisho yaliyokwisha fanywa na unaliona katika kila fungu ile asilimia iliyotajwa inavuka asilimia mia kwa sababu ya ku- *accommodate* zile *adjustment* zilizofanyika. Halafu tena mwaka huu zinaongezeka tena kwa kiasi kikubwa nikajiuliza mwaka Serikali imetangazia kwamba imeongeza mishahara katika bajeti yake, kwanini kunakuwa na ongezeko hili kubwa sana.

Na hapo hapo pia nisaidie kwamba kwa nini ninaendelea kupiga kelele Mhe. Spika, kwa nini fungu la posho maalum katika kila Wizara na Ofisi hii pia imejumuishwa linakuwa na fedha nyingi sana wakati tunaambiwa kuna *consolidation*, marupurupu na stahili nyengine zote zinajumuishwa na mishahara. Kwa nini fungu hili linaendelea kuwa kubwa sana katika kila Idara ya Serikali katika kila Wizara ya Serikali. Nilikuwa naomba maelezo Mhe. Spika, kutoka katika Afisi hii ya Makamo wa Kwanza.

Sasa naomba nije katika Idara ya Mazingira. Kwanza na mimi niungane na wenzangu kuipongeza sana Ofisi ya Makamo wa Kwanza katika Idara hii ya Mazingira katika kuweza kukabiliana vizuri kabisa na suala zima la matumizi ya mifuko ya *plastic*. Mhe. Spika, ni kweli tumeona mafanikio makubwa sana katika hili, na mimi nawapongeza sana kwa sababu ni kweli tulikuwa tuna uwezo wa kudhibiti ilikuwa inatusababishia uchafuzi

mkubwa wa mazingira sasa hivi dawa yake ilikuwa ni kuiondosha. Nashukuru leo Zanzibar inatajwa kama mfano mmoja wapo katika nchi za Afrika katika kuweza kulimudu hili, kwa hivyo tunaipongeza sana.

Lakini nikiacha pongezi hizo Mhe. Spika, najiuliza kwamba ikiwa Ofisi hii imefanikiwa kuzidhibiti mifuko ya *plastic* ya kiasi kile kwa nini katika maeneo mengine uharibifu wa mazingira tunakwama. Sasa hapo ndipo ninapopata wasiwasi je, kwamba huwa tunashindwa au hatuna nia ya kukabiliana na uharibifu wa mazingira. Kwa sababu kama tumeweza katika mifuko ya *plastic* jambo ambalo wananchi wetu walikuwa wagumu kweli kweli. Kwa nini Mhe. Spika, tunakwama katika mambo mengine.

Mhe. Spika, katika hotuba ya Mhe. Waziri ukurasa 17 kifungu namba 2 alikuwa anazungumzia pale kwamba moja katika kazi ya Idara hii ni kupokea maelezo ya miradi na kuona kiasi gani inakwenda sambamba na vigezo vya utunzaji wa mazingira. Lakini Mhe. Spika, tumeona hapa kwamba mpaka Baraza hili kupitia Kamati Teule ilipochukua kazi kwenda kuangalia na kuja mapendekezo na tumeona mambo haya yametajwa. Katika hotuba za Waziri hatuoni kuambiwa kwamba kuna hoteli gani zinakiuka sheria za mazingira. Na kwa nini kwa sababu sheria ya mazingira imewekwa mamlaka Idara na Waziri husika, kwa nini mpaka Baraza hili litoe mapendekezo kwa nini Idara hii haifanyi kazi yake inalalamika lalamika kila siku Mhe. Spika.

Mhe. Spika, na katika hilo nimeangalia pale katika kiambatisho namba 6 wametutajia miradi iliyokaguliwa mingi sana Unguja na Pemba. Lakini kile kiambatisho hakitoshelezi aje atwambie ni hoteli zipi au miradi ipi ambayo imekiuka hayo maagizo kuhusu mazingira na zimechukuliwa hatua gani. Kwa sababu Mhe. Spika, kama unakuwa na sheria halafu ikatoa na adhabu, halafu adhabu ile ikawa haitekelezwi ni sensive kwa mwengine kuifuata sheria. Hasa Mhe. Spika, ninajiuliza mpaka Baraza liingie kati ndio Serikali inaamka kuna tatizo gani hapa. Naomba hili Mhe. Waziri anisaidie.

Lakini vile vile kuna suala zima limetajwa hapa la bidhaa chakavu. Mhe. Spika, bado sijaiona kasi ya kukabiliana na suala hili. Na bahati nzuri siku ya mazingira Waziri alitaja na akatupa takwimu ndani ya hotuba yake ni kiasi gani iwe *electronic waste* zilivyokuwa zinaingia kwa wingi Zanzibar na tunaona katika kila mitaa zilivyozagaa. Zanzibar imegeuzwa kama ndio jaa ya bidhaa hizi. Kumekuwa na vidudu hapa hatujawahi kuviona kuna mende wa ajabu wamezagaa kutokana na bidhaa hizi ambazo zimeingia katika nchi zetu.

Sasa Mhe. Spika, tunasema kwamba tumeamua mara hii sasa Serikali haifikirii tena kupiga marufuku lakini inataka kuweka viwango vya bidhaa gani chakavu vitakuja. Sijui kama tuna utaalam na *main power* ya kulisimamia hilo kiasi kwamba cha kujiridhisha kwamba tunaweka viwango tukaweza kudhibiti kwamba hivi viingie na hivi visiingie. Napata mashaka sana, nilikuwa naomba hili pia atueleze kwa nini tunaendelea kukubali kuleta vifaa hivi chakavu katika nchi na baadae vinajaa tunaviona Mhe. Spika, nchi yetu ndogo hata sehemu za kutupia hatuna. Itakapofika pahala pa kutaka kuviharibu hivi tutakuja kupata hasara kubwa sana kuliko hiyo faida ambayo tunaipata hivi sasa kwa wananchi wetu. Kwa hivyo nilikuwa naomba hilo Mhe. Spika, anisaidie.

Lakini jengine Mhe. Spika, limeguswa na kila mtu hapa suala zima la uchimbaji wa mchanga na bahati nzuri kitabu cha Waziri mwenyewe katuwekea picha hapa inayoonesha ni kiasi gani uharibifu wa mazingira kwa uchimbaji wa vifusi wa mchanga unavyoathiri nchi yetu. Mhe. Spika, na mimi ninajiuliza kwamba kwa nini Waziri na Idara yake hawatumii mamlaka waliopewa na sheria kudhibiti masuala haya, anaogopewa nani katika masuala haya, nani anayehusika katika mambo haya kiasi ambacho kama tunamuogopa hachukuliwi hatua.

Jana Mhe. Spika, nilikuwa ninasoma gazeti la Zanzibar Leo Skuli ambayo ni ya kihistoria katika nchi hii, Skuli ya Lumumba imetajwa pale kwamba inaanza kuathirika na huenda ikaanguka wakati wowote kutokana na uchimbaji wa mchanga unaofanywa kwa kutumia magari ya punda. Mpaka imetajwa mule kwamba wanafunzi wanapigwa mawe na wachimbaji wale kwa sababu wanafunzi wameamua kuchukua hatua ya kuihami Skuli yao. Sasa Idara iko wapi Mhe. Spika. Serikali iko wapi katika hili mpaka tunafika hatua kama hii. Lakini karibuni Makamo wa Kwanza wa Rais alikwenda kukagua pale Uwanja wa Amani. Nacho kiwanja huku kwenye mipaka yake kimeathirika sana sana. Kwa hivyo ninajiuliza kwa nini tunashindwa kuchukua hatua zaidi.

Na hapo hapo Mhe. Spika, niunganishe na suala lile ambalo la mazingira liko katika ukurasa 18 suala zima la kushulikia taka. Kwa sababu mazingira ni pamoja na usafi katika maeneo yetu Mhe. Spika. Katika kitabu hiki Waziri katwambia kwamba kuna ujumbe ulipelekwa Moshi na Arusha ili kwenda kujifunza namna ya kutunza usafi. Niliona orodha mrefu pale Baraza la Manispaa, Halmashauri za Wilaya wamepelekwa, Idara ya Mazingira yenyewe

ilikuwemo. Lakini *impact* yake Wizara hii bado sijaiona katika Zanzibar. Naona kila siku uchafu unazidi badala ya kupungua katika Zanzibar taka zinazidi badala ya kupungua. Sasa nasema ikiwa ziara kama hizi hazileti tija kwa nini tuendelee kutoa fedha kwa ziara kama hizi ambazo zinaishia kwenye posho mifukoni lakini tija ya Wizara zile na mafunzo yanayopatikana katika hali halisi.

Mhe. Spika, pamoja na upungufu mwingi kuna eneo moja linafurahisha namba nilipongeze ndio kawaida yangu nikiona na la kupongeza huwa napongeza. Nimeona hapa kuna suala la mradi wa maji Nungwi. Nungwi Mhe. Spika, ni kijiji ambacho nimeshakitembelea sana katika makumu tofauti, kinaathirika sana na masuala ya maji ya chumvi. Kwa hivyo kama imefikiriwa kupitia mradi huu ambao umetokana na fedha za Ofisi ya Rais ya Jamhuri ya Muungano naipongeza Idara ya Mazingira kwa kuliona hili, wamesema mradi huu unategemea kukamilika karibuni naomba hili walisimamie kwa ukamilifu ili wananchi wa Nungwi waondokane na adha hii kubwa ambao wanaipata. Najua tunaathirika wengi na maji lakini Nungwi kumeathirika vibaya vibaya.

Mhe. Spika, nije kwa ufupi katika suala la Tume ya Dawa za Kulevya. Kwanza hapa vile vile namba niipongeze Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais. Nikilinganisha hali ilivyokuwa pengine kabla ya kuundwa Ofisi ya Makamo wa Rais katika suala zima watumiaji tulikuwa tukiwaona mitaani na hali ilivyo sasa naweza kusema kuna improvement kubwa sana.

Kuna kipindi hapa kati kati niliona kama waliregeza kamba wakarejea tena mitaani, lakini sasa hivi naona hii hali imerudi kuwa afadhali kidogo lakini kama alivyosema ninafikiri Mhe. Farida kwamba tunaonekana tunaongeza kasi katika kukabiliana na hawa watumiaji lakini kiasi gani tumeongeza kasi katika kuzuia uingizaji wa dawa za kulevya. Kwa sababu suala la dawa za kulevya lina ncha mbili kuna demand na *supply*. Sasa demand tunajitahidi kuipunguza, lakini huku kwenye *supply* je maana hivi ni vitu vina ushawishi wake, ikiwa madawa ya kulevya yatakuwa naingizwa bado tutapata tabu kubwa sana ya kupata watu watashawishika kuingia katika utumiaji wa dawa za kulevya.

Katika hili nilitaka kuongeza nguvu yangu katika suala zima la choo kilipata kifungu maalum pale airport cha ku-*flash* madawa haya. Mhe. Spika, inatupa mtihani kidogo na mimi sielewi ninapokuja kukuta Waziri mmoja wa Serikali hii hii analaumu sehemu nyengine analaumu sehemu nyengine ya Wizara ya Serikali hii hii kwamba haimpi mashirikiano katika kukamilisha suala hili. Mhe. Spika, aibu, aibu kwamba Jumuiya ya Kimataifa choo hiki kimekaa kwa miaka mitano, sita hakijafungwa. Sasa mimi napata mashaka Mhe. Spika, sasa hili tatizo ni kufungwa au hii ni *deal* kuna watu wanafuika pale hawataki choo kile kifungwe. Tuambiwe Mhe. Spika, hivi kweli miaka 6 Serikali inashindwa kufunga choo, kwa sababu ya mvutano au hawataki kutoa ushirikiano baina ya Polisi na ambao Mratibu wake kwa Zanzibar ni Ofisi ya Makamu wa Pili ya Rais ni Ofisi kubwa na huku Ofisi inayoshughulikia madawa ya kulevya Ofisi ya Makamu wa Rais Ofisi kubwa. Afisi hizi mbili moja iko Migombani moja iko Vuga inashindwa kushirikiana katika suala hili, kuna nini hapa Mhe. Spika, kwa hivyo katika hili naomba tusaidiwe.

Hapo hapo Mhe. Spika, naipongeza Serikali kama imeziona nyumba za *Sober House* na inatusaidia. Lakini bado mimi siridhiki na kiwango ambacho kinachowekwa. Unapoitazama bajeti ya Ofisi hii na bajeti ya Tume hii ya dawa za kulevya iliyowekwa na ile *amount* inayopelekwa katika *Sober house*, kwa sababu Mhe. Spika, isiwe tunatumia fedha nyingi katika masuala ya utawala tu kule chini kwenye *field*, kwenye *ground* zikawa hazifiki na hilo ndio tatizo letu kubwa sana Mhe. Spika. Kwa hivyo nasema Serikali haijajenga *...centre* ndio kwanza inazungumzwa sasa hivi. Kuna watu wanajitolea wanazijenga juzi namuona mama yangu Bi Fatma Sukwa katika televisheni analalamika. Kapokea ujumbe anaeleza lakini mwisho analalamika kwamba Serikali haimpi *support* ya kutosha. Nikizungumza Serikali hapa ninaizungumzia Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais. Kwa hivyo ninasema Mhe. Spika, anambie Waziri akija hapa mwaka huu katenga kiasi gani kuisaidia *sober house* ili kuweza kujikimu mahitaji yake.

Lakini hapo hapo Mhe. Spika, wanasema wanaosimamia nyumba hizi wengine tuko karibu nao, hata unapompeleka pale miezi mine akakaa ukamsaidia kuachana na tabia ile, akitoka kama hana shughuli ya kufanya basi ni rahisi zaidi kurudi akenda akanya tena suala lile la utumiaji wa dawa ya kulevya. Sasa wenyewe wameomba Serikali hawakufika mbali lakini wamefika pale wameanzisha mule mule ndani ya *Sober house* njia gani za kuwatunza watu wao ili kuwea kujifunza kazi za amali wakitoka wapate shughuli za kufanya waweze kupata riziki zao. Sasa Serikali katika mradi huu mpya umesaidia kitu gani.

La mwisho Mhe. Spika, nataka kwenda katika Tume ya Ukimwi. Katika Tume ya Ukimwi mimi natangaza kabisa hapa nitaondoa shilingi ya Tume ya Ukimwi mpaka nipate maelezo ya kutosha kuhusu matumizi ya fedha nyingi sana ambazo tukiidhinisha katika Tume hii. Mhe. Spika, kwa sababu ya kuokoa muda wako naomba tuangalie ukurasa 38 mpaka 39 ukiziangalia fedha ambazo zinapelekwa katika Tume ya Ukimwi ni fedha nyingi sana. Mwaka jana kwa mfano Tume imeidhinishiwa shilingi 472 milioni kwa kazi za kawaida lakini halafu shilingi 90 milioni kwa kazi za maendeleo kutoka Serikalini Zanzibar wametoa zote asilimia mia moja. Lakini kutoka kwa wahisani walitarajiwa kuchangiwa shilingi bilioni moja na mia tatu milioni na hadi kufikia Mei, 2012 wamepata mia saba na tano milioni laki tano na hamsini elfu. Kwa mwaka huu anatarajia kutumia jumla ya shilingi mia saba thalathini na tisa milioni kwa kazi kawaida. Lakini halafu Serikali kwa kazi za maendeleo itawachangia shilingi hamsini milioni na kutoka kwa wahisani wanategemewa wapewe mia nane tisiini na tatu milioni laki saba na tisiini elfu.

Hizi fedha ni nyingi sana lakini tuiitizame hiyo *impact* ya kazi ya Tume ya Ukimwi katika Zanzibar iko wapi? Ni semina, warsha, kujengeana uwezo ni njia ambazo Mhe. Spika, ambazo matumizi yake inawafikia wahusika? Tunawajua humu waafrika wanaishi katika hali ngumu sana hawasaidiwi. Katika hotuba hii imetajwa kwamba moja katika kazi ya Tume hii ni kusaidia kuwapa watu vyanzo mbali mbali vya mapato ili watu wasishawishike kufanya vitendo vinavyopelekea kuambukizwa ukimwi. Lakini tujiulize tukitaka mchanganuo ngapi zimekwenda huko. Leo katika bajeti ya mamilioni haya yanayokaribia bilioni Zalpha plus ni Jumuiya iliyowekwa kuwasaidia waathirika inapewa milioni 15 kwa mwaka mzima.

Mhe. Spika, kuna kituo tumewahi kukitembelea kupitia katika kamati zako tunakushukuru sana katika Baraza hili tunaona mengi. Kiko pale Chake Chake hiki kituo kinafanya kazi mbili, kimeandikishwa kwa jina la Ukimwi NGO lakini kinasaidia hata masuala haya ya *Sober house* wanapokwama mahitaji yao walikuwa wakiwapa. Lakini inafungwa kwa sababu hakina pesa, wakati tumetegemea pesa kama hizi ndio zingepelekwa pale kwenda kufikia walengwa wananchi. Kwa sababu tunadhani ni fedha za wahisani kwamba fedha za wahisani ikija hapa ni pesa ya walipa kodi wanapewa walipa kodi wa Zanzibar.

Sasa kwa sababu hiyo fedha zetu zinaishia maofisini kwa masemina lakini lengo hasa lililokusudiwa halifikiwi. Kwa hivyo Mhe. Spika, mimi katika hili nasema kabisa nimeona *brake down* kubwa sana katika kitabu hiki, lakini yote yameingizwa ndani ya utawala zaidi mambo ya semina kuliko kwenda katika shughuli ambazo pengine zitawasaidia zaidi waathirika au kuzuia watu wasiingie katika vitendo hivi vinavyosababisha ukimwi. Kwa kifupi hazendi kwa raia Mhe. Spika. Kwa hivyo nasema fungu hili mimi nitalizuia mpaka nipate maelezo ya kutosha kutoka kwa Mhe. Waziri.

Nakushukuru sana Mhe. Spika, nitaunga mkono hoja baada ya kujibiwa hoja zangu.

**Mhe. Ashura Sharif Ali:** Ahsante sana Mhe. Spika, awali ya yote nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu Mtukufu *subhanallahu wataala* aliyetujaalia uhai, uzima tukakutana hapa kutekeleza majukumu yetu kwa maslahi ya taifa letu. Lakini pia nikushukuru na wewe Mhe. Spika, kwa kunipatia nami nafasi hii ya kutoa mchango wangu mdogo katika hotuba iliyoko mezani wakati huu. Mhe. Spika, nianze pia na kumpongeza Mhe. Waziri kwa uwasilishaji wake mzuri wa hotuba hii. Lakini niwapongeze pia ma watendaji wake.

Kwanza nianze na mchango wangu mdogo kwani laiti kama sikuleta maombi kwako nisingelichangia kwani mengi tayari wenzangu wameshayachangia. Mhe. Spika, sasa niende katika ukurasa 13 kifungu cha 48 Idara ya Uendeshaji na Utumishi. Ninaiomba sana Idara hii au Ofisi hii imtafutie Makamu wa Kwanza wa Rais nyumba huko Pemba. Kwani hili ni tatizo, hana sehemu ya kufikia. Nadhani hata wewe Mhe. Spika, unalifahamu vyema suali hili wakati wa kukosa wewe kuhudhuria katika Baraza la Iddi kwa sababu Mhe. Makamu wa Kwanza wa Rais alifikia katika nyumba ambayo na wewe ndio nyumba unayofikia. Hivyo basi ninaiomba sana sana kabisa ofisi hii ilifanye hilo kumtafuta Makamu wa Rais nyumba ya kufikia huko Pemba ili na viongozi wengine wasikose fursa adhimu kama hiyo ambayo aliikosa Mhe. Spika, wa Baraza letu la Wawakilishi.

Baada ya kusema hilo sasa niende katika ukurasa wa 16 kifungu cha 60, hapa panazungumzia kuhusu mazingira. Mhe. Spika, ni ukweli usiofichika ya kwamba Zanzibar ni visiwa na kawaida ya visiwa vinakuwa na utaratibu wake maalum kwani eneo lake mara nyingi huwa haliwi kubwa na huzungukwa na bahari. Ni muhimu sana kwa wizara hii husika kuliangalia hilo na kuliona vyema.

Mhe. Spika, juzi tarehe 13 wakati tukisikiliza Bajeti ya Serikali ya Waziri wa Nchi (OR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo katika kipengele kimoja niliona anasema kuwa pato la taifa ni uchimbaji wa mawe na mchanga kijisehemu hicho kimo. Nilishitushwa mno na katika mchango wangu nilizungumza hilo, kusema kutokana na hali halisi ilivyo tumeweka wizara maalum kwa ajili ya uhifadhi wa mazingira yetu lakini pia tunasema ya kwamba uchimbaji wa mchanga na mawe ni sehemu ambayo nchi yetu inajipatia mapato. Najiuliza, hiki ni kitendawili.

Mhe. Spika, kwa kuliona hili niseme wazi kwamba Zanzibar sasa imeathirika katika sehemu tofauti za mjini na vijijini hali sio shuwari. Wananchi walio vijijini wanapiga kelele sasa hawana sehemu za kilimo ukizingatia Zanzibar kilimo ni uti wa mgongo wa wananchi wetu wengi walio wanyonge.

Mhe. Spika, imefika hadi sasa yanachimbwa mawe na vifusi bila ya kuangalia athari za mazingira na hatima ya baadae ya taifa letu, tunaingia katika miradi mbali mbali ni maendeleo lakini tutafakari na kujua kwamba Zanzibar ni visiwa. Iko haja wakati tunapotaka kutekeleza miradi yetu mizuri ya maendeleo basi tukae na kufikiria ni wapi tutachimba na tutachimba kwa hatua gani na kimo gani na wizara hizo zote husika kukaa pamoja na kuona kwamba wanafanya mambo ambayo yatakuwa na maslahi endelevu kwa wananchi wa Zanzibar na sio kufanya maendeleo ya upande mmoja na wa pili ukawa ni athari kwa Wazanzibari hao au wananchi hao ambao wanawatendea hayo.

Mhe. Spika, niendelee tena kwamba sasa Zanzibar pia imekuwa na uzoefu wa kuingiza bidhaa chakavu kutoka nchi za nje. Hili ni tatizo, ipo haja wizara husika kushirikiana na wizara zinazohusika pia kuona tunaingiza bidhaa gani ambazo zitakuwa endelevu na zitaweza kudumu kwa muda mrefu bila ya kuathiri hali halisi ilivyo. Isigeuzwe nchi yetu kuwa jalala ya mambo mabovu ambapo dunia wanashindwa pa kuyapeleka na kwauzia wafanyabiashara wetu na kuona sisi ni biashara. Wizara ilione hilo ishirikiane na wizara husika kuona bidhaa zote zinazoingizwa basi ziwe na kiwango na zinastahiki kuishi kwa muda mrefu bila ya kuhitaji kutupwa.

Mhe. Spika, pia niipongeze wizara hii kwa upigaji marufuku wa mifuko ya plastiki. Kwa hakika tatizo hili lilikuwa gumu, zito na tuliona ya kwamba ni vigumu kufanikiwa, lakini nasema naipongeza imefanikiwa kwa asilimia kubwa. Pamoja na hayo, lakini pia ningependa niwaambie wizara hii ishirikiane na Wizara ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika kuwafundisha wananchi wetu mila na desturi na utaratibu wa Wazanzibari.

Zanzibar ina mila na silka zake, Zanzibar ilitumia sana mikoba na vikapu mara nyingi kabla ya mifuko hiyo, utamaduni huo umepotea ambapo utamaduni huo ulikuwa na uwezo mkubwa wa kuhifadhi mazingira yetu. Naiomba wizara itoe taaluma tosha kwa wananchi ili nao waelewe kwamba uzalishaji huu wa ususi wa mikoba na vikapu basi pia pamoja na kwamba tunaweka vizuri mazingira yetu lakini pia ni kipato kwa wale ambao watafanya biashara hii. Kwa hivyo, ni kuwaondoshea au kuwapatia soko wale wanawake ambao mara nyingi hutumia fursa hii ya kufanya bidhaa hizo wakati mwengine kushindwa pa kuuza. Lakini kama wizara itaipa kipaumbele na kuwapa taaluma watu hawa basi naamini kwamba wataitengeneza na Wazanzibari watakumbuka mila na utamaduni wao wa kutumia vikapu na mikoba kwa ajili ya kwenda madukani kujitafutia bidhaa mbalimbali. Mhe. Spika, hiyo ni njia mbadala.

Nikiendelea na mchango wangu katika ukurasa wa 24 kifungu nambari 80, hii ni Idara ya Watu wenye Ulemavu. Mhe. Spika, watu wenye ulemavu wana haki sawa na watu wengine, hii mimi naizungumzia kwamba watoto wengi ambao wana ulemavu basi mara nyingi hukosa huduma za msingi ikawa ni tofauti na wale watoto wengine. Nalizungumzia hili kwamba mara nyingi inaonekana watoto wenye ulemavu huwa wanakosa kuendelea na elimu ya juu. Wizara yako naiomba ichukue nafasi ya makusudi ya kuona kuwa watoto hawa ambao tayari wameshakuwa na mwelekeo wa kusoma na wana uwezo wa kufaulu kwenda elimu ya juu basi wanapata tabu sana ya kufuatilia ama mikopo ama ujazaji fomu kwa ajili ya kushiriki katika zoezi la kufanya usaili.

Nakuomba Mhe. Waziri husika wa wizara hii uwatafute, uwajue hao ili pale inapotokea na wao kutaka kushiriki au kuweza uwezo wao unawaruhusu kwa vipaji vyao basi wasipate usumbufu. Ni dhahiri kwamba sote ni mashahidi kuwa maofisi yetu mengi yao ni ya ghorofa wanashindwa kabisa kuweza kushiriki au kuonekana kwa urahisi, hivyo huduma hizi huwafanya wao kujiona wanyonge na kushindwa kufikia kupata elimu wanayostahiki kupata kwa kila mwenye uwezo wa kufikia hatua hiyo.

Mhe. Spika, sasa niendelee katika ukurasa wa 27 katika kifungu cha 93 kinachohusiana na dawa za kulevya. Zanzibar ni visiwa hivi tujiulize sote baada ya kutumia Uwanja wa Ndege na Bandari kwa kuingia au kusafiri kwenda na kurudi tumeweza kuzidhibiti sehemu zote hizo? Uwanja wa ndege ni mmoja tunautumia tunaujua, lakini hebu tujiulize pembezoni mwetu mote tumezungukwa na bahari kuna utaratibu gani wizara yako Mhe. Waziri unaochukua ili kuona kwamba usalama huo unapatikana katika bandari nyengine zote ambazo vyombo hutoka nje ya Zanzibar na kurudi.

Mhe. Spika, vijana wetu wengi wameathirika mno na dawa za kulevya na sasa imekuwa ni gumzo dawa za kulevya, dawa za kulevya, taifa linaangamia nguvu kazi ya taifa inaondoka, huo ndio uhalisia ulivyo. Lakini tujiulize tumejipanga kweli kwa ajili ya kusaidia hilo? Wenzangu walitangulia kusema hivi hawa ambao walikamatwa na hizi dawa za kulevya na kuhusika kabisa kuna mtu aliyeshtakiwa na kufungwa. Hebu Mhe. Waziri utakapokuja hapa naomba unieleze kuna kesi ngapi za dawa za kulevya ambazo zimeripotiwa kwako na ngapi zimepata ufumbuzi.

Mhe. Spika, kama hatukujikaza tukafunga mikanda taifa hili litakosa warithi kwa dawa za kulevya. Wengi walidhani kwamba dawa hizi kwa mila na utamaduni wetu labda watatumia wanaume tu, lakini si sahihi hata watoto wa kike tumeshuhudia wanatumia, wanaathirika na athari yake ni nzito sana.

Mhe. Waziri katika hali hii kumejitokeza wenzetu kuandaa *Sober House* kwa ajili ya kuwasaidia vijana wetu, lakini wewe kama serikali wizara ina mpango gani kuona kwamba inaunga mkono nguvu za hawa wahisani wetu vijana mlioamua kuwasaidia vijana hawa. Kwani vijana hawa wanapokaa katika nyumba hizi na kupewa mafunzo ili kuachana na dawa za kulevya wanaporidhia na hatimaye wakaacha wanapotoka nje wanakuwa hawana ajira na hatimaye hurejea katika makundi yao na kurudi tena kule walikotoka.

Mhe. Waziri nakuomba sana, katika *Sober House* zote zilizoanzishwa lazima uwawezeshe vijana hao watokapo basi wawe na uwezo wa kujiajiri, watapokaa huko moja ya mafunzo yao ni kuona kwamba wanafundishwa mbinu za kiuchumi kwa ajili ya uzalishaji ili watokapo wamudu maisha yao na kuachana kabisa na mambo haya. Kwani mambo hayo mara nyingi huja kwa vijana ambao wamekosa kazi kukaa katika magenge ambayo hayana maana na mwelekeo mzuri.

Mhe. Spika, nikiendelea na mchango wangu sasa niingie katika ukurasa wa 34 katika kifungu cha 116, kifungu hiki kinazungumzia UKIMWI. UKIMWI na dawa za kulevya ni vitu vinavyofanana mno, kwa sababu ukiwa ni mlevi wa dawa za kulevya basi na UKIMWI uko karibu mno kuupata.

Mhe. Spika, hapa niseme kwamba inaaminika kabisa kwamba katika dunia wataalamu wameumiza vichwa vyao mno na wamehangaika kiasi cha kuhangaika lakini tiba kwa ajili ya gonjwa hili imekosekana. Zimepatikana dawa za kujipa matumaini ya kuendelea kuishi zaidi au kutokukondeana au kuathirika zaidi lakini dawa hasa ya tiba haikupatikana. Suala lililo mbele yetu la UKIMWI ni athari ambayo imekuwa mzigo kwa taifa, tunalazimika kutumia fedha nyingi ambazo tungezitumia katika shughuli zetu nyingi za maendeleo lakini tumelazimika tuzitumie katika sekta ya UKIMWI kwa kuona ndugu zetu wapo katika hali ngumu. Kwa misingi ya haki za binadamu tunatakiwa wenzetu hao tuwe nao kwa ukaribu, dawa ya tatizo hili inaonesha dhahiri kwamba kinga yake ni bora kuliko tiba maana haipo.

Hivi niulize hapa kwetu Zanzibar tumejipanga vipi kutumia mila na desturi na utamaduni wetu kwa ajili ya kuondosha yale ambayo yanakaribisha zaidi, mambo ya uchomaji wa sindano haya madaktari wameyamudu mno. UKIMWI unapatikana zaidi kabisa katika njia ya kujamiiana, hebu tujiulize tuna mpango gani kutumia mila na utaratibu wetu kuona kwamba tunajilinda na kuweza kuhifadhika kutokufika katika hali hii ambayo inasababisha kuondoa kabisa fedha hizi badala ya shughuli za maendeleo tukalazimika kuzitumia kwa ajili ya shughuli hizi za kuwasaidia wenzetu waliofikwa na mtihani huu mzito.

Mhe. Spika, ni ukweli usiofichika asilimia kubwa ya Wazanzibari ni Waisilamu na naamini na wengine wote ambao wana dini nyengine zinakataza haya mambo. Ni dhahiri kwamba kwenye Dini ya Uislamu inasema kwamba, *'laa takrabu zinaa'*, usiikaribie mbali ya kufanya bali usiikaribie hasa ni kosa, tunajiepushaje? Nadhani kitandawili hiki kama tutajiweka vizuri na kuona kwamba wageni ambao wanaingia Zanzibar katika sekta yetu ya uwekezaji utalii nao wanaiga mila na silka za Wazanzibari basi nadhani kwamba hiyo ni dawa tosha.

Mhe. Spika, sote ni mashahidi tunapoingia katika mahoteli ya kitalii tunakuta mavazi ya ajabu ajabu, mila na silka za Wazanzibari haziruhusu huo ndio ukweli, pamoja na uhuru wake mtu lakini mila na utamaduni wa nchi ni lazima uheshimiwe, laiti haya tungelikuwa tumeyapa kipaumbele na misongamano isiyo ya lazima, ngoma ambazo hazina faida, vituo vya mabaa na sehemu kubwa za starehe kwa sababu sehemu ya starehe ukinywa pombe umeibadilisha akili itakuruhusu kufanya kitu chengine chochote bila ya kujali na hatimaye unakuja kushitukia hali hii. Naamini kwamba kama serikali itatilia mkazo wa kuzungumza, kunasihiana na kutumia viongozi mbali mbali wa kidini hasa rasmi na kuwaelekeza na kutumia utalii ambao unaingiza pato la taifa lakini na wao kuwaona kwamba wanafuata mila na silka za Zanzibar hususan katika wakati wa uajiri wa vijana wetu.

Kwa sababu hata vijana wetu ukivaa shungi na nikabu *Wallahi* hutakiwi kuajiriwa katika hoteli, huo ndio utaratibu. Tumewashuhudia vijana wetu wengi Wakizanzibari wakitoka nyumbani wamevaa baibui na mtandio mzuri vazi la Kizanzibari lakini ingia hotelini ukapate huduma uone mambo, nenda *beach* pwani huko wanakokoga Wazungu na watoto wa Kizanzibari wadogo wapo, mtoto akibebwa hutizama kichogo cha mzazi wake, mambo yalioko pwani na vijana wadogo wanajaribu mapema na hali ya uchangiaji wa ubakaji nayo huongezeka pia, hili nalo linachangiwa na hayo. Hili namuomba Mhe. Waziri lazima akae na sekta zinazohusika mashekhe, watu wa dini ili tuone, hatuna njia ya kujinasua kwani wataalamu wameumiza vichwa tiba yake haikuonekana.

Mwisho kabisa niseme kwamba tusisahau kuwa sisi tumeumbwa na tutaondoka katika ulimwengu. Njia pekee ni ile aliyoiona Mwenyezi Mungu (*S.W*) ya kutukataza *laa takrabu zinaa*, tuachane na hilo. Jengine litakalokuja kwa bahati mbaya tutakuwa tunajua ni bahati mbaya na sisi sote tutakuwa na imani ya kulichangia hilo, lakini lile ambalo limekuja kwa misingi ya starehe na kuona kwamba utabakia milele naamini kwamba hili ni mzigo kwa taifa hili.

Mhe. Spika, kuna wengi ambao wanataka kufanyiwa mengi hususan mambo ya afya na elimu, lakini yanashindikana na pesa nyingi za wafadhili zinatumika kwa ajili ya hao na sijui na mimi niseme hivi, zile fedha zote nyingi Mhe. Waziri zinatumika kwa ajili ya UKIMWI au ndio semina za kulipana tu wizara kwa wizara na hatimaye tukaambiwa kuwa zimetumika kwenye UKIMWI. Hebu twambie Mhe. Waziri ni kiasi gani ambacho kilitengwa kipindi cha mwaka 2011/12 na huu 2012/13 kuna kiasi gani ambacho unakihitaji kwa ajili ya tatizo hili la UKIMWI kwani huu umekuwa ni mtihani.

Mhe. Spika, baada ya kusema hayo, mimi pamoja na wanawake wenzangu wa Mkoa wa Kaskazini tunaunga mkono hotuba hii kwa asilimia mia moja.

**Mhe. Jaku Hashim Ayoub:** Ahsante sana Mhe. Spika, nami niungane na wenzangu waliopita kina Mhe. Saleh Nassor kwa kushukuru jinsi unavyoendesha vikao vyako hivi kwa hekima na busara zako Mhe. Spika.

Vile vile nimshukuru Mhe. Waziri pamoja na watendaji wake wote kwa bajeti hii waliyotuletea. Mimi kama nilivyozungumza Mhe. Spika, hazitozidi dakika tano nina mambo matatu tu, mawili nitahitaji maelezo na moja litakuwa la kawaida.

Nije katika ukurasa wa sita Ziara za Makamu wa Kwanza wa Rais. Mhe. Makamu wa Kwanza wa Rais aliposafiri kwenda katika ziara zake ili kuwaletea maendeleo wananchi sijui ofisi yake inafuatilia vipi baada ya ziara hizo, ikiwa msafara huo umetumia pesa za walipa kodi wengi na utendaji wake unakuwa hauonekani. Hii tumekuwa tumezowea kwa viongozi wetu wengi kwenda safari kubwa kwa kutegemea mategemeo baadae hayaonekani. Hapo Mhe. Waziri nitahitaji maelezo.

Nikitoka hapo nije ukurasa wa 11. Waziri ameeleza kuhusu uamuzi wa vifaa vya marekebisho ya makazi, mimi nilikuwa nataka kujua tu, nyumba aliyokuwa anakaa Mhe. Makamu wa Kwanza wa Rais kama ni ya kukodi au vipi, na kwa gharama gani. Hili suala umelipigia kelele mara nyingi kuwa viongozi wetu wanakuwa na matatizo ya nyumba za kuishi na nyumba huwa zinaanguka ikisha hazifanyiwi marekebisho yoyote. Kwa hivyo hili nitahitaji maelezo Mhe. Waziri iko pahali gani na sehemu gani.

La tatu ni kuhusu dawa za kulevya. Suala hili tunakuwa tunafanyiwa semina mara nyingi lakini utekelezaji wake bado umekuwa kizungumkuti, kwa kweli waletaji ndio wenye jukumu kubwa la kushughulikiwa kuliko hawa watoto wa mitaani. Imefika pahali utakuta watu wanasinzia ovyo tu uwajibikaji unakuwa haupo. Semina zimekuwa nyingi, sheria nyingi, mikakati mingi lakini utekelezaji wake ni mfupi.

Kwa hayo machache Mhe. Spika, nakushukuru sana.

**Mhe. Fatma Mbarouk Said:** Ahsante Mhe. Spika, kwa kunipa na mimi fursa hii nichangie hotuba hii ya Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais. Kwanza nimshukuru sana waziri mwanamama ambaye kama walivyosema wenzangu nimpongeze sana na hasa ilivyokuwa jina letu ni moja na maana yake jina hili ni mtu ambaye anapenda maendeleo kwa wenzake basi nimshukuru sana.

Mhe. Spika, niwashukuru pia watendaji wake, kwa kweli hotuba hii imejaza kila kitu kwa upeo na niseme kwamba serikali na hasa Wizara ya Fedha bajeti hii kila kifungu alichokiomba basi wapewe kwa ukamilifu.

Vile vile Mhe. Spika, ni kwamba kwenye matumizi kuna mambo mbali mbali, ni lazima na wao wakishakupitishiwa pesa hizi basi watumie zile kanuni na sheria za fedha na manunuzi ya pesa za umma, sheria ile ya manunuzi basi ifuatwe.

Mhe. Spika, pia niipongeze Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa kwa yale yote ambayo waliona ni kikwazo na kuyaeleza hapa mbele ya Baraza lako hili tukufu.

Sasa niende kwenye suala la mazingira, kama ilivyo ofisi hii inasimamia mazingira basi na mimi niseme kwamba kwa yale waliyoyasema kamati ile ilipotoa ripoti yake kuhusu mitaro. Kwa kweli mitaro inayomwaga maji moja kwa moja na hasa kule Chake Chake kwamba mitaro ile maji yanatuama na inaweza kusababisha maradhi ya miripuko. Kwa hivyo, mitaro ile ishughulikiwe ili isije ikasababisha maafa makubwa.

Vile vile niseme kwamba wizara hii ina majukumu ya kusimamia mazingira basi ni lazima elimu ya kutosha itolewe kwa wananchi. Kwa vile tunajua kwamba ulimwenguni sasa hivi kuna hali ya kuongezeka hewa ukaa ambayo inasababisha joto jingi ulimwenguni na kusababisha kwamba sasa hata zile barafu kwenye milima zinayeyuka na kufanya kujaa kwa maji ya bahari. Kwa hivyo, wananchi wetu lazima wapewe elimu ya kutosha ili wasikate miti ovyo na tuweze kuikabili hali hiyo.

Pia nimpongeze waziri kwa kuandaa mkakati huu wa kutokuingizwa mifuko ya plastiki nchini na kwa hili limefanikiwa kwa kiasi kikubwa.

Mhe. Spika, vile vile nije kwenye suala la UKIMWI. Kwa kuwa wizara hii inashughulika na mambo ya vijana waathirika wa UKIMWI kufanya mikakati, basi pia niwashukuru sana, isipokuwa niseme kwamba serikali izidishe juhudi zaidi. Kwa sababu dawa za kulevya tusiwaone wale wanaoshughulika na dawa zenyewe, lakini wale waingizaji wa dawa hizo ndio wa kuwafuatilia zaidi.

Kama walivyosema wenzangu kwamba dawa za kulevya zinapita kwenye njia mbili, baharini na uwanja wa ndege. Kwa hivyo ni lazima kuandaliwe mikakati ili dawa hizi zisiweze kupita, kwa sababu hawa wanaopitisha wanaonekana wana *technique* kubwa na niseme kwamba serikali ni lazima ilishughulikie suala hili ili dawa hizo zisiweze kupita. Kwa sababu kila zikipita basi zinaathiri nguvukazi ya taifa ambao ni hawa vijana wetu wadogo unaowakuta njiani wanasinzia sinzia ovyo.

Mimi niseme kwamba serikali ikilitilia nguvu hasa na kulisimamia jambo hili basi tunaweza tukafikia pahala na tukafanikiwa na kuondoka dawa hizi tukapata afuweni.
Mhe. Spika, nikija kwenye hizi *Sober House* ni muhimu sana na naiomba serikali kupitia wizara hii isaidie sana *Sober House* ili vijana wetu waachane na hizi dawa kabisa kabisa.

Vile vile wenzangu walizungumzia kwenye dawa za kulevya kuhusu kudhibitiwa kwa sababu tulikuwa na mbwa lakini amefariki. Sasa mtu akifariki basi hurithiwa, lakini mpaka leo mbwa huyu hatujaona kwamba kuna mbwa mwengine ambaye amepatikana. Kwa hivyo, wizara ichukue juhudi na hapo atakapopatikana mbwa huyo basi asiwe mmoja wapatikane mbwa mke na dume ili wapate kuzaliana Mhe. Spika. Sasa ningeomba kuwa hili suala la mbwa litiliwe maanani sana. *(Kicheko)*

Mhe. Spika, niseme suala jengine la watoto walemavu ni watu ambao serikali itie mkazo zaidi ya kuwasaidia, na hasa pale inapotokea suala la kubakwa. Kwa kweli ni tatizo kubwa mpaka hivi sasa hatujafikia kitu gani kinachojitokeza hata kwamba mwisho wa kesi zile za watoto hawa kubakwa, basi haipatikani *solution*. Kwa hivyo

Mhe. Spika, ningemuomba sana Mhe. Waziri kwa kushirikiana na Wizara ya Wanawake na Watoto suala hili walishughulikie, hiki kifaa cha *DNA* ni lazima kupatikana hapa kwetu, kama ilivyokuwa mambo mengine ni muhimu na kifaa kipatikane.

Ni lazima wale wote wanaodhalilisha watoto hawa wenye ulemavu basi wachukuliwe hatua za kinidhamu na sheria. Kulikuwa na sheria nzuri hapa iwapo umempa mtoto ujauzito ambaye hajawahi kuolewa basi kulikuwa na sheria ya miaka mitano. Kwa hivyo ninafikiria hizi sheria zinakwenda zinajirejea. Ninasikia kuna sheria nyengine ambayo ilikuwepo mwanamme na mwanamke wote adabu, lakini bado vitendo hivi vinaendelea. Kwa hivyo niseme kwamba hii sheria itakayopitishwa iwe-*strict* kweli kweli, na kila mtu ajue kwamba akifanya suala hili, basi anachukuliwa hatua zile za kufaa.

Kwa hayo machache na kwa sababu kwanza nimeiamini ile Ripoti iliyotolewa Kamati ya Kusimamia Viongozi Wakuu wa Kitaifa, hivyo mimi naona imenimaliza ile ripoti na ninaunga mkono hoja ya Mhe. Waziri kwa wananchi wangu walionichagua wa Jimbo la Amani ninaunga mkono asilimia mia kwa mia. (*Makofi*).

**Mhe. Salim Abdalla Hamad:** Mhe. Spika, na mimi ninashukuru sana kwa kupata nafasi hii kuchangia kwa ufupi tu kuhusu hotuba ya Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais Mhe. Fatma Abdulhabib Ferej inayohusiana na makadirio ya mapato na matumizi ya mwaka wa fedha 2012/13.

Mhe. Spika, kwanza ni lazima nitoe pongezi za pekee kwa Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais kwa uwasilishaji mzuri wa hotuba yake. Pili nipongeze Wizara hii kuwa yenye majukumu makubwa sana. Kwa sababu majukumu ya kupambana na dawa za kulevya ni kazi nzito, uharibifu wa mazingira, ukimwi na walemavu. Haya ni mambo mazito na haya yote yanakusanywa katika wizara moja.

Mhe. Spika, mambo haya yanahitaji msaada wa kila hali ili wizara hii iweze kutekeleza wajibu wake ipasavyo. Kwanza Mhe. Spika, naomba kwa ruhusa yako kuzungumza kuhusu mazingira, maelekezo ambayo yametolewa katika kitabu hiki kwa urefu sana.

Mhe. Spika, mazingira ni kitu muhimu sana. Bila ya mazingira kuweka katika hali inayohitajika ni athari kwetu sisi na viumbe vyengine kwa jumla. Usafi wa mazingira ni kitu muhimu na cha lazima. Lakini Mhe. Spika, kwanza mimi nianze kusikitika kuwa tuna wizara kama hii iliyokuwa ina kazi ya kupambana na uharibifu wa mazingira.

Mhe. Waziri na hapa ninazo kumbukumbu zake alipokuwepo katika kamati ya *PAC*, alikwenda mpaka Malaysia ambapo ninasikia, kule watu wanajua namna ya kutunza mazingira. Leo tukaunda taasisi nyengine inayoshughulikia Baraza la Mji inachafua mazingira kiasi ambacho hakiwezi kustahamilika.

Mhe. Spika, kama utapita Darajani kwenye kituo cha Daladala kila asubuhi, hakuna kitu utakakiona kama harufu mbaya ya uchafu uliotupwa pale na haujaondolewa bado. Tunajua umuhimu wa usafi wa mazingira, na tukumbuke Zanzibar mazingira yaliweza kuleta maradhi ya kipindupindu kwa muda mrefu sana. Lakini sasa hali inarudi kuwa mbaya.

Mhe. Spika, ushauri wangu kwa vile kitabu kimeeleza kuwa shughuli zote za maendeleo zitafanywa kwa kuangalia hifadhi ya mazingira. Kuondoa uchafu kutoka sehemu moja ni maendeleo lakini kuuweka pahala pengine ni athari kubwa zaidi. Ningelimuomba Mhe. Waziri anayehusika na kuuweka uchafu ule ambao anaipa jina baya wizara hii, washirikiane kiasi ambacho vyovyote tusione ulazimu wa kukusanya uchafu pale kila siku na kuondolewa asubuhi, au pafanywe rai ile sehemu ya Baraza la Mji, ipelekwe katika wizara ili wizara iweze kujipanga vizuri kwa sababu katika sehemu nyengine imefanya vizuri sana.

La pili Mhe. Spika, mazingira ni aina nyingi na uharibifu wa haya mazingira siku zote unatokea kutokana na kazi za binadamu mwenyewe. Kuna wengine wanalima katika kutafuta maisha katika kilimo ambacho utaratibu wake haukubaliki ni kukata miti, halafu ukikata miti kunakua na mmong'onyoko wa ardhi, wengine wanafanya kazi hii hata kwenye vianzio vya maji, maji yanakauka na yanaleta athari kubwa sana.

Kuna wengine wanajenga viwanda. Hata Mhe. Saleh kaeleza hapa ni miradi ya maendeleo lakini matokeo yake inazalisha moshi wa carbondioxide na kadhalika ambayo ni yenye kuleta madhara kwa binadamu.

Kuna wengine wanavua wanatumia vifaa visivyofaa na badala yake wanachafua mazingira ya bahari. Kuna wengine kwa bahati mbaya na kwa kutokujua wanaagiza vitu vinaletwa hapa kama biashara, kumbe vitu vyenyewe vimeshaandikwa *used*. Na kitu kikishatumia na kukichukua wewe kwa kukitumia, maana yake hivyo vitu ni vibovu vinaharibu mazingira.

Mhe. Spika, hivyo wito wangu ni kuwa kwa sababu mazingira yanagusa kila wizara kwenye wizara tulizonazo 16 za serikali hii. Ningeliomba kuwe na mashirikiano ya kutosha. Kila wizara kwa upande wake kuona kuwa mazingira yanadumishwa na kuipunguzia kazi kubwa Wizara hii katika kuweka usafi wa mazingira.

Jengine Mhe. Spika, Wizara hii imejitahidi sana kutuelimisha kuhusu mambo ya *MKUHUMI* na tumeona athari ya kukata miti ovyo mpaka tukatakiwa tufanye rai ya kuonesha kuwa tunaipunguza gesi makaa wakati wenzetu huko wanaendelea kuingiza na sisi tukatakiwa tufanye hivyo. Kuna misumeno ya vyuma.

Sasa badala ya kufanya kazi wahusika katika kuimarisha mazingira tunazidi kuyaharibu. Kwa hivyo natoa nasaha kubwa sana kwa Wizara ya Kilimo, wao ndio wanaoruhusu miti kukatwa, wao ndio wanaojua misumeno wa moto, wahakikishe kuwa hii kazi inafanywa kiutaalamu kiasi ambacho miti mingi inapandwa, na ile inayokatwa ikatwe kwa sababu ya ruhusa maalum isiwe kama hivi sasa kila mtu kujifanyia anavyotaka.

Mhe. Spika, na umaskini tulionao unasababisha pia kuharibu mazingira. Tunajua kuwa pamoja na wenzetu walitoa sifa kubwa sana hapa kuwa tuna umeme kutoka Tanga na wapi na kadhalika, lakini kwa bei ya umeme huu ilivyo na umaskini ya watu walivyo ni kama kwa upande mwengine kuwaambia sasa kaingieni katika mazingira muzidi kuyafuja.

Miti inakatwa ovyo na ni lazima watu wafanya hivyo kwa sababu ya kupatia mkaa wa kupikia. Kwa hivyo ninatoa ushauri kama nilivyosema kuwa kila Wizara inahusika. Wizara inayohusika na mambo ya umeme ifanye ile rai tuliyokuwa tunaishauri siku zote ili tuone kuwa tumepata umeme wetu wenyewe utakaokuwa rahisi, tutakaoumudu na kuona kuwa hii hali ya kuharibu mazingira kwa sababu ya umeme tulionao imeondoka.

Mhe. Spika, ninarudia bila ya mashirikiano wizara hii haiwezi ikafanya kazi zake ipasavyo. Katika mazingira Mhe. Spika, kuna kuondoa kunguru kwenye kisiwa cha Unguja ambao wapo wengi ambapo Pemba wako kidogo tu.

Mhe. Spika, Mhe. Waziri kaeleza kwenye kitabu chake kuwa alitumia shilingi milioni thalathini na tano, na akaua kunguru 11596, na hiyo ni sawa sawa na shilingi elfu tatu na kumi na nane na senti thalathini kwa kila kunguru mmoja.

Mhe. Spika, tuna kunguru kwa malaki na kwa njia hii ya mitego na sumu maisha hawamaliziki. Kunguru ni moja ya viumbe ambao wana hadhari kubwa sana. Wakiona taabu imeongezeka kidogo wanaweza wakahama hapa wakaingia kwenye visiwa wakazaliana zaidi wakawa hawaondoki.

Sasa mimi ninaomba kama kuondoa kunguru wote kwa kutafuta mitego na sumu, tutamaliza bajeti ya serikali hii kwa sababu hawa wanazaliana, wakiona hapa pana adha wanakimbia halafu utaona siku zote wanaongezeka na itakuwa pesa nyingi tunatumia. Kwa hivyo rai yangu kama uwezekano wa kitaalamu wa kutumia kutumiwa dawa fulani katika chakula au katika sehemu zozote ikawa hawa kunguru wanaishi lakini hawazaliani tena. Ninaamini mwisho wake wanaweza wakapungua kwa wingi kwa sababu ni viumbe itafika pahala watakufa. Kuliko kutumia pesa nyingi sana hizi kwa viumbe wanaoruka na kukimbia na waliokuwa wanalinda maisha yao.

Jengine Mhe. Spika, ni suala la walemavu. Mhe. Spika, tunajua Zanzibar ni moja ya nchi za dunia na tuna walemavu. Tuna walemavu wa viungo, wengine hawawezi kwenda, wengine hawaoni, wengine hawasikii na kadhalika. Kwa sababu wizara inashughulikia walemavu naamini ingekuwa wizara na ina nia ya kuona kila mlemavu anahitaji wamempa msaada huo, lakini uwezo haina.

Kwa hivyo mimi ninakuomba Mhe. Spika, yale mambo ya lazima ya kumsaidia mlemavu aweze kuendesha shughuli zake yanayoweza kutekelezeka, Mhe. Waziri ajitahidi kutafuta misaada popote na aliyekuwa kwa bahati mbaya mguu umekatika apate mguu, hana mkono apate mkono wa bandia, kiziwi apate *sound receiver* aweze kusikia ili wajione kuwa ni walemavu lakini tumewathamini na tumewaingiza katika *environment* ya wale waliokuwa wazima.

Mhe. Spika, kwa maana hiyo kuwepo na utaratibu kamili ya kuweza kupatiwa elimu yao ipasavyo, kwa sababu hivi sasa walemavu wengi hawajui chochote kutokana na ulemavu wao.

Mhe. Spika, ninaipongeza Wizara kwa kufanya usajili wa walemavu katika Wilaya nne za Pemba na kule wamepata walemavu wengi tu, lakini nimesikitishwa kuona kuwa hakuna Wilaya hata moja hapa Unguja ambayo tathmini yake imechukuliwa. Kwa hivyo nikitaka nipate maelezo kwa Wilaya 6 za Unguja jee tumeziwekea katika utaratibu gani.

Mhe. Spika, jengine ni suala la ukimwi, ninakwenda kwa ufupi ufupi. Ukimwi ni maradhi ambayo yakimpata ndio moja kwa moja ni safari tu. Isipokuwa inategemea mazingira lakini hayana dawa. Wizara hii inapambana na Ukimwi lakini sheria imeweka kuwa Zanzibar ni njema atakaye aje.

Mhe. Spika, sasa wamekuja watu *more than hundred percent*, ni watu waliokuwa wanaonesha hasa kuwa hapa pahala kwa mazingira yalivyo ni pabaya sana kwa ukimwi. Ndio niliposema bila ya mashirikiano hatuwezi.

Mhe. Spika, Zanzibar imeingiliwa na sitaki nieleze kwa sababu nitakuwa ninakiuka utaratibu. Lakini ukiifanya kuwa ni nchi mtu afanye atakavyo, kwa maisha haya tuliyo vijana wetu watazidi kuangamia siku hadi siku. Kazi yetu itakuwa ni kutoa ushauri nasaha pamoja na dawa za kuongeza umri lakini nguvu kazi hizi zitapotea moja kwa moja.

Mhe. Spika, ili Wizara iweze kufanya kazi isaidiwe kikamilifu. Wizara inayohusika na kuingia watu hapa bila ya mpangilio ifanye kazi kuona kuwa *at least* hii hali ambayo viashiria vya ukimwi ninafikiri nikisema hivyo Mhe. Spika, unanifahamu viweze kupungua vyenginevyo itakuwa ni *kutwanga maji kinuni* tu, hakuna lolote litakalokuwa.

La mwisho Mhe. Spika, kwa mujibu wa mtiririko wa wizara hii, kuna dawa za kulevya. Mhe. Spika, ulevi ni kitu kibaya sana kweli kweli. Mhe. Spika, kitu cha aibu kabisa katika nchi hii ni ulevi. Ulevi unaoingia ulevi huu ninashukuru kuwa haufanywi hapa Zanzibar lakini unaingizwa Zanzibar. Kitabu hakikueleza ni namna gani wizara itapambana na wanaoingiza ulevi katika kisiwa hiki au katika visiwa hivi vya Unguja na Pemba. Kimeeleza tu kuwa kitapambana tu na biashara ya ulevi.

Kwa hivyo kama ulevi unachukuliwa kuwa ni biashara, ninafikiri hili si jina zuri Mhe. Spika. Mhe. Spika, Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano ndio yenye sehemu kwenye bahari na anga ya kuingiza watu Zanzibar na kutoka Zanzibar kwenda sehemu nyengine. Ifanye kila utaratibu na kwa kuangalia hali ya vifaa vyetu vilivyo, kuna bandari za kawaida na bandari za vichochoroni, tuone kuwa mtu yeyote atakayeingia hapa kwa vile tumeanzia na uongozi wa Masheha ambao wanasifiwa sana kwa kazi zao, waanze na wao kuwahamasishwa kikamilifu, tena ikiwezekana hata kuahidiwa kuzawadiwa atakayefanya kazi vizuri ya kupambana na walevi. Tuone kuwa mtu yeyote atakayeingia na ulevi katika visiwa hivi anaadhibiwa ipasavyo.

Vyenginevyo Mhe. Spika, tutaendelea na kupambana na ulevi na dawa za kulevya yatakuwa yanaingizwa hapa, na yakiingizwa hapa yanatuathiri kama tunavyoona. Ninashukuru Wizara kwa kiasi fulani wale wanaolala ovyo wamepungua lakini bado dawa zinaingizwa. Hiyo ni kwanza.

Mhe. Spika, la pili kuna ulevi mkubwa. Sana. Kuna ulevi wa bangi. Kuna wengine ninasikia wanapanda hapa hapa Zanzibar na wengine wanachukua kutoka kwa ndugu zetu wa damu. Ninashangaa mtu anaonekana huyu keshalewa bangi, kama kweli serikali ipo makini isiweze kumdhibiti mpaka akajua bangi ile kaipata wapi na kauziwa na nani ili suala hili likaondoka.

Mhe. Spika, ninasikika sana siku hizi hali inapungua. Mimi nilikuwa nina ushahidi pale bandarini Wete Pemba, watu wakipita na bangi kutoka Tanga wala walikuwa hawaulizwi chochote. Lakini ninashukuru tokea kuzama ile meli mambo haya kidogo yamepungua. Lakini bado bangi inaingizwa kwa nguvu hata kwa zile njia ambazo si za kawaida.

**Mhe. Spika**: Una dakika 2.

**Mhe. Salim Abdalla Hamad:** Mhe. Spika, kuna watu wanapiga gongo. Zamani ilikuwa askari wakifanya kazi mpaka vile vibuyu na kadhalika wanavitia moto, yale mambo wanayaharibu moja kwa moja, siku hizi hapashughulikiwi. Ulevi unakuwa unaachwa ovyo ovyo.

Mhe. Spika, ili tuweze kufika katika malengo tuliyokusudia na wizara hii ifanye kazi nzito iliyopangiwa tuisaidie ipasavyo ili ulevi, halafu mambo haya niliyoyazungumza ya ukimwi na mambo mengine yaweze kuondoka kwa maslahi yetu na taifa letu na watoto wetu. Mhe. Spika, ninashukuru ahsante sana.

**Mhe Mtumwa Kheir Mbarak:** Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia afya na uzima kwa kuweza kutekeleza majukumu yetu.

Lakini pili nimpongeze Mhe. Waziri kwa sababu ana kila sifa ya kupongezwa ni mwanamke lakini anafanya shughuli zake kwa umahiri.
Mhe. Spika, na mimi nitatoa mchango wangu kidogo kwa kuwa wenzangu wengi wameshazungumza, na ukitazama kitabu hiki uzungumze humo kwa humo. Mimi nitaanza katika Idara ya Mazingira.

Mhe. Spika, Mwenyezi Mungu alipoumba kwanza alitanguliza kuumba miti ili kuja kuweka mazingira mazuri katika ardhi. Miti hiyo ndio itakayoweka hali ya hewa nzuri katika ardhi. Hapo hapo Mwenyezi Mungu ndipo akaja akamuumba mwanadamu. Tizama hekma ya Mwenyezi Mungu kwanza alitanguliza miti, halatu ndio akaja binadamu ili atakapokuja katika ulimwengu akute hali ya mazingira ipo vizuri. Kwa hivyo baadae alipokuja Mtume wetu (SAW) hapo tukapewa amri. Katika katika Korani yake akasema, *walaa tufsiduu fil ardhi baada iswlaahiha,* ina maana musiharibu ardhi baada ya kutengenea kwake. Nani kapewa amri hiyo, kwa hivyo amri hiyo tumepewa sisi na kama viongozi basi hapo pana amri ya kuilinda ardhi kuwa isifisidiwe baada ya kutengenea kwake.

Kwa hivyo mimi ninadhani Mhe.Spika, mwenye jukumu la kulinda ardhi ni viongozi waliokuwepo. Hivyo hili ni jukumu tosha, ni amri inayotoka kwa Mwenyezi Mungu ili tuhifadhi ardhi. Kwa hivyo Mhe. Waziri nakuomba una jukumu kubwa la kutekeleza hilo.

Mhe. Spika, Mhe. Saleh alisema hapa kuwa serikali haipo makini juu ya kutunza mazingira, inaonesha labda ndio ile tunayosema kwamba kuna kitu cha kuona haya na taabu. Lakini mimi ninadhani tujue hilo ni jukumu na amri imetoka, halikutoka ombi imetoka amri.

Lakini Mhe. Spika, kuna suala zima la uharibifu wa mazingira, na halafu kuna suala zima la uchafuzi wa mazingira; ni vitu viwili tofauti. Mhe. Spika, suala zima la kuchimbwa mchanga, lakini ukitazama na huo mchanga wenyewe unaochimbwa tunajenga. Kila anayejenga anataka mchanga. Nadhani hakuna nyumba hata moja inayojengwa isitumie mchanga.

Lakini sasa ni jukumu Mhe. Spika, la kuweka kima kizuri cha kuchimbwa ule mchanga, na pakisha pale basi papandwe miti. Hili ni jukumu ambalo la kusimamia. Ndio utakuta mengi hata hiki kitabu kinaonesha huku nyuma, handaki hili lakini pahala panaonesha athari iliyotokea ndio hii, hapana chengine chochote. Kwa hivyo hii ndio unaikuta athari kubwa usimamizi na kupata taaluma ya hayo.

Kwa hivyo Mhe. Spika, Mhe. Waziri naomba kwa hili nadhani ni kazi kubwa ipo ya kuona kulinda haya mazingira yetu. Lakini jengine Mhe. Spika, hapo hapo kuna suala ambalo la huu ukataji miti Mhe. Salim kagusia hapa alisema unasababishwa na umaskini. Leo makaa tunataka tunayatumia, kuni zinatumika lakini ukija twende katika mbadala kuna gesi, gesi hainunuliki.

Mimi mwenyewe nina jiko la gesi nimeanza kununua tangu ninatia gesi kwa shilingi kumi na nne, ikaja shilingi kumi na sita, ikaja kumi na nane, ikaja ishirini, ikaja ishirini na mbili na ishirini na nne. Inakwenda tu kweli mnyonge ataweza kutumia gesi. Kwa hivyo hii hali lazima tukae tuwe makini, kwa hali hii ikiwa hatukuweza kupanga mipango yetu mizuri, tukaona umeme na gesi unakuwa katika hali nzuri, uchafuzi wa mazingira utazidi.

Mhe. Spika, ukija katika uchafuzi wa mazingira. Kwa kweli mji wetu ni mchafu mno lakini mimi hapa ningeomba nimuulize Mhe. Waziri, sijui anashirikiana vipi au ana mashirikiano vipi na Baraza la Manispaa ili kuondoa tatizo hili.

Baada ya hapo nizungumzie kidogo kwenye suala la dawa za kulevya. Kwenye ukurasa wa 31 Mhe. Spika, Mhe. Waziri katika malengo yake *item number one* inasema, “Kuratibu na kuendeleza mapambano dhidi ya uingizaji na usafirishaji wa dawa za kulevya”. Mhe. Spika, tuliwahi kupata semina moja tukaelezwa kuwa hili suala lina

mtandao mkubwa. Kwa hivyo mimi hapa ndio nikapata mtandao wasi wasi, na kweli linaonesha kuwa lina mtandao mkubwa.

Sasa nimuulize Mhe. Waziri katika huu mtandao mkubwa uliokuwepo, kama yeye ni Waziri na ninajua ni mwanamke, maana yake halikumgusa yeye suala hili basi limemgusa ndugu yake au jamaa yake na sote limetugusa na linatuathiri sana suala hili, kukamatwa vidagaa vidogo vidogo mapapa yakaachiwa.

Sasa Mhe. Waziri utapambana vipi na mtandao huu, vipi ulivyojipanga kupambana na mtandao mkubwa. Siku moja niliangalia televisheni kulikuwa na kanda moja, bosi kakaa juu ya kiti, huku anakaa anatoa masemina kwamba msiingize dawa za kulevya na anayeingiza dawa za kulevya itakuwa hivi na vile. Lakini yeye kumbe tayari ndio mfanyabiashara mkubwa, kisha anapiga simu kuwa hivi sasa ulinzi uende bandari ya Malindi lakini wale watu wake anawapitisha katika bandari ya Uzi.

Kwa hivyo mimi nikaanza kujiuliza inaonesha hii ndio mipango inayotumika. Huku akikaa anasema leo mzigo utapitishwa katika bandari ya Uzi, lakini wale watu wake wenye kuleta dawa anawaambia piteni bandari ya Malindi. Ndio inavyoonesha hii hali kwa sababu kama kupungua dawa za kulevya zingekuwa zimeshapungua humu ndani na wasingevuta wavutaji kama sikuingizwa.

Nina imani mtu hafanyi kitu wakati kipo na kikawa hakipo hakitumiki. Kwa hivyo mimi ninahisi suala hili lishakuwa kero kuliko hiyo kero ya Muungano. Utapambana nalo vipi hili. Mhe. Spika, mimi ninadhani hili suala tuwe makini. Mara nyingi na huko nje wananchi wanasema viongozi wenyewe hawajawa tayari kuliondosha suala hili na ikiwa tayari hili litaondoshwa.

Mifuko ya plastiki ipo wapi, inatumika haitumiki kwa kuwa haipo na kama ipo ingetumika. Kwa hivyo mimi ninahisi hili suala tuwe s*erious* kwa suala hili, taifa linapotea, mbali ya kuwa utawachukua na kuwapeleka huko *Sober House* hata wakitoka kauli zao zile zile, wanatwambia wenyewe hata wakitoka hatuaminiwi, hawa watu wetu wengine hawatutaki.

Kwa hivyo hili ninahisi Mhe. Waziri ninajua wewe ni mwanamke, na Rais hakukosea kukuweka wewe mwanamke. Pahala palipokuwa na matatizo yoyote ambalo linagusa ini la mzazi akiekwa mwanamke nina imani patakuwa na mafanikio makubwa.

Mhe. Spika, ninadhani nigusie jengine ambalo hili ni jinamizi la taifa suala la Ukimwi. Mhe. Spika, ulipoanza huu ukimwi tuliukaribisha vibaya baada ya kuingia tu tulishindwa kukinga. Ninasema siku zote kuwa kitu chochote kikiingia basi ukiwahi mwanzo, waswahili wanasema *udongo upate ulimaji*, ukishakauka huwezi kuupinda tena au *samaki mkunje bado mbichi*, na ile chechea ndogo inawasha shamba lote. Kwa hivyo lilipoingia tu hili suala la ukimwi tulishindwa sisi pale kujipanga vizuri.

Mhe. Spika, ulianza ukimwi huu kuupamba na kuwawekea kinga, tukauvishia soksi, tukauvishia *rain coat*. Mtu atakuwa na hofu, hana hofu. Mhe. Spika, nimetizama hiki kitabu katika kiambatanisho nambari 14, kuna idadi ya makundi maalum waliofikiwa kwa elimu mrika Unguja na Pemba.

Lakini baada ya kuona hapa Wilaya zote zilizofikiwa, huduma zilizotolewa. Huduma ya kwanza katika Wilaya ya Mjini na Wilaya zote kupatiwa elimu ya ukimwi, ushauri nasaha, usambazaji wa kondomu. Mimi nikajiuliza sasa tushaisambaza hii kondomu na waliopatiwa masuala haya yote ni wanaume wanaofanya mapenzi na wanaume wenzao. Mimi Mhe. Waziri nikiuliza hapa tu maana yake hili suala limeshazungumzwa siku nyingi, na mimi nimeshazungumza sana, jee huu usambazaji wa kondomu waliopelekewa tunakwenda kuondoa tatizo au kuzidisha tatizo.

Kwa sababu humu ni binadamu Mhe. Spika, nimepewa mimi elimu na ukishanipa elimu, ninadhani wengi wanakaa kwenye madrasa wanasoma na wanaambiwa hasa. Lakini lile linalom-*touch* mtu katika nafsi yake kuliacha lina taabu. Ninadhani siku zote madrasa mawaidha alhamdullilah, mawaidha yanatoka. Mwanamke anatakiwa ajihifadhi vipi, taaluma. Lakini unapochukua hii kondomu na kumwambia hii ni kondomu, wakati imani yangu ishakuwa dhaifu sitaki kuliacha hili suala, ina maana unanichangia unaniambia nikafanye.

Hapa hukunipa msaada. Unaniambia nikafanye. Kwa hivyo hili Mhe. Waziri ni tatizo. Hivi sasa Mhe. Waziri nikwambie watu wanasema bora uugue sukari, anaogopa mtu maradhi ya sukari kuliko ukimwi. Kishafikia mtu kusema hivyo una nasaha gani ya kumpa.

Mimi nilidhani kwamba patatolewa adhabu juu ya watu hawa. Ukishawajua kuwa watu hawa wanafanya wanawake kwa wanawake au wanaume kwa wanaume. Lakini unachukua na kondomu unawaambia hii unaposhindwa kupokea elimu fanyeni hivi. Mimi naona haikunikalia sawa hata isipokuwa hapa kinachoonesha kushajihisha tu hili suala.

Kwa hivyo Mhe. Waziri nadhani hili suala uje unipe taaluma pengine ufahamu wangu wa elimu ni mfupi, hapa unaondoa tatizo au unazidisha tatizo? Ikiwa unaondoa tatizo, hivi kusambaza kondomu, na kama ni hivyo kusambaza kondomu kuondosha ukimwi ungekuwa umeshakwisha zamani. Nilisema siku moja kama ukimwi utaondoka kwa makongamano basi utaondoka. Huwezi ukajua tathmini ya ukimwi mpaka utasikia leo kuna maziko hapo, kafa nani? Mtu mbwana kaguswa na mawaya. Unajua kumbe upo, leo kuna faradhi hapo, haya kaondoka nani, baba mzazi kaondoka lakini na mama mzazi yupo taabani. Unajua ile hali kwamba hili suala lipo na linateketeza.

Kwa hivyo hili suala la kusema kwamba tunapokwenda kutoa taaluma na elimu, elimu mtu apewe ipo lakini ni suala ambalo linakuja na hatari yake ni hiyo. Ninadhani Mhe. Waziri Mhe. Spika, mimi kwa hili kidogo uje nisaidie hapo.

Mhe. Spika, muda wako naona umemalizika, nilikuwa na moja lakini basi ni mtu mzima ninakuheshimu baba yangu. Kwa hivyo ninaunga mkono hotuba hii kwa asilimia mia moja.

**Mhe. Spika:** Waheshimiwa Wajumbe kuna wachangiaji kama watano waliobaki, ninategemea jioni kwa kutumia muda vyema na kutorejea, basi tunaweza tukamaliza hao na baada ya hapo ikawa ni zamu ya majumuisho na hatimae kupitisha vifungu.

Watano wa jioni ni pamoja na Mhe. Mohamed Said Mohamed ambaye alipata dharura kwa muda mrefu hapa akawa hayupo, mwengine Mhe. Hamza Hassan Juma, Mhe. Abdalla Mohamed Ali, Mhe Mohamed Mbwana Hamad na Mohamed Haji Khalid. Hawa wanatosha kumaliza mchango kwa hoja hii.

Kwa hivyo baada ya hayo Waheshimiwa Wajumbe tusitishe shughuli zetu hadi saa 11.00 jioni.

*(Saa 7.00 mchana Baraza liliahirishwa hadi saa 11.00 jioni)*

*(Saa 11:00 jioni Baraza lilirudia)*

*(Majadiliano yanaendelea)*

**Mhe. Abdalla Mohamed Ali:** Ahsante Mhe. Naibu Spika, na mimi Alaasiri hii kunipa fursa ya kuzungumza machache kuhusu mpango huu wa mapato na matumizi ya Wizara ya Nchi Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais.
Mhe. Naibu Spika, mara nyingi tunapokuwa madereva na kuingia barabarani tunatakiwa tuwe waangalifu sana na tusiwe tunaangalia yale ambayo yako mbele tu. Tunatakiwa tuangalie na yaliyopo pembeni mwetu, yanayokuja nyuma na pia tuzingatie kwamba barabarani kuna waliokuwa hawaoni na waliokuwa hawasikii hata ukiwapigia honi, na vile vile kuna wanyama ambao nao wana fursa na haki ya kutumia barabara hizo.

Mhe. Naibu Spika, wengi tumezungumzia mazingira hapa, na ni kweli hivi sasa katika nchi nyingi ulimwenguni, kipaumbele chao kikubwa ni kuzingatia kwamba mazingira hayachafuliwi, kwa kuogopa labda dunia yetu inaweza kubadilika mwenendo wake, badala ya kuanzia Mashariki ikaja kuanzia Magharibi.

Mhe. Naibu Spika, ni jambo zuri na tunapaswa na sisi tuliendeleze katika nchi yetu, kwani na sisi tumo katika mfumo huo huo wa dunia, tunatakiwa tuyatunze mazingira. Mhe. Mtumwa hapa alisema sana kwamba ardhi ndio iliyokuja mwanzo kuliko sisi watu, kwa kujua kwamba tukifika sisi mwanzo labda tusingekuwa na pa kufikia, lakini ilifika hii ardhi mwanzo ili tuone ule umuhimu wake kwamba kuwepo kwake ndio kulikotufanya sisi tuweze kuendelea na maisha yetu.

Mhe. Naibu Spika, mimi kidogo nataka niende kinyume na labda wengi waliozungumza, kwa nini basi. Kama nilivyosema mwanzo kwamba tunapokuwa barabarani tunatakiwa tuzingatie mambo mengi sana, na mimi katika suala la mazingira nasema tuna umuhimu wa kuona mengi na kuyazingatia mengi.

Mhe. Naibu Spika, mara nyingi serikali yetu inapokuwa inataka kutekeleza jambo lake, inakwenda mbio mno. Hivi karibuni tulipiga marufuku uingiaji wa mifuko ya plastiki ni kweli kwamba mifuko hii labda ingekuwa na athari katika mazingira yetu. Lakini Mhe. Naibu Spika, ukweli ni kwamba uingizwaji wa mifuko ya plastiki ilikuwa ni biashara, kwa maana hiyo watu walichukua mikopo wakaingiza katika biashara hii, kwa maana hiyo ikawa maisha yao kwa asilimia mia moja wanatarajia biashara yao hii ya kuleta mifuko kutoka nje ya nchi. Kwa hivyo, mara moja serikali yetu ikapiga marufuku kwamba mifuko hii sasa hitakiwi iingie katika nchi hii, bila ya kuzingatia kwamba huyu ambaye anaileta hii mifuko ataathirika kwa kiasi gani.

Kwa hivyo, mimi ningewaomba tu wahusika katika kufanya maamuzi wakaangalia kwamba je, wakati wa kufanya tathmini ya uharibifu wa mazingira je na jamii nayo wanaifanyia tathmini kwamba uamuzi wetu utawaathiri wananchi kwa kiasi gani. Sambamba na hilo ni kwamba sio hao wanaoleta mifuko ya plastiki tu, lakini Mhe. Naibu Spika, kuna wananchi wengi ambao wanajishughulisha na uvuvi wa kutumia nyavu. Punde tu kuna baadhi ya nyavu ambazo zimeambiwa zinaharibu mazingira, lakini wananchi hawa wakaambiwa kuanzia sasa hamtakiwi kutumia tena nyavu hizi, lakini hawa hawakuwezeshwa, hawakufanyiwa fidia yoyote. Sasa kila siku tunafukuzana baharini, na watu hawa na tunawapeleka ndani, tunawachukulia nyavu zao, lakini tunawakosesha ajira, kwa sababu ajira yao kubwa inategemea kule baharini na nyavu zao.

Kwa hivyo, Mhe. Naibu Spika, ningeomba kwamba wakati wa kufikia maamuzi kama haya, basi tungeyazingatia haya mengine kwamba kutakuwa na watu ambao na wao wataathirika, sio mazingira peke yake yatakayoathirika kuna na watu wataathirika, ajira zao na maisha yao wanategemea humo. Sambamba na watu hao pia kuna wale ambao wana misumeno, na wao pia labda kuna utaratibu gani sijui serikali imeandaa au wizara ya kuwapa fidia au kuwalipa ile misumeno yao wasiitumie. Kama si hivyo Mhe. Naibu Spika, mimi naona itakuwa ni vita tu vya kupigishana mbio, kwa sababu hawa kwa asilimia kubwa wanategemea zana zao vile kwa ajili ya kuendeshea maisha yao.

Mhe. Naibu Spika, ili watu hawa watulie na ili Idara au wizara ijitosheleze kwamba kwa hivi sasa mambo haya hayatumiki, basi labda wangeinunua. Kuna misumeno inauzwa milioni moja, milioni mbili wengine. Sasa Wizara ingejipanga kwa hilo, wakawaambia kwamba kwa sababu mnaharibu mazingira, basi sisi tutainunua misumeno yenu na badala yake nyinyi hizo pesa zenu mtakazozipata muingie katika ajira nyengine. La si hivyo, basi itakuwa ni kufukuzana tu.

Kwa sababu hivi sasa Mhe. Naibu Spika, wale wenye misumeno hawatumii tena kwa mchana, wanakuwa mara nyingi wanatoka wakati wa usiku, wakisubiri labda hao askari walioko huko maporini hawapo tena, wao ndio wanafanya shughuli zao, ukiamka alfajiri unaona mbao na vifaa vyao vyengine viko barabarani. Kwa hivyo, ninachosisitiza hapa ni kwamba ni lazima Wizara iangalie nayo, kwamba tunapofanya tathmini, basi na hawa wapigiwe tathmini vile vile, kwamba na wao wataathirika kama vile Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano inavyofanya tathmini ya mazao au nyumba ili kuwapa fidia wale wananchi watakaoathirika, basi na wizara hii iangalie kwamba ili kudhibiti mambo haya basi hawa watu wanafanyiwa kitu chengine mbadala, ili wasiingie katika shughuli ile na kuendeleza kuangamiza hayo mazingira yenyewe.

Mhe. Naibu Spika, tunazungumzia suala la ukimwi. Ukimwi ninachokijua ni suala la kimataifa na hivi sasa ulimwengu mzima unapigia kelele suala hili au umo mbioni kulitafutia ufumbuzi suala hili. Sisi hivi sasa katika nchi yetu tuna watu ambao wanaingia kutoka nchi tofauti. Kuna wale ambao wanakuja kutafuta ajira, na kuna wale ambao wanaingia kwa ajili ya kuja kufanya kazi. Tulikuwa tunalalamika sana kwamba nchi yetu hivi sasa hasa katika sekta ya utalii, walioajiriwa katika sekta hii wengi ni wageni na hilo ni kweli. Lakini sijui Wizara imeandaa utaratibu gani kwa wale ambao wanaingia na kuja kufanya ajira au kujipatia ajira katika nchi yetu wakati wanapoomba vile vibali, huwa na wao wanafanyiwa uchunguzi kwa maradhi haya.

Mhe. Naibu Spika, kwa nini nikasema hivi. Kwa sababu hivi sasa katika nchi za Ufalme wa Kiarabu nchi za *Emirates,* kama unaomba ajira basi kitu cha mwanzo unachotakiwa ukioneshe mbele yao ni uthibitisho kwamba wewe sio muathirika, si hivyo basi huwezi kuingia katika nchi ile na wala huwezi kupewa kibali cha kufanyia kazi. Sasa sijui katika nchi yetu hii kuna utaratibu kama huo uliowekwa, wa kuona kwamba wanaoingia na kupatiwa ajira,

na labda wale ambao wanatoka katika zile nchi ambazo zimeathirika zaidi na tatizo hili la ukimwi. Je, watu wale wanakuwa na utaratibu maalum, na labda kuna sheria ambayo inatufanya kwamba mtu kama amebainika kufanya hivyo, hatakiwi kufanya kazi katika nchi yetu.

Lakini Mhe. Spika, suala hili limekuwa ni zito sana, kwa sababu maadili yake naona yanaturudisha nyuma. Hadi hivi sasa suala la ukimwi nafikiri tunaliogopa kuliweka hadharani. Kwa nini nasema hivyo Mhe. Naibu Spika, kwa sababu maadili yanatukataza kwamba mtu labda akiwa na tatizo hili, hatakiwi labda ajulikane na wenzake na inafika wakati kwamba mtu anajulikana kuwa huyu katangulia mbele ya haki kwa sababu ya tatizo hili, lakini mpaka hivi sasa huwezi kumsikia mtu akitangaziwa rasmi kwamba mtu huyu kaondoka katika dunia hii kwa sababu ya tatizo hili. Kwa maana hiyo labda kama angekuwa aliondoka, lakini akajulikana kwamba huyu kaondoka kwa tatizo hili, basi ingekuwa ni taarifa tosha kwa wale wengine kujua kwamba yule aliyeondoka alikuwa moja, mbili na tatu. Kwa hivyo, mimi natakiwa kuchukua hadhari moja, mbili na tatu. Kilichobakia sisi kama alivyosema Mhe. Mtumwa Kheir ni kuwaendeleza zaidi kufanya tukio lile, kwa kuwapatia mambo ambayo labda hayana uhakika kwa asilimia mia moja kwa kuondosha tatizo hili.

Mhe. Naibu Spika, sasa niingie kidogo katika tatizo ambalo mimi nasema uwezo wa kuliondoa moja kwa moja hatuna. Tatizo hili ni la dawa za kulevya. Mhe. Naibu Spika, hebu tukumbuke kwamba tatizo hili ni vita, lazima tujue kwamba tatizo hili ni vita. Vita baina ya nani na nani, hii ni vita baina ya matajiri wa dawa za kulevya na wale ambao wanakataza dawa hizi.

Mhe. Naibu Spika, nchi kubwa kama ya Marekani ina mkakati maalum wa kupiga vita tatizo hili. Hivi karibuni baada ya miaka nenda miaka rudi, walifanikiwa kumdhibiti Pablo Escobar ambaye alikuwa ni tajiri mkubwa wa dawa hizi, lakini walitumia pesa nyingi sana katika kumdhibiti. Sasa sijui hapa kwetu na kwa vile biashara hii hasa haianzii hapa kwetu, sijui kuna mashirikiano gani kati ya nchi yetu na yale mataifa ambayo yanajulikana ulimwenguni kwamba wao ni wasafirishaji wa dawa hizi.

Mhe. Naibu Spika, lakini katika hili, kama nilivyosema sitaki nizungumze sana, kwa sababu inanikumbusha miaka miwili iliyopita kwamba Mhe. Mjumbe mmoja mwanamke wa Bungeni, aliwahi kulizungumza hili katika Bunge. Lakini kwa mshangao tu kwamba baada ya muda mchache, mama yule aliondoka katika dunia hii. Kwa hivyo, hili sio tatizo la kwamba sisi tuje tuseme hapa moja, mbili na tatu, kwa sababu mimi mwenyewe hapa ninayezungumza ninahofia kwamba sijui leo itakuwaje, kwa sababu hii ni biashara ambayo inamilikiwa na matajiri wakubwa.

Kwa maana hiyo Mhe. Naibu Spika, kuna mambo mengi ambayo yanatokea na kubwa linalotokea katika matatizo haya kuhusu suala hili, ni kwamba ule ushirikiano baina ya vyombo vya dola haupo kwa sababu inatokea katika jamii zetu, tunamgundua mmoja anahusika katika matatizo haya kwa tuhuma. Lakini utakapofika katika vyombo vya dola, basi unamuona mtu huyu kwa siku ya pili tu tayari ameshapata dhamana yuko nje, na kutokana na kuwa waliomfadhili wana uwezo kwa kiasi kikubwa, basi kesi yake mara nyengine inaishia hujui wapi. Kwa hivyo, bado watu hawa

**Mhe. Naibu Spika:** Mhe. Mjumbe bado dakika tano.

**Mhe. Abdalla Mohamed Ali:** Ahsante Mhe. Naibu Spika, kwa hivyo unakuta watu hawa wanaendelea kuwepo katika jamii, na wala hakuna hatua zozote zinazofikishwa, kiasi kwamba sisi tuliomo katika majimbo kuna sehemu tumeanzisha polisi jamii na wanasaidia sana katika shughuli hizi. Lakini wanarudi nyuma kwa sababu wanamuona mtuhumiwa ambaye wamempeleka katika vyombo vya hukumu, siku ya pili yupo na wala hana hatia yoyote ambayo anapatiwa. Kwa hivyo, mimi ningeomba tu kukawa na ushirikiano mkubwa kati ya vyombo vinavyohusika katika suala hili.

Kwa sababu sisi tunaliona na tunaliweka kwamba dawa za kulevya, lakini msingi wake mkuu ni utajiri, kwa hivyo hakuna yeyote yule ambaye atakuwa yuko tayari kunyang'anywa utajiri wake.

Mwisho Mhe. Naibu Spika, labda katika kitabu chetu tumeelezwa tu kwamba kuna wale wanaume kwa wanaume ambao wanaingiliana kijinsia, na kwa Ripoti ya Mjini Magharibi kuna watu wasiopungua 40. Hivi karibuni Waziri Mkuu wa Uingereza David Cameroon, yeye alikuwa na wazo lake na akaomba labda ulimwengu waliruhusu suala lile liwepo. Baada ya kutokea suala hili sisi hapa Tanzania nafikiri tulitoa makero yetu. Sasa sijui serikali hivi sasa inatuambia tu kwamba kuna watu wanaofanya vitendo kama hivi katika nchi yetu na waendelee kuwapa ushauri

nasaha na condom, lakini hakuna tamko rasmi kwamba tendo hili hatulitaki au tendo hili litatufikisha hatua fulani, kwa maana hiyo kutungwe sheria maalum. Mhe. Naibu Spika, naomba nimalizie hapo, ahsante.

**Mhe. Mohamed Mbwana Hamad:** Ahsante Mhe. Naibu Spika, kwanza na mimi nachukua nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia jioni hii kuwepo hapa katika kutekeleza majukumu yetu. Pia nachukua nafasi ya kukushukuru wewe Mhe. Naibu Spika, kwa kunipa nafasi ya kuchangia angalau mawili au matatu katika bajeti hii ya hotuba ya Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais.

Vile vile Mhe. Naibu Spika, nichukue nafasi tena ya kumpongeza Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais, kwa jinsi alivyoiwasilisha hotuba yake kwa ufasaha na kwa upeo wenye kufahamika sana. Pia nawapongeza watendaji wake wote walioshirikiana naye katika kukamilisha kitabu hiki, ambacho sasa kiko mbele yetu tunakitolea maelezo na maelekezo.

Mhe. Naibu Spika, mimi mchango wangu nitaanzia na Idara ya Watu Wenye Ulemavu. Mhe. Naibu Spika, watu wenye ulemavu kwa kweli ni binadamu kama binadamu wengine, lakini Mwenyezi Mungu tu kawapa mitihani ya ulemavu ili iwe ni majaribio kwao na majaribio kwetu sisi ambao bado tuko katika hali ya viungo salama. Kwa maana hiyo watu hawa wanahitaji kutunzwa, kulelewa na kuthaminiwa kama anavyothaminiwa mtu mwengine ambaye ana viungo kamili.

Mhe. Naibu Spika, watu wenye ulemavu wanahitaji kupewa fursa sawa sawa na watu ambao wana viungo salama. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri watu hawa awaangalie vyema na awape fursa mbali mbali katika ofisi yake, na aungane na wizara nyengine ili kuhakikisha kwamba watu hawa wanapewa vipaumbele katika mahitajio yao ya aina mbali mbali ambayo wanayahitaji.

Kwa mfano, tunao vijana wengi ambao wana ulemavu hivi sasa wanasoma. Kwa hivyo, katika kusoma kwao kunahitaji kuendelezwa muendelezo ya hali ya juu kabisa. Mhe. Naibu Spika, napenda nizungumze kwamba watu hawa wenye ulemavu Mhe. Waziri unapaswa uungane na Waziri wa elimu ili watu hawa wenye ulemavu watakapofika katika kiwango cha elimu ya juu, basi wapewe vipaumbele katika kupewa mikopo kwa ajili ya kuendelea na elimu ya juu na mengineyo. Lakini pamoja na hayo, watu hawa inapaswa pia katika masuala ya matibabu waangaliwe vizuri zaidi, na ikiwezekana wanapofika katika vituo vya afya na hospitali basi wasiwekwe katika foleni, ili wasipate usumbufu kutokana na hali zao. Ikiwezekana watu hawa wawekewe maeneo maalum ya kufanyiwa matibabu, ili iwe ni urahisi kwao kukaa katika maeneo yale ambayo yanatolewa huduma za matibabu.

Pia niziombe Wizara za serikali hasa zinazojengwa hivi sasa na majengo mbali mbali yaweke majengo maalum ambayo ni kwa ajili ya watu wenye ulemavu, ni rahisi kwao kupata kuingia na kutoka katika majengo hayo. Vile vile Idara hii ipatiwe nyenzo za kuweza kufuatilia watu hawa wenye ulemavu katika maeneo mbali mbali ambayo wanaishi.

Mhe. Naibu Spika, nikiondoka hapo nataka niingie kidogo katika suala zima la mazingira. Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak nataka nimnukuu kidogo hapa, alizungumza jambo muhimu sana, kwamba Mwenyezi Mungu alipoiumba hii dunia, kisha akaumba miti, halafu akatuumba sisi wanadamu. Sasa miti hii tumeikuta sisi. Alitumia maelezo ya aya hapa, alisema kwamba 'baada ya kwisha kuumbwa sisi Mwenyezi Mungu alituambia kwa kupitia ndani ya kitabu chake kitukufu kwamba msifanye uharibifu katika ardhi baada ya kutengenea kwake'. Ina maana kwamba hapa tunahitajika sisi wanadamu tulinde misitu na tuiendeleze.

Kwa hivyo, kutokana na hali halisi ilivyo hivi sasa watu wengi sana wanakata misitu ovyo. Nikisema wanakata misitu ovyo ni kwamba hakuna sheria ambazo zinawadhibiti mpaka hivi sasa Zanzibar yetu imekuwa kama jangwa, sehemu nyingi ambazo zilikuwa na miti, sasa hivi miti imetoweka kabisa, kwa sababu ya kukatwa kwa wingi kwa ajili ya matumizi ya kuni, mkaa na kupiga chokaa.

Mhe. Naibu Spika, kama hatukuwa makini, basi visiwa vyetu hivi baada ya muda mchache tu vitakuwa havikaliki kwa joto, pamoja na matatizo mbali mbali ambayo yataathiri kwa kiasi kikubwa afya zetu. Kwa hivyo, ningemshauri Mhe. Waziri anayehusika na suala zima la mazingira, awe makini kuzisimamia sheria zilizopo ili mazingira yetu yawe katika hali nzuri.

Mhe. Naibu Spika, miongoni mwa uharibifu wa mazingira ambao unaendelea katika nchi yetu au katika visiwa vyetu vya Unguja na Pemba, ni uchimbaji wa mchanga usiokuwa na kiwango, pamoja na uchimbaji wa mawe na uchimbuaji wa matofali usiokuwa na kiwango.

Kwa hivyo, ningemuomba Mhe. Waziri kwamba taratibu ambazo zimewekwa kuwa ardhi ichimbwe kiasi fulani katika sehemu za michanga, na mawe yachimbwe kiasi fulani, basi isiendelee kuchimbwa kima kikubwa zaidi, na hizo sehemu ambazo zimeshachimbwa basi palipo na uwezekano wa kurejesha yale matuta ya mchanga yalioko nje yarudishwe, halafu kupandwe miti.

Mhe. Naibu Spika, katika kuhifadhi mazingira labda ningemuuliza Mhe. Waziri, kuna NGO's ngapi hapa Zanzibar zinazoshughulikia mazingira ambazo yeye anashirikiana nazo na kuzipa uwezo wa kuhamasisha katika nchi yetu ya Unguja na Pemba.

Halafu ningemuuliza tena swali jengine. Je, ana mashirikiano gani au amejipanga vipi kushirikiana na Waziri wa elimu, kutokana na umuhimu wa mazingira kuliingiza somo la mazingira katika mitaala ya skuli. Vyenginevyo kwa kweli somo hili kuwaachia watu wachache tu, basi tunaweza tukafika pahala ambapo ni pabaya.

Mhe. Naibu Spika, baada ya kuzungumzia suala la mazingira. Vile vile niendelee kuzungumzia hilo hilo suala la mazingira, lakini katika nyanja nyengine. Wenzangu wamesema hapa kwamba baadhi ya shehia mbali mbali kuna vikundi vya polisi jamii, ambapo vikundi hivi vinashughulikia masuala ya kuhifadhi mazingira na mengineyo. Mhe. Naibu Spika, mimi namuambia Mhe. Waziri kwamba katika Jimbo langu la Chambani, Shehia ya Chambani, kuna kikosi cha askari jamii ambacho kiko makini sana. Hivi sasa wamesimamia masuala ya ukataji wa miti ovyo katika maeneo. Pia wamesimamia kuzuia ukataji wa mikoko katika maeneo ya bahari, *Alhamdulillah* hali hii ni nzuri.

Je, Mhe. Waziri atashirikiana nao vipi polisi jamii wa Shehia ya Chambani kuwapa uwezo wa kuweza kudhibiti mazingira zaidi ya hivi wanavyodhibiti hivi sasa. Baada ya hayo niingie kidogo Mhe. Naibu Spika, kuhusu suala la ukimwi.

Mhe. Naibu Spika, kwa kweli ukimwi ni janga la taifa. Kama hatukuwa makini basi ukimwi utatumaliza. Kwa hivyo, Mhe. Waziri mimi naomba kwamba suala hili la ukimwi tusilichukulie tu katika karatasi au katika vitabu ikawa ndio basi. Suala hili linahitaji kuwekewa mikakati ya makusudi. Mimi nimeshtuka sana katika ukurasa huu wa 98, kwenye kiambatisho nambari 14. Mhe. Naibu Spika, kinachonisikitisha zaidi hapa ni kwamba tunakinga ukimwi, lakini mimi nahisi kwamba kinga yetu hii inaweza ikawa inawapa hawa tunaowafikia kuwapa taaluma nguvu zaidi ya kutenda matendo ambayo yanasambaza ukimwi.

Mhe. Naibu Spika, hapa katika kiambatisho nambari 14 kinasema, kwamba 'idadi ya makundi maalum waliofikiwa na waelimishaji rika Unguja na Pemba, kwa Wilaya ya Mjini huduma zilizotolewa ni kupatiwa elimu ya ukimwi, kupatiwa ushauri nasaha, usambazwaji wa condom, kupatiwa huduma ya upimaji. Lakini hawa waliotembelewa ni wanaume wanaofanya mapenzi na wanaume wenzao kwa Wilaya ya Mjini ni watu 40, halafu wanawake wanaojiuza 63.

Mhe. Naibu Spika, mimi nasema kwamba *Inna Lillah Wainna Ilaihi Rajiun*, kwa nini nasema hivi kwa sababu huu ni msiba. Kwa kweli hawa wanaume wanaofanya mapenzi wao kwa wao, jamani sisi tuliomo humu kwa asilimia 99 na nukta tukumbuke Kaumu Luti ilifanywa nini. Kwa hivyo, Mhe. Spika, hili si jambo la mchezo wala si jambo la kuliangalia ama kulisikiliza katika masikio tu, bali hili liingie kwenye nyoyo zetu.

Pamoja na ushauri nasaha waliopewa hawa na kupewa kondom, mimi nasema kwamba mwanadamu ana baadhi ya viungo vikihamaki kiungo havihitaji chochote ila vipigane tu. Sasa kondom kuwapa vijana ni kuwaongeza mori katika viungo vyao vyenye hasira. Kwa hivyo, vipi tufanye ili kulitatua tatizo hili na wala si kuwagawia watu kondom tu ikawa hili ndio suluhisho la kuondoa tatizo hili. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, namuomba Mhe. Waziri atafute mbinu mbadala ambayo itaweza kuzuia visiwa vyetu na maangamizi ya aina yoyote ambayo yanaweza kutokea kwa masuala haya.

Nikiendelea na mchango wangu, sasa nizungumzie kuhusu safari za nje ambazo alikwenda Mhe. Makamo wa Kwanza wa Rais. Kwa mfano, tumeambiwa hapa katika mwaka uliopita, bajeti iliyopita kwamba Mhe. Makamo wa Kwanza wa Rais amekwenda safari ikiwemo India, kwa sababu ndani ya Baraza kuna Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa.

Mhe. Naibu Spika, naomba nimuulize Mhe. Waziri, je katika ziara hii kuna mjumbe yeyote wa kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa ambaye alikwenda katika ziara hiyo, zaidi ya hayo niseme kwamba ziara za Viongozi Wakuu ndani na nje ya nchi ni vyema kuwachukua baadhi ya wajumbe wa kamati inayosimamia viongozi wakuu, ili wajumbe wa kamati hii kupata uzoefu na kusoma zaidi katika mambo yalivyo kwa wenzetu, ili na wao wakifika hapa yale yaliyo mema wayatekeleze na yaliyo maovu watukanye tusiendelee nayo.

Mhe. Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi hii na mimi niseme kwamba nitaiunga mkono hoja hii baada ya maelezo ya Mhe. Waziri atakaponipa ufafanuzi wa yale ambayo nilimuuliza. Ahsante sana Mhe. Naibu Spika. *(Makofi)*

**Mhe. Naibu Spika:** Mhe. Mjumbe, ahsante sana na sasa nampa nafasi Mhe. Asha Bakari Makame na amalizie Mhe. Mohammed Haji Khalid.

**Mhe. Asha Bakari Makame:** Mhe. Naibu Spika, ahsante sana kwanza nichukue nafasi hii ya kumshukuru Mwenyezi Mungu ambaye ametuwezesha katika hali ya afya njema. Vile vile nichukue fursa hii kukushukuru wewe Mhe. Naibu Spika kwa kunipatia nafasi na mimi japo machache nichangie.

Kwanza nichukue nafasi hii kuipongeza hotuba ya Makamo wa Kwanza wa Rais, ambayo kwa kweli kwa kipindi hiki cha mwaka huu ni hotuba mwanana imeeleza, kwa sababu kipindi kilichopita cha mwaka uliopita wizara nyingi zilikuwa hazijui cha kufanya kutokana na mambo ya Bango Kitita.

Vile vile nichukue nafasi hii kumpongeza sana Mhe. Waziri pamoja na watendaji wake wote, ambao wamemsaidia kwa namna moja au nyengine.

Mhe. Naibu Spika, nitakuja moja kwa moja kwenye mazingira. Kwa kweli tulitoa mawazo hapa na tukasema kwamba Kisiwa Panza karibu kitaghariki, lakini mimi nasema hivi visiwa vyote vikubwa, Kisiwa cha Pemba na Kisiwa cha Unguja tukifanya mchezo vitakwenda na maji, kwa sababu visiwa hivi vinapungua kwa kasi kubwa sana hivi sasa. *(Makofi)*

Kwa hivyo naiomba sana wizara husika kupitia kwako Mhe. Naibu Spika, ikae na kufanya tathmini na ipitie na izunguke haidhuru iingie hasara kubwa sana, lakini izunguke katika visiwa vyetu vidogo vidogo pamoja na hivi visiwa hivi vya Unguja na Pemba na kuangalia taathira gani visiwa hivi vinaanza kukumbwa na *erosion* kwa hali kubwa sana.

Mhe. Naibu Spika, nitatoa mfano kuhusu Mkoa wangu wa Kaskazini Pemba katika Wilaya ya Wete sehemu ya Mtambwe Kusini, Kaskazini, Gawani, Makomeni, Kisiwani Mtambwe pamoja na Mtambwe Mkuu vimeathirika vibaya sana, kwa sababu katika sehemu hizi ambazo nimezitaja Mhe. Naibu Spika, kulikuwa na watu maalum ambao wanalima, na leo hawathubutu tena kulima kutokana na bahari ilivyokula vibaya sana. *(Makofi)*

Lakini hata Wilaya ya Micheweni kwa upande wa Msuka Mashariki, Magharibi, Tumbe, Sizini, Mapape na Sichoki vyote kwa kweli wananchi wetu hivi sasa wanapata shida kwa ukulima wa mpunga na muhogo, sehemu hizi zote zimeliwa Mhe. Naibu Spika. *(Makofi)*

Kutokana na hali hiyo, naiomba sana Idara ya Mazingira pamoja na kwamba imetenga fedha kwa ajili ya kusomesha watu pamoja na kutoa mafunzo. Lakini naiomba sana Wizara hii ambayo ni nyeti Mhe. Naibu Spika, hivyo naiomba Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais ihakikishe kwamba visiwa hivi vinamekuliwa na bahari, kwa hivyo mutembelee na mufanye tathmini na kuona ni sehemu zipi ambazo zimeathirika. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, nikiendelea na masuala ya mazingira, wakati mtu anapofanya vizuri basi mpongeze. Kwa kweli tulilaani sana hapa Hoteli ya *Zanzibar Ocean View* jinsi ilivyojenga kwenye bahari. Mhe. Naibu Spika, nichukue

nafasi nimpongeze Mzalendo kwa kweli amewajibika kwa upande mmoja au mwengine lazima alipoona kwamba amekosolewa basi na yeye amejirekebisha. *(Makofi)*

Kwa hivyo, nichukue fursa hii Mhe. Naibu Spika kumpongeza sana ndugu Makungu kwa jinsi alivyotii, kwa sababu yeye ni Mzalendo ametii amri ambayo imetolewa na Wajumbe wako wa Baraza hili tukufu. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, niende mbio kwa sababu wenzangu tayari wameshachangia na wakati haupo, nikiendelea na masuala ya mazingira. Kwa kweli hii tabia nchi nayo inatumalizia nayo tuiangalie pamoja na haya mazingira na tayari nimeshatoa mifano.

Kwa hivyo, naiomba wizara hivi sasa ifunge mkaja na kuhakikisha kwamba kweli visiwa vyetu havivamiwi na bahari kwa sababu bahari si ya kuchezea, isipokuwa wahakikishe kuwa pamoja na kuomba misaada kutoka nje, kwa sababu watu wanafanya mambo yao huko na mazingira yanatufika sisi huku.

Mhe. Naibu Spika, naiomba Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais ishirikiane na mashirika ya nje kuhakikisha hii tabia nchi wanasaidiana.

Nikiondoka hapo sasa niende kwenye Idara ya Watu Wenye Ulemavu. Mhe. Naibu Spika, Idara hii nimesikitishwa kidogo pamoja na kwamba wamefanya tathmini na kujua. Lakini naiomba Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais, hawa wenzetu watu wenye ulemavu ni sawa na watu sisi ambao hatuna ulemavu, na siku zote tunasema hujamaliza kuumbwa mpaka siku yako ya kufa. Kwa mfano, wengine ulemavu wamezaliwa nao, wengine wa kupata ajali.

Kwa hivyo, ninaiomba Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais itoe kipaumbele cha hali ya juu kuhusu watu wenye ulemavu. Mhe. Naibu Spika, nimesoma kwenye *statistics* zao ni kwamba wameainisha ni walemavu wangapi, mkoa huu wako wangapi na wala mimi sijatosheka Mhe. Naibu Spika. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, naiomba Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais, ituainishie walemavu taahira, vipofu, mabubu, walemavu wa viungo kujua idadi yao, ili kuona namna gani ya kuweza kuwasaidia watu kama hawa, kwa sababu tunao watoto wengi ambao ni taahira. Kwa kweli ni karatasi kidogo sana ambazo ndizo lilizozungumzia kuhusu watu wenye ulemavu. *(Makofi)*

Vile vile tuhakikishe kwamba hawa nao wanayo haki kama tuliyonayo sisi ambao Mwenyezi Mungu hajatupa ulemavu na Mwenyezi Mungu atunusuru, tuwatafutie ajira, kwa sababu wamo walemavu ambao wamesoma. Kwa mfano, wakati niliposoma mimi kuna watu wenye *PhD*, wengine *Diploma*, kwa hivyo tuwatafutie ajira na hawa ndio wa kusaidia hasa. Kwa hiyo, naiomba sana Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais kupitia kwako Mhe. Naibu Spika ifanye hivyo. *(Makofi)*

Nikiendelea na mchango wangu sasa naomba nizungumzie kuhusu suala la dawa za kulevya. Mhe. Naibu Spika, dawa za kulevya tusizifanyie mas-hara, mimi nasema tena pamoja kuwaapiza kwamba wale waliotuletea dawa za kulevya kwa kweli Mwenyezi Mungu atusaidie, lakini hizi ni dawa ambazo zimetupotoshea watoto au vijana wetu wengi wamepotea kwa dawa hizi za kulevya. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, naiomba Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais, kwamba vile vitengo ambavyo kabla ya ofisi hii kuundwa vimesaidiwa. Kwa mfano, Mama Shadya Karume amesaidia sana na ninampongeza sana kwa kweli amesaidia. Kwa hivyo, ni vyema kushirikiana na vitengo vile, ili kuhakikisha kwamba watu wetu wanakwenda kupima. *(Makofi)*

Lakini si hivyo tu, dawa za kulevya sambamba na suala la UKIMWI, kwa sababu dawa za kulevya ndio athari ya kupata UKIMWI. Mhe. Naibu Spika, hapa nataka nizungumze kidogo kwamba UKIMWI ni ugonjwa hatari na sote tunajua. Kwa hivyo, naiomba Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais, tuhakikishe kumbi zote za starehe zinawekwa matangazo ya UKIMWI.

Vile vile tuhakikishe wale wenzetu wanaotoka Kenya na Uganda, kwa sababu tunapokea wageni kutoka Kenya na Uganda, lakini wameshatuambikizia UKIMWI mwingi sana hapa Zanzibar. *(Makofi)*

Kutokana na hali hiyo, ni vyema kuhakikisha kwamba watu kama wale bila ya kwa sababu wanafanyakazi mahotelini tena wapishi wakubwa sana, tuhakikishe tunawapima kwanza ndipo wapatiwe kazi za upishi katika mahoteli, kama si hivyo watatumalizia Mhe. Naibu Spika na sisi *population* yetu ni ndogo. Kwa maana hiyo, watatumalizia kwa sababu na sisi tuchukue mambo kama wenzetu na wagonjwa wapo. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, nakuomba kidogo tu si muda mrefu nitamaliza.

Kwa hivyo, na sisi tuweke vitu vya kupima Mhe. Naibu Spika, nilikuwa na mengi lakini kwa kuwa umeniridhia, basi naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja, pia naomba na wenzangu tuipigie kura ya ndio. Ahsante sana. *(Makofi)*

**Mhe. Naibu Spika:** Mhe. Mjumbe, ahsante na mchangiaji wa mwisho Mhe. Mohammed Haji Khalid naomba na wewe ujali muda.

**Mhe. Mohammed Haji Khalid:** Mhe. Naibu Spika, ahsante sana na mimi kupata nafasi ndogo jioni hii.

**Mhe. Naibu Spika:** Waheshimiwa Wajumbe, tumsikilize Mhe. Mjumbe ambaye anayechangia, mazungumzo yamekuwa mengi na muda si mrefu tulikuwa tumepumzika.

**Mhe. Mohammed Haji Khalid:** Mhe. Naibu Spika, mawazo yangu juu ya kitabu kilichopo mbele yetu, ambacho kimeletwa kwa ajili ya kukiombea fedha kwa matumizi ya mwaka 2012/2013.

Kwanza nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa jioni hii ya leo kusimama hapa kwa ajili ya kutoa mawazo yangu. Vile vile nikushukuru wewe kwa kunipa nafasi hii ya mwisho kwa leo kuwa mchangiaji pengine kwa upande wa *back benchers*.

Kadhalika nimpongeze Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais, kwa uwasilishaji wake mzuri wa hotuba hii, ambayo imejaa ufasaha, pia niwashukuru watendaji wake wote akiwemo Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu, Wakurugenzi, Ofisa Mdhamini pamoja na wafanyakazi wote wa ofisi hii, nawaambia ahsanteni sana kwa kazi nzuri ambayo mumetuletea mbele yetu hapa. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, ofisi hii imekusanya taasisi nyingi ambazo hazina uwezo (*disabilities*) wakiwemo walemavu, watu walioathirika kwa UKIMWI, dawa za kulevya. Kwa hivyo, ofisi hii inahusika na mambo magumu mno. Pamoja na pongezi nilizowapa pia niwape na pole juu ya kazi ngumu waliyokabidhiwa na taifa. Lakini wafunge mkaja kuweza kuitekeleza, ili yaliyokusudiwa yaweze kufikiwa. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, nianze na mchango wangu kuhusiana na suala la mazingira kama walivyozungumza wachangiaji wengi waliopita. Zanzibar inakumbana na matatizo mengi, ambayo chanzo chake ama ni uchafuzi au uharibifu wa mazingira. Baadhi ya shughuli za maendeleo au zile za kupatia ajira ni vichochezi vya uchafuzi na uharibifu wa mazingira.

Kwa mfano, watu wanaoishi ukanda wa Mashariki, kama vile Mwambe, Micheweni, Vitongoji, watu hao shughuli zao kubwa kipindi hiki ama ni uchongaji wa matofali, uchimbaji wa mawe, kifusi na kadhalika. Kwa kweli haya yote kwa kiasi fulani yanaharibu mazingira, lakini imekuwa ni moja katika njia ya kujipatia riziki zao. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, kwenye hotuba ya Mhe. Waziri wa Nchi (OR), Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo ile ya Bajeti ya Serikali, mambo haya yalitajwa kuwa ni sehemu ambayo inaongeza mapato serikalini pamoja na kuwa yanachafua au yanaharibu mazingira. Kwa hivyo, maendeleo yetu au shughuli zetu pia zinasababisha matatizo yetu.

Jambo la kufanya ni lazima ofisi hii iandae sheria maalum pamoja na kanuni ambazo zitaweza kutumika katika kuhifadhi mazingira yetu, vyenginevyo baada ya muda mchache ujao Zanzibar itakuwa nusu jangwa, kwa sababu miti inapotea, ardhi tunaichimba kwa shughuli zetu nab ado hatujakuwa na kitu mbadala kuacha kutumia mawe na mchanga katika ujenzi.

Kwa hivyo, hata tukifanya nini lazima mambo haya yataendelea kutumika. Kwa maana hiyo, kuwe na sheria ambayo itakuwa makini na kuruhusu shughuli kufanyika na wala zisiharibu na wala zisichafue mazingira.

Mhe. Naibu Spika, mbali ya shughuli ambazo tunafanya kama ni kazi zetu za kawaida, uingizaji wa baadhi ya vitu katika nchi, ambavyo vinapo-*expire* au kukosa kutumika vikawekwa pia navyo vinatuchafulia au kutuharibia mazingira yetu.

Hivi karibuni tulipata semina iliyotuonesha kuwa *televisions* nyingi ambazo tunazozitumia hivi sasa tarehe 31 Disemba, 2012 nyingi zitakuwa hazitumiki tena. Kwa hivyo, kuna uwezekano hivi sasa mtu kuweza kumpa mwenzake *television* kama ni zawadi kumbe vile anajipunguzia mzigo katika nyumba yake, kwa sababu anajua kwamba *television* hii itakuwa haina kazi tena. Lakini hata ukimpa mtu bado itabakia ipo kwenye kisiwa, na itakuwa ni mzigo ambao haufukiliki wala hauyayuki.

Kutokana na hali hiyo, sijui ofisi hii itakuwa na mpango gani madhubuti wa kuweza kuvidhibiti vifaa vya aina hii, ambapo itafika wakati viwe havitumiki na tuweze kuviangamiza bila ya kuleta athari katika maisha yetu, kwa sababu baadhi ya vyengine vina *mercury* ambayo ni hatari kwa kiasi fulani.

Mhe. Naibu Spika, baadhi ya hoteli ambazo ni sehemu ya uchumi wetu zinaingia katika kundi hili la uharibifu wa mazingira. Kwa hivyo, Idara hii ya Mazingira lazima ipewe nafasi yake kabla hoteli haijajengwa, basi watu wa mazingira watoe *concern* zao pamoja na kuelekeza vipi iweze kujengwa bila ya kuathiri mazingira yetu.

Vile vile kuna msumeno wa moto, ambao unafanya kazi nzuri ya kuangamiza miti. Mhe. Naibu Spika, nikisema nzuri sio kama ninaipongeza, isipokuwa nzuri kwa sababu ya kipindi kifupi inaweza kuangusha miti kadhaa. Kwa kweli sijui wanaofanya hivi wanafanya katika ile njia ambayo tumewataka watu wajiajiri kwa ajili ya kujitafutia maisha. Kwa hivyo, sijui ofisi hii itawaelekeza vipi watu hawa au kuwatafutia njia mbadala ya maisha badala ya kuangamiza miti.

Mhe. Naibu Spika, katika kuhifadhi mazingira hapa karibuni sisi hapa kwenye Baraza tulipewa mashimo na miche, ili kila mmoja atie mche wake katika shimo alilopewa, kwa ajili ya kuweka ofisi katika hali nzuri ya mazingira. Sasa wito huu aliotuletea Mhe. Spika usimalizie hapa ofisini tu. *(Makofi)*

Kwa hivyo, Waheshimiwa Wajumbe ninawaomba kupitia kwako Mhe. Naibu Spika, kwamba tupande miche katika majumba na mashamba yetu, ili kurudisha miti ambayo inapotea kwa wingi.

Nikiendelea na mchango wangu sasa nizungumzie kuhusu dawa za kulevya, ambalo hili ni janga. Mhe. Naibu Spika, sisi wajumbe wa Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa, hawa wamekuwa ni marafiki zetu, kwa sababu tunatembelea mara kwa mara kwenye *Sober Houses* katika kazi zetu na wanatueleza matatizo yao. Kwa mfano, mimi nimetumia kwa muda wa miaka 15 ndio bwana, lakini sasa nimeacha. *(Makofi)*

Sasa namuomba Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Naibu Spika, kwamba hizi *Sober Houses* waziwezeshe na tuwaandalie vijana hawa wakitoka pale, basi wawe na jambo la kujishughulisha ili wasirudie tena. Kwa kweli akiondoka pale kama hakupata shughuli ya kufanya atarudi katika shughuli ile, kwa ajili ya kuwa tajiri mkubwa, meli zote kubwa ni zake, ndege angani ni ya kwake pamoja na kila kitu ni cha kwake, kumbe vile hana chake.

Kwa hivyo, hili ni janga la nchi na iko haja ya makusudi ya kuwashughulikia vijana hawa. Mhe. Naibu Spika, ulevi ni mama wa maasi, ukishalewa basi jengine lolote unaweza kulifanya. Sasa kwa wale ambao waliwahi kuingia katika janga hili na wenyewe wamejitolea kujikusanya katika *Sober Houses*, basi ningeiomba ofisi hii kwamba ni ulezi huo, waukubali na walee, pengine tunaweza kupata nusu yao wakaokoka.

**Mhe. Naibu Spika:** Mhe. Mjumbe, bado dakika tano.

**Mhe. Mohammed Haji Khalid:** Mhe. Naibu Spika, dakika tano ulizoniambia naomba nizungumzie kidogo na kama ni kuuliza swali tu. Utafiti gani ofisi iliotumia kuweza kuwabaini hawa watu ambao wanaume kwa wanaume wanaingilia wenyewe, hivi ni utafiti gani umefanyika? Kwa sababu hili ni jambo ambalo ni siri ya ndani, sasa hawa tuliwabaini vipi kama kuna watu wanaofikia kiasi hiki wanazo shughuli hizi? *(Makofi)*

Vile vile kwa upande wa wanawake ambao wanajiuza. Lakini kwa wanawake nasikia na wala sina hakika kwamba kuna kundi moja la wanawake na wao wanafanya kama wanaume wanaoingiliana wenyewe, sasa sijui lipo kweli au ni maneno tu ya mitaani? *(Makofi)*

Mhe. Waziri ofisi yako ina mambo mengi tena ni magumu, na yanahitaji kufanyiwa kazi. Mhe. Naibu Spika, kuna Mhe. Mjumbe mmoja alisema hapa ambaye ni Sheikh, kwamba haya yote yanayotokezea kuwa leo visiwa vyetu bahari inatusogelea pengine ni baadhi ya mambo tunayoyafanya ambayo Mwenyezi Mungu hayaridhii. Kwa hivyo, kama hatukuchukua tahadhari na mapema, wataalamu wameshaona kama Kisiwa Panza kitaanza, lakini hatujui hatimae itafuatia wapi.

Mhe. Naibu Spika, niseme kuwa ofisi hii imepewa majukumu mazito, isipokuwa nawaombea kwamba wajitahidi kufanya kazi, kwa ajili ya kuliokoa taifa katika majanga yaliyotukabili. Ahsante sana. *(Makofi)*

**Mhe. Naibu Spika:** Mhe. Mjumbe, ahsante sana na huyo ndiye alikuwa mchangiaji wa mwisho. Kwa hivyo, hivi sasa ni wakati wa Mhe. Waziri kuja kufanya majumuisho, hivyo ni vyema tusitoke nje ikawa mtu hoja yake imejibiwa yeye mwenyewe hayupo. Hata hivyo, mahudhurio yetu hayajawa mazuri, na hoja hii tunataka tuimalize hivi jioni. Waheshimiwa Wajumbe, nawaomba tutulie na tumsikilize Mhe. Waziri, ili tumalize kazi yetu vizuri.

**Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais:** Mhe. Naibu Spika, awali ya yote napenda nianze kwa kumshukuru Allah kwa kutujaalia jioni hii ya leo kuwa wazima wa afya na kuweza kuendelea na shughuli zetu. Mhe. Naibu Spika, naomba nichukue fursa hii kuwashukuru Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako tukufu, kwa michango yao pamoja na ushauri waliotoa katika kuchangia hotuba ya bajeti ya Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais. Ninaamini michango yote hiyo imelenga katika kuleta mafanikio ya shughuli zinazotekelezwa na Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais, ambazo ni shughuli mtambuka na zinamgusa kila mmoja wetu.

Mhe. Naibu Spika, kwa kweli michango iliyotolewa imenipa faraja sana, hasa pale nilipoona baadhi ya Waheshimiwa Wajumbe wakitoa michango inayotoa taaluma ndani yake. Nimepata faraja kuona ile taaluma tuliyoitoa kupitia njia za semina imefahamika vya kutosha. Aidha napenda kuwahakikishia Waheshimiwa Wawakilishi kuwa michango yao yote tunaithamini, tunaipokea na tutaifanyia kazi.

Mhe. Naibu Spika, niwatambue kwa kuwataja kwa majina wale wote ambao walipata nafasi ya kuchangia kwa kuzungumza humu ndani ya Baraza lako tukufu, nao ni kama ifuatavyo:-

| | |
|---|---|
| Mhe. Mwajuma Faki Mdachi | Makamo Mwenyekiti kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Kusimamia Viongozi wakuu wa Serikali, ambaye pia aliisoma taarifa ya kamati kwa niaba ya Kamati yake. |
| Mhe. Makame Mshimba Mbarouk | Mwakilishi wa Jimbo la Kitope. |
| Mhe. Abdalla Juma Abdalla | Mwakilishi wa Jimbo la Chonga |
| Mhe. Suleiman Hemed Khamis | Mwakilishi wa Jimbo la Konde |
| Mhe. Bikame Khamis Hamad | Mwakilishi wa Viti maalum |
| Mhe. Amina Iddi Mabrouk | Mwakilishi wa Viti maalum |
| Mhe. Farida Amour Mohammed | Mwakilishi wa Viti maalum |
| Mhe. Saleh Nassor Juma | Mwakilishi wa Jimbo la Wawi |
| Mhe. Ismail Jussa Ladhu | Mwakilishi wa Jimbo la Mji mkongwe |
| Mhe. Ashura Shariff Ali | Mwakilishi wa Viti maalum |
| Mhe. Jaku Hashim Ayoub | Mwakilishi wa Jimbo la Muyuni |
| Mhe. Fatma Mbarouk Said | Mwakilishi wa Jimbo la Amani |
| Mhe. Salim Abdalla Hamad | Mwakilishi wa Jimbo la Mtambwe |
| Mhe. Mtumwa Kheri Mbarak | Mwakilishi wa Viti maalum |
| Mhe. Hamza Hassan Juma | Mwakilishi wa Kwamtipura |
| Mhe. Abdalla Mohammed Ali | Mwakilishi wa Jimbo la Mkoani |
| Mhe. Mohammed Mbwana Hamad | Mwakilishi wa Jimbo la Chambani |
| Mhe. Mohammed Haji Khalid | Mwakillishi wa Jimbo la Mtambile |
| Mhe. Asha Bakari Makame | Viti Maalum. |

Mhe. Naibu Spika, waliochangia kwa njia ya maandishi ambayo nayo nimeipata michango yao ni Mhe. Marina Joel Thomas Mwakilishi uteuzi wa Rais. Mhe. Kazija Khamis Kona Mwakilishi wa viti maalum, Mhe. Wanu Khamis Ameir Mwakilishi wa viti maalum, Mhe. Salma Mohammed Ali wa viti maalum na Mhe. Panya Ali Abdalla viti maalum.

Mhe. Naibu Spika, sasa naomba nianze kutoa ufafanuzi pamoja na majibu ya maswali yaliyoulizwa na Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako tukufu.

Mhe. Naibu Spika, michango na maswali mbali mbali ya Waheshimiwa wa Baraza lako tukufu nimeigawa katika Idara tofauti ambazo zimo ndani ya Ofisi yangu, na nitapenda kujibu kufuatana na hoja zenyewe kama zilivyojitokeza katika Idara mbali mbali.

Mhe. Naibu Spika, naomba nianze na Ofisi ya Faragha. Waheshimiwa ambao walichangia na pia kuweza kuuliza maswali mbali mbali kutoka Idara hii ni Mwenyekiti wa Kamati Mhe. Abdalla Juma Abdalla, Mhe. Farida, Mhe. Ismail Jussa Ladhu, Mhe. Jaku Hashim Ayoub, Mhe. Ashura na Mhe. Saleh Nassor Juma.

Mhe. Naibu Spika, katika Idara hii mambo muhimu yaliyojitokeza kutokana na michango ya Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza hili ni pamoja na kwanza ufuatiliaji wa tija inayotokana na safari ya Mhe. Makamo wa Kwanza wa Rais nchini India. Katika hotuba yangu nimeeleza kuwa Mhe. Makamo wa Kwanza wa Rais kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2011/2012 alifanya ziara moja tu ya kikazi nchini India, na katika ziara hiyo Zanzibar inatarajiwa kunufaika katika nyanja mbali mbali zikiwemo teknolojia ya habari na mawasiliano, elimu, kilimo, biashara na uwekezaji.

Mhe. Naibu Spika, kwanza napenda kulijulisha Baraza hili kuwa ziara za viongozi wakuu wa serikali ni muhimu sana kwa maendeleo ya nchi yoyote ile. Katika ziara hiyo ndio nchi huweza kujenga na kudumisha mahusiano na nchi nyengine, kuitangaza nchi yetu kwa wawekezaji pamoja na kupata misaada katika sekta mbali mbali.

Aidha ni vyema tukafahamu kwamba ziara hizo zinapofanywa ni sawa na kazi ya ukulima, kwamba ukilima leo hutegemei kuvuna leo, mavuno yanategemea aina ya kilimo, mbegu iliyopandwa na pia wakati mwingine hali ya hewa. Hivyo viongozi wetu wanapokwenda katika ziara za nje wanakuwa kama wakulima wanaohangaika na jua na mvua kwa nia njema kabisa ya kututafutia lile lenye kheri na maslahi kwa nchi yetu.

Mhe. Naibu Spika, aidha napenda kuwatoa wasiwasi Wajumbe wa Baraza lako tukufu kuwa serikali inafatilia kwa karibu matunda ya ziara zote za viongozi wakuu wa serikali. Serikali tayari imeunda kamati ndogo ya Baraza la Mapinduzi ambayo ina jukumu la kufatilia mafanikio ya ziara hizi. Mimi mwenyewe nikiwa Mwenyekiti wa Kamati ya kufuatilia ziara za Mhe. Makamo wa Kwanza wa Rais.

Hadi wakati huu tayari Serikali ya mapinduzi Zanzibar imeshatiliana saini mkataba wa mashirikiano yaani MOU kati ya Serikali ya Zanzibar na Serikali ya Jimbo la Hyderabad katika eneo zima la teknolojia ya habari na mawasiliano. Na kwa upande wa Serikali ya Mapinduzi mratibu ameshachaguliwa na katika maeneo mengine ufatiliaji unaendelea, na kila eneo basi wizara ambayo inahusika na sekta yake imepewa mamlaka kamili ya kufuatilia na baadae kutoa taarifa serikalini.

Swali la pili lililoulizwa katika Idara hii ni tatizo la nyumba kwa Mhe. Makamo wa Kwanza wa Rais Pemba na Dar es Salaam. Mhe. Naibu Spika, ni ukweli kwamba hadi sasa Mhe. Makamo wa Kwanza wa Rais hana nyumba maalum Pemba na Dar es Salaam. Hali inayoleta usumbufu mkubwa, hali hii inatokana na kutowepo nyumba ya serikali stahiki kwa hadhi ya Mhe. Makamo wa Kwanza wa Rais. Hata hivyo napenda kuwahakikishia Wajumbe wa Baraza lako kwa mwa mwaka huu 2012/2013, Ofisi yetu imejipanga kukodi nyumba kwa Mhe. Makamo wa Kwanza wa Rais kwa upande wa Pemba.

Aidha kwa upande wa Dar es Salaam hali imekuwa ngumu kupata nyumba ya serikali stahiki kwa hadhi inayomfaa Mhe. Makamo wa Kwanza wa Rais. Jitihada mbali mbali zimechukuliwa lakini imeshindikana kupatikana hadi sasa. Ofisi yangu ilifikiria wazo la kukodi nyumba kwa ajili ya Mhe. Makamo wa Kwanza wa Rais huko Dar es Salaam, lakini kutokana na gharama zake kuwa kubwa ndio maana hadi hii leo Mhe. Makamo wa Kwanza anapokwenda Dar

es Salaam hulazimika kukodiwa hoteli ambayo hukaa yeye pamoja na wasaidizi wake wa lazima, ambao hata kama angelikuwa na nyumba basi angelazimika kukaa nao.

Mhe. Naibu Spika, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ilitenga nyumba ya serikali iliyopo Maisara kuwa ndio makaazi ya muda ya Mhe. Makamo wa Kwanza wa Rais mara baada ya uteuzi wake, na baadae iweze kutafutwa nyumba nyengine ambayo inalingana na hali yake. Hii ni kutokana na uchakavu wa nyumba yenyewe ya Maisara pamoja na mambo mengine mengi ambayo yalikuwa yakisababisha usumbufu mkubwa katika nyumba hiyo kuwa ni makazi ya kudumu ya Mhe. Makamo wa Kwanza wa Rais.

Mhe. Spika, ofisi yetu kwa kushirikiana na Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati tulifanya kila juhudi kutafuta nyumba ya serikali ambayo ingeweza kutumika kuwa makaazi ya Mhe. Makamo wa Kwanza wa Rais. Napenda kulijulisha Baraza lako hili kuwa katika jitihada zote hizo tuliweza kupata nyumba moja tu iliyopo eneo la migombani ambayo ingebidi kwanza ifanyiwe matengenezo kwa gharama isiyopungua milioni 400, ndipo serikali sasa ilipotafuta njia mbadala ya kukodi nyumba stahiki kwa hadhi ya Mhe. Makamo wa Kwanza wa Rais kulingana na uwezo wa Serikali. Katika zoezi hili la kutafuta nyumba ya kukodi kwa awamu ya mwanzo tulipata nyumba 4 ambazo zote hakuna inayopungua dola za kimarekani 4000 kwa mwezi.

Kutokana na ughali huu na kwa busara za serikali tukazikataa nyumba hizi. Katika awamu ya pili ndipo ilipopatikana nyumba ambayo hivi sasa ndiyo anayotumia Mhe. Makamo wa Kwanza, nyumba hii inalipiwa dola za kimarekani elfu mbili na wala si milioni kumi kama inavyosemwa mitaani. Nyumba hii imekubaliwa na Ofisi yangu baada ya kuridhiwa kuwa ina vigezo vyote vya kukaa kiongozi wa juu wa kitaifa pamoja na kumridhisha yeye mwenyewe na watu wanaohusika na usalama wa viongozi ambao wameipasisha nyumba hiyo. Makaazi haya mapya ya Mhe. Makamo wa Kwanza yapo Mbweni, Wilaya ya Magharibi Mkoa wa Mjini Magharibi.

Mhe. Spika, jambo jengine muhimu ambalo limechangiwa na Waheshimiwa wa Baraza lako ni kuhusu tatizo la wafanyakazi wa kumuhudumia Makamo wa Kwanza wa Rais Pemba. Ni ukweli kwamba hadi hivi sasa hakuna mfanyakazi yoyote aliyeajiriwa kwa madhumuni hayo. Hii ilitokana na upya wa ofisi yenyewe na pia kupatikana nyumba ambayo kwa kawaida wafanyakazi wa aina hiyo huwa ndio ofisi yao. Kwa hali hiyo ndiyo inayomfanya Afisa Mdhamini kusimamia huduma zote za Makamo wa Kwanza akiwa Pemba, ikiwa ni pamoja na huduma za chakula na wala sio kupika, isipokuwa tu kuangalia aina ya chakula chenyewe na shughuli zinavyokwenda.

Aidha huduma za Ofisi zinatolewa kwa sasa hivi na wahudumu kutoka Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais. Hata hivyo katika mwaka huu wa fedha wa 2012/2013 tunatarajia kuwaajiri wafanyakazi 3 ambao ni dereva, mpishi na mratibu wa shughuli za Mhe. Makamo wa Kwanza wa Rais huko Pemba.

Mhe. Naibu Spika, naomba sasa niingie katika michango ambayo imetolewa katika Idara ya Mipango, Sera na Utafiti. Katika Idara hii hoja kuu mbili ziliulizwa. Hoja ya ufafanuzi wa miradi miwili inayolenga katika kujenga uwezo ambayo imeulizwa na ndugu yangu Mhe. Ismail Jussa Ladhu. Mhe. Naibu Spika, napenda kumjibu Mhe. Mjumbe kama ifuatavyo:-

Kwa kutambua kwamba suala la kujenga uwezo ni pana sana. Ofisi ya Makamo wa kwanza wa Rais kwa makusudi iliwasilisha miradi 2 tofauti huko *UNDP* na Benki ya Dunia. Mradi wa kujenga uwezo uliowasilishwa *UNDP* umelenga katika kutekeleza mambo maalum yakiwemo kuandaa mpango mkakati wa Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais, mpango wa utafiti, mfumo wa ufuatiliaji na tathmini, na pia kutoa mafunzo ya ufuatiliaji na tathmini kwa watendaji wa Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais.

Mradi uliowasilishwa benki ya dunia umekusudia kuibua miradi mbali mbali mikubwa ambayo imetokana na mpango mkakati, pamoja na kusaidia utekelezaji wa mpango huo ambao unazigusa sekta zote zilizo chini ya Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais. Aidha suala la kuwajengea uwezo kwa kuwapa mafunzo watendaji pia nayo yamezingatiwa.

Hoja nyengine ambayo inahusu miradi imeulizwa na Mhe. Ismail Jussa Ladhu na Mhe. Saleh Nassor Juma. Mhe. Naibu Spika, napenda kujibu hoja hizo kama hivi ifuatavyo:

Hoja ya kwanza ni kuhusu uangamizaji wa kunguru. Mhe. Naibu Spika, napenda kuchukua fursa hii kumjibu Mhe. Mwakilishi wa Jimbo la Wawi Mhe. Saleh Nassor Juma suala la kuangamiza kunguru kwa njia zinazotumika. Mhe.

Saleh ametumia neno *Predator prey relationship* kwa maana ya mahusiano baina ya mwindaji na muindwaji. Hili ni moja ya neno muhimu la somo la uhai yaani biology kuonesha umuhimu wa kuwepo mwindaji na mwindwaji kwenye mzunguko wa maisha ya maeneo ya viumbe hai wanavyoishi, yaani ndani ya *eco system*. Unapomuondoa mwindaji ukabakisha muindwaji ni hatari, na unapomuondoa muindwaji na ukambakisha mwindaji hayo yanakuwa pia ni mashaka.

Mhe. Naibu Spika, kunguru ni aina ya viumbe wavamizi kitaalamu wanaitwa jina la *investive species* viumbe hao wanakuwa ni tishio kwa *bayoanuai* na *ikolojia* ya sehemu wanayoingia. Ni wazi na ninaamini sote tunafahamu athari mbali mbali zinazosababishwa na kunguru hapa ndani ya visiwa vyetu lakini hata duniani kwa ujumla. Kunguru wamekuwa ni tishio kwa ndege wa asili, kilimo na mifugo ya aina mbali mbali hapa nchini. Kuwepo kwao hapa Zanzibar kunaaminika kuwa wanaingia katika mzunguko wa maisha ikiwa hawana asili ya mahali walipokuwepo na kusababisha matatizo mbali mbali.

Mfano magugu mwitu katika ziwa Victoria. Hilo gugu mwitu ni *investive species*, ingawa hilo gugu linaweza kutumika kama chakula kwa wanyama lakini limeleta matatizo makubwa katika mzunguko wa maisha ya ziwa Victoria ikiwa ni sawa na kunguru, kwani kunguru anasababisha kupotea na kupungua kwa *bayoanuai* mbali mbali ikiwa wadudu na ndege, aidha kunguru huwasababishia madhara ng'ombe na kuwatia majeraha hata kusababisha upofu.

Mhe. Naibu Spika, naomba Mhe. Saleh Nassor Juma akubali kuwa si vizuri kuwaleta ndege ambao ame-*propose* au wanyama wanaoitwa koho sijui kwa kizungu wanaitwa nini, kwa sababu ili waweze kuja kuwala kunguru Mheshimiwa kuna ukweli wa hadithi moja nchini *Seychelles*, ambapo wao walikuwa wanasumbuliwa na panya, panya ambao walikuwa wanataka wawaondoe katika kisiwa cha *Seychelles*. Baadhi ya watu waka-*suggest* walete wanyama wanaoitwa bundi, ili bundi wawale hao panya. Mhe. Naibu Spika, habari ya kuaminika inasema kwamba bundi wamezaana kwa wingi na panya wapo pale pale.

Kwa hivyo tunaogopa sana ku-*introduce species* hiyo mpya isije ikaleta madhara kwa viumbe wengine ambao wapo pia ndani ya *eco-system*. Naomba atukubalie kwamba njia tunayokwenda nayo ni sahihi kabisa kabisa.

Mhe. Naibu Spika, naomba sasa niingie katika Idara ya Mazingira. Kwenye Idara hii naomba nianze kwa kumshukuru sana kwanza Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dr. Ali Mohammed Shein kwa maamuzi yake ya kuiweka Idara ya Mazingira ndani ya Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais. Uamuzi huu umetoa nafasi kwa Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako tukufu kupata fursa inayostahiki ya kuchangia kwa kina juu ya masuala ya uhifadhi na utunzaji wa mazingira hapa nchini.

Mhe. Naibu Spika, kwa kuzingatia umuhimu wa mazingira na kuwa maisha yetu ya kila siku yanagusa mazingira, hotuba ya Idara ya Mazingira imepata bahati ya kuchangiwa na karibu ya Waheshimiwa wote waliopata fursa ya kuchangia bajeti yangu, wale ambao wamechangia kwa maandishi lakini pia waliozungumza katika Baraza lako tukufu.

Mhe. Naibu Spika, kwa ujumla Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais inapokea pongezi zote zilizotolewa na Waheshimiwa Wajumbe juu ya utekelezaji wa mafanikio ya Idara hii ikiwa ni pamoja na pongezi juu ya kusimamia vyema suala la marufuku ya mifuko ya plastiki. Mradi wa maji Nungwi na mradi wa maji machafu msingini Pemba, tunashukuru kwa pongezi hizo. Mhe. Naibu Spika, kwa ujumla michango ya Idara ya Mazingira imegawika katika makundi makubwa yafuatayo. Iligusa sera na sheria za mazingira, hoteli ya Palumbo ya Uroa, mifuko ya plastiki, jengo la Afisi ya Idara ya Mazingira Unguja, vitendea kazi ya Ofisi ya Idara ya Mazingira Pemba, uchimbaji wa mali asili zisizorejesheka, bidhaa chakavu za umeme na elektroniki, kunguru, mradi wa maji machafu, misumeno ya moto, ukataji wa miti na mikoko, mabadiliko ya tabia ya nchi, ziara za kimasomo Moshi na Arusha, elimu ya mazingira na mashirikiano na taasisi mbali mbali. Mhe. Naibu Spika, Kiwanda cha Makonyo pia kiliguswa, lakini pia mradi wa maji wa Nungwi.

Mhe. Naibu Spika, nikianza na sera na sheria ya mazingira. Zanzibar imebahatika kuwa na sera ya mazingira mwaka 1992 ambapo ndio inatoa muongozo wa kisera juu ya uhifadhi na usimamizi wa mazingira. Miaka 20 imepita sasa tokea kuzinduliwa kwa sera ya mazingira, hivyo ni wazi kuna mabadiliko ya sera, mazingira yanahitajika ili kuielekea Zanzibar kwenye maendeleo endelevu yanayozingatia matumizi bora na endelevu pia maliasili zilizopo. Hivi sasa mabadiliko hayo yameshafanyika na yanasubiri kujadiliwa katika vikao husika vya kisheria.

Aidha sheria ya mazingira ni ya mwaka 1966 hata hivyo sheria hiyo ina mapungufu vile vile ambayo yanazuia utekelezaji wake. Mhe. Naibu Spika, ni nia ya ofisi yangu kuifanyia marekebisho sheria ya mazingira ya mwaka 1966 mara baada ya kupitishwa sera mpya ya mazingira. Tukimaliza tu kuipitisha sera mpya tutaifanyia mabadiliko sheria ya mazingira, kwa sababu mambo haya mawili yanategemeana. Ni imani yangu kwamba Waheshimiwa Wajumbe watapata nafasi ya kuipitia na kuijadili sheria hiyo mpya wakati itakapofika, ili tuwe na sheria yenye kukidhi haja inayojitosheleza ya uhifadhi wa mazingira yetu.

Mhe. Naibu Spika, kuhusu suala la hoteli Palumbo ya Uroa, baada ya kubainika kwamba hoteli ya Palumbo imekiuka taratibu za kimazingira kwa kuchimba mchanga wa fukwe kwa kutumia kijiko, pia kukiuka kanuni za matumizi ya ardhi na vitega uchumi kwa kuongeza eneo na kujenga ukuta kwenye ufukwe kinyume na utaratibu. Idara ya Mazingira iliamrisha kusimamisha ujenzi huo kwa maana ya kutoa *stop order* kwa ajili ya kusimamisha shughuli zenyewe.

Hatua iliyofuata ni kulipeleka shauri hilo Polisi kwa ajili ya kufikishwa kwenye vyombo vya sheria. Kabla ya kesi hiyo kufunguliwa rasmi Mwakilishi wa hoteli hiyo alipata wito wa Polisi, na baada ya kufika alikubali kuwa ni kosa na aliomba suala hilo atalitekeleza bila ya amri ya mahkama. Idara ya Mazingira ilitoa masharti mawili. La kwanza kubomolewa kwa ukuta, na pili kufanya mkutano wa maelewano na jamii ya watu wa Uroa. Mkutano wa maelewano na watu wa Uroa ulifanyika kupitia Ofisi ya Mkuu wa Wilaya ya Kati kama tulivyokubaliana lakini wamiliki wa hoteli walishindwa kubomoa ukuta.

Mhe. Naibu Spika, Ofisi yetu inakubaliana na Kamati ya kudumu ya kusimamia ofisi za viongozi wakuu wa kitaifa kwamba muwekezaji wa hoteli hiyo abomoe ukuta huo. Ndio maana Ofisi yangu kupitia Idara ya Mazingira imepeleka shauri hilo kituo cha Polisi cha Chwaka na kufunguliwa kesi namba 345.

Mhe. Naibu Spika, kuhusu jengo la Ofisi ya Idara ya Mazingira Unguja, naomba nikubaliane na Kamati ya Kudumu ya Baraza la Wawakilishi ya Kusimamia vingozi wakuu wa kitaifa juu ya haja ya kujenga jengo la kisasa la Idara ya Mazingira Unguja. Ni kweli Ofisi iliyopo hivi sasa ni ndogo na haiko kwenye viwango vya hadhi ya Ofisi ya kusimamia mazingira. Ofisi yetu imeolina jambo hili na imeshaanza mchakato wa kutafuta mfadhili wa kujenga jengo jipya. Aidha Ofisi yetu imeshapeleka maombi kwa taasisi husika ya kupatiwa kiwanja kwa ajili ya kujenga jengo hilo.

Mhe. Naibu Spika, kuhusu suala la vitendea kazi, Idara ya Mazingira Pemba katika kipindi kilichopita cha 2011/2012 kimeweza kupata baadhi ya vitendea kazi ambavyo vitaongeza ufanisi katika utendaji wa kazi zake. Vifaa hivyo ni kama kompyuta, *GPS, Digital camera* na *moving camera.* Vitendea kazi hivi vitaongeza ufanisi kwa Idara kutekeleza majukumu yake. Ofisi yangu itaendelea vifaa kwenye Idara hii Pemba kadri hali itakavyoruhusu.

Mhe. Naibu Spika, kuhusu suala la uchimbaji wa maliasili zisizorejesheka. Mhe. Naibu Spika, mimi nakubaliana kabisa na Waheshimiwa kwamba bado kuna uharibifu unaoendelea katika maeneo mbali mbali ya visiwa vyetu yakiwemo maeneo ya fukwe. Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais kwa kulitambua hili inaendelea kushirikiana na taasisi husika pamoja na viongozi wa shehia na wananchi kwa jumla kupitia kamati za mazingira na Polisi jamii kwa kudhibiti suala hili. Aidha tunaendelea kutoa elimu kwa jamii ili kuweza kuelimisha haya.

Katika suala la ukamataji wa magari kutokana na makosa ya uchukuaji wa maliasili isiyorejesheka kama vile mchanga kutekelezwa kwa kutumia sheria ya mazingira ya mwaka 1966, ambapo Idara ya Mazingira imekuwa ikishiriki kutoa ufafanuzi wa sheria hiyo pale inapohitajika katika vituo vya Polisi. Hata hivyo kwa kuwa zoezi la utoaji vibali vya uchukuaji wa maliasili hizo sambamba na doria za ukamataji wa magari yanayokiuka sheria hufanywa na Wizara ya Kilimo na Maliasili kupitia Idara ya Misitu na Maliasili zisizorejesheka, kumbukumbu za ukamataji huo huwekwa katika Idara hiyo ya Misitu na Maliasili zisizorejesheka.

Hivi sasa kama nilivyoeleza katika hotuba yangu kuwa tayari Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais imeshawasilisha kwa Mwanasheria Mkuu kanuni ya kusimamia na kudhibiti uvunaji wa maliasili zisizorejesheka, ambayo tumepatiwa maoni juu ya kanuni hiyo na tunaendelea kuyafanyia kazi maoni hayo.

Kuhusu uchimbaji mchanga na mawe kuwa ni kitega uchumi cha nchi, ni kweli Mhe. Naibu Spika, sio kwamba serikali imejikita kutegemea uuzaji wa maliasili hizi na kupata kipato, isipokuwa kama Wajumbe wengine

walivyoona kuwa maliasili ni lazima zitumiwe na wananchi katika kujenga nyumba bora za kuishi pamoja na majengo muhimu. Hivyo katika uchukuaji wa maliasili hizi serikali pia huchukua ada kidogo kutoka kwa watumiaji. Kwa sasa naomba sana tuendelee kushirikiana katika kuwaelimisha wananchi wetu juu ya athari zitakazotufika endapo tutafanya mzaha katika kulinda mazingira ya visiwa vyetu.

Kuhusu usafi wa mazingira. Mhe. Naibu Spika, ziara ya mji wa Moshi imetokana na kwamba kiasi ya mara tatu mji huo umekuwa ukiongoza kwa usafi na kupewa zawadi. Ziara ya washiriki katika mji huo ni kujifunza juu ya mafanikio yaliyofikiwa. Kutokana na ziara hiyo hivi sasa Baraza la Manispaa limeanza utaratibu wa kufanya usafi nyakati za usiku, lakini pia wameweka utaratibu wa siku maalum ya kila mwezi ya kufanya usafi.

Mhe. Naibu Spika, kuhusiana na suala zima la mabadiliko ya tabia nchi. Kama walivyochangia Waheshimiwa wengi kuwa hivi sasa Zanzibar inakabiliwa na athari mbali mbali za mabadiliko ya tabia nchi. Baadhi ya athari hizo ni kilimo, uvuvi, maji safi, kupotea kwa *bayo anuai* na mmong'onyoko wa fukwe. Ni dhahiri kuwa athari hizo zinagusa maisha ya watu wa kila siku.

Athari za mabadiliko ya tabia nchi Zanzibar zinaongezeka kutokana na ukataji wa miti na mikoko ambayo hupunguza kasi ya kuingia kwa maji ya bahari. Mhe. Naibu Spika, ili kukabiliana vizuri na athari hizo ni wazi kuwa tunahitaji kuwa na mkakati madhubuti, na ndio maana ofisi yetu kwa kushirikiana na wadau, imeweka lengo la kuandaa mkakati huo ambao utatoa kipaumbele cha hatua zinazofaa kuchukuliwa.

Kuhusiana na kiwanda cha makonyo Mhe. Naibu Spika, kama tunavyofahamu kwamba Kiwanda cha Makonyo Pemba kimezaliwa zamani kabla ya kuzaliwa kwa Idara ya Mazingira. Kwa maana hiyo kiwanda hicho kimeanzishwa bila ya kufanyiwa tathmini ya afya za kimazingira, yaani *environmental impact essessment*. Hata hivyo mwaka 1995 kiwanda hicho kilifanyiwa ukaguzi mfupi wa mazingira na kupata suluhisho la kuongeza urefu wa sehemu ya kutolea moshi. Hali hiyo ilisaidia kwa kiasi fulani kupunguza athari za moshi zilizokuwepo. Ili kupata suluhisho la kudumu Ofisi yetu imewasiliana na Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko kwa ajili ya kufanya ukaguzi wa kikamilifu wa kimazingira ambao utaonesha mapungufu yote yaliyopo na hatua zinazofaa kuchukuliwa. Ukaguzi wa awali unategemewa kufanyika hivi karibuni ambapo pamoja na mambo mengine utatoa muongozo wa kufanywa kwa ukaguzi kamilifu wa kimazingira. Hivyo namuomba Mhe. Saleh Nassor Juma asubiri mpaka hapo ripoti kamili ya ukaguzi itakapokamilika. Matumaini yangu kwamba Wizara ya Biashara watawezesha ukaguzi huo ukamilike si zaidi ya miezi sita ijayo.

Mhe. Naibu Spika, sasa nazungumzia suala zima la masuala ya msumeno wa moto na ukataji wa miti na mikoko. Mhe. Naibu Spika, suala la kuwahimiza na kuwahamasisha wananchi kupanda miti halina mjadala na linapaswa kutekelezwa na kudumishwa. Mikutano, vipindi na programu mbali mbali zimekuwa zikitekelezwa kwa malengo mbali mbali yakiwemo ya kuhamasisha wananchi kuhifadhi na kutunza mazingira na hasa kwa kupanda miti. Ingawa Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais kupitia Idara ya Mazingira imekuwa ikitoa misaada midogo midogo kwa jamii kwa vikundi vinavyopanda miti sambamba na elimu kwa jamii juu ya hili, pia suala hili limekuwa likiongozwa na Wizara ya Kilimo na Maliasili, hivyo sina shaka eka zilizopandwa miti zitaendelezwa.

Mhe. Naibu Spika, kuhusu matumizi ya msumeno wa moto naomba niliache pia suala hili kwa kuwa litaelezwa kwa ufasaha zaidi na Wizara ya Kilimo na Maliasili wakati ikiwasilisha hotuba yake ya bajeti ya wizara kwa mwaka huu. Hata hivyo, kutokana na mashirikiano tuliyonayo naomba niseme kwa ufupi tu, kwamba serikali kupitia Wizara ya Kilimo na Maliasilia imeshaweka kanuni ya kudhibiti matumizi ya msumeno wa moto na hivi sasa inaendelea kutekelezwa, ingawaje jitihada na kuelimisha jamii nazo zinakwenda sambamba.

Mhe. Naibu Spika, naomba sasa nigusie masuala ambayo yamezungumzwa katika Idara ya Watu wenye Ulemavu. Hoja ya watu wenye ulemavu ilichangiwa na Waheshimiwa wote waliopata bahati ya kutoa michango yao na naomba kujibu hoja hizo kama ifuatavyo.

Hoja ya kwanza ilihusiana na ajira kwa watu wenye ulemavu. Hadi sasa Idara ya Watu wenye Ulemavu bado haijafanya utafiti kutambua idadi ya watu wenye ulemavu walio katika ajira katika taasisi mbalimbali za serikali. Hata hivyo, kupitia usajili uliofanywa tumeweza kutambua kuwa kuna watu ambao wana sifa za kuweza kuajiriwa. Kufuatia hali hii idara itafanya mawasiliano na wizara inayoshughulikia ajira ili kuona ni kwa namna gani watu hao wataweza kupata ajira.

Vile vile idara iliandaa ripoti fupi juu ya haja ya kupatiwa ajira watu wenye ulemavu na tayari imewasilishwa katika Wizara ya Nchi (OR) Utumishi wa Umma na Utawala Bora kama ilivyoagizwa na Kamati ya Usimamizi ya Ofisi ya Viongozi Wakuu wa Kitaifa. Tunaamini taarifa hiyo itasaidia serikali kuona umuhimu wa ajira kwa watu wenye ulemavu hasa kwa kutilia maanani sheria mpya ya utumishi ambayo inatoa kipaumbele kwa ajira kwa watu wenye ulemavu. Lakini napenda kueleza tu kwamba Idara ya Watu wenye Ulemavu yenyewe ina wafanyakazi wanane wenye ulemavu kati ya wafanyakazi 15 walioko Unguja na Pemba.

Hoja ya pili Mhe. Naibu Spika, ilikuwa ni ya usajili kwa watu wenye ulemavu. Napenda kuwaeleza Wajumbe kwamba Idara ya Watu wenye Ulemavu itaendelea na zoezi la usajili kwa upande wa Unguja katika bajeti ya mwaka 2012/13. Baada ya zoezi hilo kukamilika taarifa sahihi za watu wenye ulemavu pamoja na mahitaji yao zitakuwa zimepatikana.

Hoja nyengine Mhe. Naibu Spika, ni hoja ya kufikia majengo au maeneo mbali mbali kwa watu wenye ulemavu. Mhe. Naibu Spika, kama nilivyotangulia kusema katika hotuba yangu Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais kupitia Idara ya Watu wenye Ulemavu imeanzisha Maafisa Waratibu wa masuala ya watu wenye ulemavu katika taasisi mbali mbali za serikali. Ni matarajio yangu kwamba maafisa hawa watatumika katika kutambua mapengo yaliyopo katika sekta zao yakiwemo ufuatiliaji wa majengo, upataji wa mikopo, kesi za ubakaji pamoja na changamoto mbali mbali zinazowagusa watu wenye ulemavu. Aidha, programu mbali mbali zitazolenga katika kufanyia kazi changamoto zilizopo zitaandaliwa na kufanyiwa kazi. Natoa wito kwa viongozi kuwaunga mkono watendaji hawa ili kuleta mafanikio na kuhakikisha kwamba tunakuwa na jamii jumuishi.

Mhe. Naibu Spika, wazo lililotolewa na Mhe. Bikame Yussuf Hamad la kuwatafutia makazi maalum watu wenye ulemavu wasiojiweza napenda nitoe indhari kwamba huenda ikawa ni kinyume na Sheria ya Watu wenye Ulemavu ya Zanzibar pamoja na mikataba ya mataifa kwa kuona kwamba wanatengwa.

Mhe. Naibu Spika, naomba sasa kujibu hoja ambazo zimewasilishwa kupitia Tume ya Dawa za Kulevya. Kabla ya kujibu maswali ya Wajumbe ningependa kuliarifu Baraza lako tukufu kwamba Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais kupitia tume hii pamoja na mambo mengine ina jukumu la kuratibu harakati za udhibiti wa dawa za kulevya na taasisi mbali mbali za dola zilizopewa jukumu la utekelezaji wa Sheria ya Udhibiti na Usafirishaji wa Dawa za Kulevya Zanzibar. Hivyo basi, baadhi ya maswali yaliyoulizwa utekelezaji wake hufanywa na taasisi nyengine ambazo zimepewa majukumu hayo.

Mhe. Naibu Spika, naomba sasa uniruhusu niwataje Wajumbe ambao walichangia katika Tume hii ya Dawa za Kulevya. Mhe. Makame Mshimba Mbarouk, Mhe. Abdalla Juma Abdalla, Mhe. Amina Iddi Mabrouk, Mhe. Bikame Yussuf Hamad, Mhe. Ismail Jussa Ladhu, Mhe. Jaku Hashim Ayoub, Mhe. Suleiman Hemed, Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak, Mhe. Marina Joel Thomas na naomba sasa uniruhusu nitoe maelezo kwa wajumbe hawa kama ifuatavyo:

Napenda kuchukua nafasi hii kuungana na hoja ya Mwakilishi kwamba nadharia ya ulinzi shirikishi imesaidia kwa kiasi kikubwa katika kupunguza vitendo vya uhalifu ikiwemo matumizi ya dawa za kulevya katika baadhi ya maeneo. Kumekuwa na mifano hai na mizuri ya baadhi ya shehia hapa nchini ambazo zimekuwa mstari wa mbele katika kuchukua juhudi za makusudi za kutekeleza nadharia hiyo ya ulinzi shirikishi ikiwemo kukemea kutenda maovu katika maeneo yao, kupiga vita matumizi ya mihadharati na mengineyo. Juhudi hizo zinapaswa kupongezwa na kuigwa katika maeneo mengine.

Mhe. Naibu Spika, napenda nimhakikishie Mjumbe wako kwamba wazo la kuvitembelea vikundi vya ulinzi shirikishi tumelichukua. Aidha, napenda kumjuilisha Mjumbe pamoja na Wawakilishi kwa ujumla wa Baraza lako tukufu kwamba, ofisi yetu imo katika mchakato wa ukamilishaji wa mpango wa utekelezaji wa sheria ya dawa za kulevya ambao umetilia maanani kwa kiasi kikubwa ishiriki wa jamii katika vita dhidi ya dawa za kulevya. Naamini kukamilika kwa mchakato huo kutakuwa ni dira kwa taifa letu katika kukabiliana na vita hii ya mapambano dhidi ya dawa za kulevya hapa nchini kwetu.

Mhe. Naibu Spika, napenda nimjuilishe Mjumbe wa Baraza lako tukufu kwamba nia na azma ya serikali ya kuwa na kituo cha marekebisho ya tabia kwa watumiaji wa dawa za kulevya bado ipo palepale kama nilivyoeleza hapo awali katika uwasilishaji wa hotuba yangu. Hatua mbali mbali huko nyuma zilichukuliwa za kutafuta washirika wa maendeleo katika kufikia lengo hili ambazo hazikuzaa matunda.

Napenda kuwajuilisha wajumbe kwamba hatua za awali za ujenzi wa kituo hicho zinatazamiwa kuanza katika mwaka huu wa fedha huko Tunguu. Ujenzi wa kituo hicho umetiwa katika programu ya miradi ya maendeleo ambapo jumla ya shilingi 100,000,000/- zimetengwa kwa ajili ya shughuli za awali na kinategemea kuwahudumia wateja kati ya 50 na 80 kwa wakati mmoja.

Mhe. Naibu Spika, kabla sijamjibu Mjumbe naomba nichukue nafasi hii kueleza kwamba Shirika la Afya Duniani limetoa ufafanuzi wa kina juu ya matumizi tegemezi ya dawa za kulevya katika mnyambuliko wa magonjwa mbali mbali. Utegemezi wa dawa za kulevya ni ugonjwa unaohitaji mhusika kupatiwa huduma muwafaka za kimatibabu ikiwemo ushauri nasaha. Aidha, utegemezi sugu wa mihadharati huwa na sifa ya kujirejea rejea na hivyo tiba yake kuchukua muda mrefu.

Mhe. Naibu Spika, ni vyema tukaelewa kwamba vijana wanaotumia dawa za kulevya ni vijana wetu, vijana wa taifa letu, ni watoto wetu na ni watu wanaohitaji msaada kwa kujikwamua na tabia hiyo. Hawapaswi kutengwa na kwa kweli wanahitaji msaada wa kifamilia katika kupata huduma zinazostahili. Watumiaji wa dawa za kulevya huchukua sehemu kubwa kabisa ya maisha ya mtumiaji, dawa huwekwa maanani zaidi huku amali na shughuli nyengine za kijamii na za kimaendeleo zikipotea kabisa. Naamini sote tunayafahamu hayo.

Mhe. Naibu Spika, napenda kumjuilisha Mhe. Mwakilishi kwamba, katika hatua zilizochukuliwa na serikali katika kudhibiti hali hiyo ni kama zifuatazo:

Ofisi yetu lifanya juhudi za makusudi za kufanya mapitio ya Sheria ya Udhibiti wa Dawa za Kulevya ili kuleta ufanisi zaidi katika dhana nzima ya udhibiti wa dawa za kulevya. Mchakato unaoendelea hivi sasa wa uandaaji wa mpango wa utekelezaji wa sheria hiyo utakaowahusisha wadau mbali mbali zikiwemo taasisi za dola zilizo katika mapambano dhidi ya dawa za kulevya. Mpango huu utajikita katika suala zima la uendeshaji wa kesi za dawa za kulevya, upatikanaji wa vifaa kwa taasisi mbali mbali vinavyohusiana na udhibiti na taaluma vile vile.

Kumekuwa na juhudi mbali mbali kwa Kitengo cha Udhibiti wa Dawa za Kulevya cha Jeshi la Polisi katika ukamataji na uingizaji wa dawa za kulevya, ambapo katika kipindi cha mwaka 2011/12 hadi Mei, 2012, jumla ya watuhumiwa 148 wakiwemo wasambazaji na waingizaji wamekamatwa, wanaume wakiwa 140 na wanawake 8. Kumekuwa na changamoto katika udhibiti wa maeneo ya bandari zisizo rasmi hasa ukiangalia kwamba nchi yetu imezungukwa na bahari na kumekuwa na maeneo ya bandari hizo zaidi ya 500. Ofisi yetu inatoa wito kwa jamii ambazo zinaishi katika maeneo hayo kushirikiana na vyombo vya dola katika masuala mazima ya udhibiti wa dawa za kulevya kupitia ulinzishirikishi.

Napenda kulihakikishia Baraza lako tukufu kwamba ofisi yetu itafanya juhudi za makusudi kwamba choo ambacho kinatarajiwa kipo katika Uwanja wa Ndege kwa kushirikiana na Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais ambayo imebeba dhima ya kutoa fedha ya kumaliza choo hicho basi hivi karibuni mtasikia habari njema kwamba juhudi yetu imekamilika.

Ofisi ya Makamu wa Kwanza kwa kushirikiana na Wizara ya Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika inatarajia kuwa na mpango kwa watumiaji walioacha dawa katika programu ya ujasiriamali ili waweze kujikimu kimaisha.

Mhe. Naibu Spika, napenda kuungana na Mhe. Mwakilishi kwamba vitendo vya rushwa vimekuwa vikitajwa sana katika taasisi zilizo katika masuala ya udhibiti wa dawa za kulevya. Aidha, napenda kuchukua nafasi kuziomba taasisi zote zilizopewa majukumu kuwa waadilifu na kuzingatia maadili ya kazi yao.

Kuhusiana na *Sober House* ofisi yetu inatambua mchango wa taasisi ambazo si za kiserikali ambazo zimeanzisha *Sober House*. Kwa kuptia Tume ya Waratibu na Udhibiti wa Dawa za Kulevya ilizipatia jumla ya shilingi 9,900,000/- nyumba 9 za makaazi ya vijana wanaoacha matumizi ya dawa za kulevya Unguja na Pemba ambazo zimetumika katika malipo ya kodi ya nyumba, chakula na vifaa vidogo vidogo vya nyumbani. Aidha, ofisi yetu imetoa msaada wa vifaa vya electronic ikiwemo televisheni na redio kwa *Sober House* Unguja na Pemba. Mafunzo juu ya uongozi, utunzaji kumbukumbu na fedha yameweza kutolewa kwa viongozi wa makaazi hayo. Kwa kutambua umuhimu wa kuwa na uwiano mzuri wa huduma zenye kuleta ufanisi, ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais imetayarisha muongozo maalum kwa ajili ya makazi hayo.

Mhe. Naibu Spika, ofisi yetu itaendelea kuunga mkono juhudi hizo na napenda kutoa wito kwa taasisi nyengine mbali mbali na jamii kwa ujumla kuendelea kutoa msukumo na michango yao katika kuendeleza mbele harakati hizo.

Mhe. Naibu Spika, naomba sasa nizungumze hoja ambazo zimezungumzwa katika Tume ya UKIMWI. Wajumbe ambao wamechangia katika tume hii ni Mhe. Abdalla Juma, Mhe. Ismail Jussa Ladhu, Mhe. Bikame Yussuf Hamad, Mhe. Farida Amour, Mhe. Jaku Hashim Ayoub, Mhe. Ashura Sharif Ali, Mhe. Fatma Ali, Mhe. Mtumwa Kheir. Mhe. Abdalla Juma alitaka kujua kwa nini tume inajikita zaidi katika utoaji ushauri nasaha kwa makundi maalum baada ya kuwepo sheria ya kuweza kuwabana na kuwaadhibu.

Mhe. Naibu Spika, kutokana na haki za binadamu makundi haya ni sehemu ya binadamu na wana haki ya kupata huduma kama binadamu wengine. Vile vile makundi hayo ni miongoni mwetu kama sio sisi basi itakuwa ni ndugu zetu. Ushauri nasaha unaotolewa kwa makundi mbali mbali katika jamii ikiwa ni pamoja na makundi hatarishi ni kuweza kuwabadilisha kutoka katika makundi hayo na kuwa raia wema (kuachana na tabia hiyo). Mkazo mkubwa umewekwa katika makundi hayo kwa sababu imegundulika maambukizi makubwa yapo kwao kuliko makundi mengine. Vile vile rasimu ya sheria ya UKIMWI ipo tayari ambayo itaweza kutoa haki kwa mtu ambaye ataambukizwa virusi vya UKIMWI kwa makusudi.

Mhe. Bikame Yussuf alitaka kujua hali ya tathmini ya maambukizi ya UKIMWI kiwilaya. Takwimu hizo hupatiwa wadau wote ambazo zinaonesha hali ya maambukizi kwa taifa na kila wilaya ambazo zinachanganua kijinsia na kiumri.

Mhe. Naibu Spika, maelezo haya yanapatikana katika taarifa ya hali ya maambukizi ya UKIMWI kwa mwaka ambayo inaonesha hali ya maambukizi kati ya mwezi wa Julai, 2011 na Juni, 2012 ambavyo nimevisambaza kwa Wajumbe wa Baraza lako tukufu.

Mhe. Farida Amour alitaka kujua kama UKIMWI umepungua kwa kiasi gani Zanzibar. Mhe. Naibu Spika, kwa mujibu wa taarifa za utafiti juu ya UKIMWI na malaria Tanzania ambao umefanyika mwaka 2008 unaonesha kuwa maambukizi ya jamii kwa ujumla ni asilimia 0.6. Ila napenda kulitaarifu Baraza lako tukufu kwamba maambukizo hayo yamechangiwa na makundi maalum ambayo maambukizi yao yako juu zaidi. Wanawake wanaouza miili yao ni asilimia 10.8, wanaume wanaofanya mapenzi na wanaume wenzao asilimia 12.3 na wale wanaotumia madawa ya kulevya kwa kujidunga sindano asilimia 16. Vile vile takwimu zinaonesha kwamba kiwango cha maambukizi ni kikubwa kwa wanawake yaani asilimia 0.7 na kwa wanaume kidogo ni 0.5. Pia maambukizi ni makubwa kwa Unguja ambapo ni asilimia 0.8 na kwa Pemba ni asilimia 0.3.

Mhe. Naibu Spika, Mhe. Mtumwa Kheir alitaka kujua juu ya usambazaji wa kondom kwa makundi maalum na ni kwa ajili ya kinga au kuongeza UKIMWI. Mhe. Naibu Spika, suala la usambazaji wa kondom kwa makundi maalum limeonekana kuwa ni muhimu kwa ajili ya kukinga maambukizi kwa jamii, kwani makundi haya wateja wao ni miongoni mwa wanajamii. Kwa kufanya hivyo, tunazuia maambukizi kutokana na makundi hayo kuja katika jamii kwa ujumla.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu alitaka kujua mchanganuo wa matumizi ya fedha za mapambano ya UKIMWI katika mwaka 2011/2012. Mhe. Naibu Spika, fedha zilizoingizwa hazikidhi mahitaji ya mapambano dhidi ya UKIMWI kutokana na shughuli zinazotekelezwa na UKIMWI. Miongoni mwa shughuli hizo ni pamoja na kuratibu, kujenga uwezo wa wadau mbali mbali, kufuatilia na kutathmini pamoja na uandishi wa ripoti za kitaifa na kimataifa. Vile vile kazi kubwa ya kuweza kudhibiti maambukizi zaidi ya chini ya asilimia moja (0.6) katika jamii ambayo inahitaji kushirikisha makundi mbali mbali, kushawishi, kuelimisha na tafiti ambazo zinatuongoza katika kuchambua hali halisi na hivyo kupelekea kupanga mipango sahihi ya utekelezaji. Mchanganuo wa matumizi ya fedha kwa kipindi husika Mhe. Naibu Spika, nitampatia Mhe. Jussa.

Kwa upande wa *ZAPHA+* shilingi 15 milioni walizopewa ni kwa ajili ya bajeti ya serikali, lakini walipatiwa shilingi 47,500,000/- kwa shughuli zao nyengine, hizo ni fedha ambazo zilipitia tu tume lakini zilikwenda moja kwa moja kwa *ZAPHA+*. Lakini *ZAPHA+* kwa kipindi hicho wamepatiwa fedha kutoka kwa wahisani bila ya kupitia tume.

Mhe. Kazija Khamis Kona kwa vile mtu anayeishi na virusi vya UKIMWI huwezi kumjua kwa kumuangalia, je ofisi yangu anauliza imejipanga vipi kuzuia maambukizi mapya ya virusi hivi vya UKIWMI. Mhe. Naibu Spika, nakubaliana na mawazo ya Mjumbe kuwa mtu anayeishi na virusi vya UKIMWI huwezi kumjua kwa kumuangalia mpaka apime afya yake na suala la kupima afya kwa kweli ni la hiari. Kutokana na hilo Tume ya UKIMWI inaendelea kuhamasisha na kutoa elimu juu ya umuhimu wa kujikinga, kupima kwa kupitia wadau wa mapambano ya UKIMWI kuanzia ngazi ya shehia, wilaya, asasi za kiraia, asasi za kidini pamoja na viongozi wa wananchi yaani Wawakilishi.

Kutokana juhudi hiyo, muamko wa jamii umekuwa mkubwa na hasa ukiangalia katika suala zima la upimaji kabla ya ndoa na katika shughuli za kijamii na kitaifa kwama vile siku za maadhimisho ya Siku ya UKIMWI Duniani na katika shughuli mbalimbali, hata pia katika mikesha ya mwenge.

Mhe. Naibu Spika, naomba sasa nimalizie kwa kuzungumzia mambo mbali mbali ambayo yameguswa kutokana na Idara ya Utumishi. Suala lililoguswa hapa ni kutokana na tofauti ya mshahara kwa mwaka wa fedha 2011/12 na 2012/13. Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba kumshukuru Mhe. Ismail Jussa kwa kutoa mchango wake katika Idara hii ya Uendeshaji na Utumishi. Hii inatokana na mwaka wa fedha wa 2011/12 Idara ya Utumishi na Uendeshaji ilikuwa ndio idara ambayo inalipa mishahara ya idara tatu ambazo ni Idara ya Uendeshaji na Utumishi yenyewe, Idara ya Mipango, Sera na Utafiti na Ofisi ya Faragha zote za Unguja na kwa sasa kila idara imetengewa kasma yake katika bajeti zao kwa ajili ya kulipia mishahara na kuendeshea kazi.

Suala jengine Mhe. Naibu Spika, ambalo limeguswa hapa ni suala zima ambapo imeelekezwa juu ya ufafanuzi wa safari mbali mbali ambazo zimefanywa na viongozi na watendaji wa ofisi yetu. Hoja hii nayo pia iliulizwa na Mhe. Ismail Jussa na napenda kutoa maelezo yafuatayo:

Ofisi yetu inashughulikia masuala mtambuka ambapo masuala yote haya utekelezaji wake unakwenda sambamba na makubaliano yaliyoridhiwa na nchi yetu kwa kupitia mikataba ya kimataifa na kikanda. Kutokana na utaratibu uliopo kila baada ya muda nchi wanachama hupata nafasi ya kukutana. Aidha katika ngazi ya taifa, ngazi ya kikanda, ngazi ya kimataifa ili kujadili utekelezaji wa mambo ambayo yamekubaliwa. Aidha, makubaliano mbali mbali hufikiwa kupitia vikao hivyo, mchanganuo wa safari ambazo zimefanywa ni kama ifuatavyo na kopi Mheshimiwa tunaweza kumpatia.

Kulikuwa na safari ya Katibu Mkuu Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais kwenda Afrika ya Kusini ili kushiriki vikao juu ya masuala ya UKIMWI kwa watendaji wakuu. Masuala haya yalikuwa kwa nchi za Afrika na safari hii ilikuwa na mfadhili ilidhaminiwa lakini ofisi yetu ililipa nusu posho kama ilivyo taratibu za serikali.

Mhe. Waziri naye alikwenda China akifuatana na ujumbe wa mawaziri wengine katika juhudi nzima ya Serikali ya China kuwachukua mawaziri na kuwajengea uwezo na kuwaonesha jinsi gani wenzetu wameweza kupiga hatua za maendeleo, lakini pia kuyatembelea maeneo huru ili kuweza kutoa changamoto katika utekelezaji wetu. Ziara hiyo nayo ilidhaminiwa na China lakini vile vile ililipiwa nusu posho katika ofisi yetu.

Vile vile kulikuwa na ziara ya Naibu Katibu Mkuu Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais yeye alikwenda Ujerumani katika vikao ambavyo vinajulikana kwa jina la kitaalamu *Negotiation Team,* ambapo kabla ya mikutano mikubwa ya kimataifa kama mkutano wa mazingira au mkutano wa UKIMWI. Wataalamu kutoka nchi mbali mbali wanakutana kuanzia wiki tatu au mbili wakijadili maeneo mbali mbali. Katika vikao hivyo nchi nazo huzigawa. Kwa mfano, katika mkutano wa karibuni Tanzania ilikuwa katika kundi la nchi za Afrika ambayo ilikaa katika meza ya makubaliano kuweka msimamo wa pamoja na China pamoja na nchji za G77. Kwa hivyo huwa ni timu ambazo zinahitaji kwenda wajumbe wasikie.

Mhe. Naibu Spika, mara nyingi Baraza lako tukufu limekuwa linalalamika kwamba Zanzibar inaachwa nyuma katika masuala ya kimataifa na wenzetu kutoka Tanzania Bara ndio wanaohudhuria vikao hivi. Serikali imelitafakari hilo na imeona ipo haja Wazanzibari ikiwa kuna mkutano katika ngazi ya mawaziri kwa sasa mawaziri wawili wanakwenda kuiwakilisha Tanzania na katika safari nyengine Mhe. Naibu Spika, Zanzibar inapata nafasi katika ngazi ya waziri kuiwakilisha Tanzania kama nchi.

Safari nyengie pia ilikuwa ni ya Waziri, Naibu Katibu Mkuu na Mkurugenzi wa Mipango nchini Afrika ya Kusini kuhudhuria mkutano wa mazingira Durban. Lakini vile vile kulikuwa na safari moja ambayo ofisi ilihudumia nusu

tu kuhusiana na mafunzo mafupi juu ya usimamizi wa rasilimali watu. Hii ilikwendwa na Mkurugenzi Uendeshaji na Utumishi wa Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais. Lakini vile vile Mhe. Waziri alikwenda Spain pia kuhudhuria mikutano ambayo ni ya kimataifa.

Nilitakiwa pia nitoe maelezo nini *impact* ya safari hizi. Mhe. Naibu Spika, watendaji wanapata kushiriki katika mchakato mzima wa kufikia maamuzi ya kimataifa kama nilivyoeleza. Lakini pia wanaweza kuelewa fursa mbali mbali ambazo zipo katika kukabiliana na changamoto mfano za kimazingira au UKIMWI. Aidha, hupata nafasi ya kukutana na wadau mbali mbali wa kimataifa hivyo kurahisisha kupata misaada ya kifedha ama kitaaluma, lakini pia kupata nafasi ya kubadilishana mawazo na nchi nyengine ambazo changamoto zetu za kimazingira zinafanana. Mfano, Zanzibar kushiriki katika itifaki ya *Barbados Convention* kupitia mradi wa Ireland.

Zanzibar kuanza mkakati wa matumizi ya nishati safi, *Clean Development Mechanism* Zanzibar kuwa na mradi wa MKUHUME ni *out put* ya Copenhagen, kuhudhuria mikutano ya Copenhagen, *Africa Adaptation Program* ambayo hapa leo nimeizungumzia kwamba ilitupatia fedha kwa ajili ya mradi wa maji ya Nungwi, *Green Climate Fund* nayo pia ni fedha ambazo tunategemea kuzipata kwa ajili ya kusaidia kutunza mazingira. Lakini pia *Climate Change Impact Study out put* ya mkutano wa Windhoek Namibia. Hii imetusababishia kuweza kuanza kujipanga kiserikali katika ngazi ya kitaifa jinsi gani ya kuyashughulikia masuala mbali mbali ya mazingira.

Naomba nimtoe wasiwasi Mhe. Mwakilishi kwamba, kwa kweli katika ofisi yetu hata fedha ambayo unaiona imetengwa kama si msaada ambao tunaupata kutoka kwa wafadhili, *UNFCC* kwa suala la mazingira, *SMOLE* kwa suala la mazingira basi hizi safari zingekuwa ngumu sana. Kwa sababu unapobadilisha dola kwa shilingi ya Tanzania kwa kweli unaweza wewe mwenyewe ukapanga pale ukaona ni jinsi gani safari zinakuwa ni ghali sana.

Vile vile tunaishukuru wakati mwingi sana tunapata fursa kama mawaziri kuingia katika msafara wa viongozi wakuu ambao wanaiwakilisha nchi kwa hivyo gharama huwa hazibebwi na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Mhe. Naibu Spika, baada ya maelezo marefu sana naomba pia nitoe takwimu moja ambayo inahusiana na mradi wa kunguru ambayo iliulizwa. Waheshimiwa Wajumbe walikuwa wana wasiwasi juu ya shilingi 35 milioni, kwa kweli matumizi katika mradi wa kunguru kidogo yameleta kutokufahamika na kuona kuwa tayari asilimia 70 ya shilingi 35 milioni imetumika na kunguru 11,596 ndio wameuliwa. Sasa kwa fedha hizi mtego mmoja wa kunguru unagharimu shilingi laki nne na ishirini. Kwa hivyo, mitego 30 ni sawa na shilingi 12 milioni na laki sita, sumu ni sawa na shilingi 7,950,000/-. Gharama nyengine ni shilingi 14,450,000 kwa ajili ya ununuzi wa vifaa mbali mbali ambavyo nimevitaja ndani ya hotuba yangu. Shughuli hii inakuwa kama unaandaa harusi, unahitaji mabeseni na vitu vyengine vingi ili kuweza ku-*take care* sumu hii isiwafike wananchi.

Mhe. Naibu Spika, tunaposema thamani ya kunguru mmoja kuua ni shilingi elfu tatu kimahesabu haitokuwa sahihi, kwani mitego, sumu na vifaa vyengine vyote vitaendelea kuwepo. Kwa ujumla takwimu za kunguru waliouliwa ni kuanzia mwezi wa Aprili na Mei kwa sababu fedha zenyewe zilichelewa kuingizwa.

Aidha ninapenda kutoa taarifa kwamba kwa ujumla Unguja na Pemba kuna mtandao mmoja wa mazingira unaoitwa MTAMAZA, na jumuia za kiraia pia kuna kamati mbali mbali katika Shehia za Unguja na Pemba.

Mhe. Naibu Spika, kuna wajumbe wako ambao wamechangia wakati huu lakini naona muda umekimbia sana, naona mengi yao yanakubaliana na majibu ambayo nimeyatoa. Lakini kama kuna lolote jipya ambalo halihusiani na haya, sitoona taabu kuwapa majibu kama watahitajia.

Mhe. Naibu Spika, ninakushukuru sana na kuwashukuru sana Waheshimiwa Wajumbe kwa kunisikiliza. Sasa Mhe. Naibu Spika, naomba kutoa hoja.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

*(Hoja imeamuliwa na kuafikiwa)*

**Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais:** Mhe. Naibu Spika, kwa kuwa Baraza limejadili na kuikubali hotuba ya bajeti ya Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais, sasa naomba Baraza lako tukufu likae kama Kamati ya Matumizi ili kuvipitisha vifungu vya matumizi vya Wizara yangu.

**KAMATI YA MATUMIZI**

**FUNGU 06 OFISI YA MAKAMO WA KWANZA WA RAIS**

| | |
|---|---|
| Kifungu 0901 Idara ya Mazingira | shs.10,800,000/= |
| **Jumla ya Fungu** | **shs.10,800,000/=** |

*(Kifungu kilichotajwa hapo kimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

| | |
|---|---|
| Kifungu 0301 Ofisi Kuu Pemba | shs.316, 659,000/= |
| Kifungu 0401 Idara ya Mipango na Utafiti | shs |

**Mhe. Ismail Jussa Ladhu**: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwanza nimshukuru Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais kwa kujitahidi kutupa majibu ya hoja mbali mbali ambazo tuliziibua. Lakini jumla niliyoyazungumza kuna nukta moja sikuisikia kabisa.

Katika mchango wangu Mhe. Mwenyekiti, nilihoji juu ya Idara hii tu lakini nimeipigia buti Idara hii haidhuru inahusu Idara zote, vifungu vya posho maalum ambalo linaonekana lipo katika kila idara.

Mhe. Spika, sikupata majibu kabisa ya majibu ya hoja hii kwamba kwa sababu kuna *consolidation* ya mishahara na marupurupu, kwa nini fungu hili linaendelea kujitokeza kila pahala likiwa na fedha nyingi sana. Naomba maelezo yake Mhe. Mwenyekiti.

**Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais:** Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba kutoa ufafanuzi kuhusiana na posho maalum kama linavyoonekana katika kitabu kizima hiki kama anavyosema mwenyewe kama hivi ifuatavyo.

Mhe. Mwenyekiti, ninaamini kwamba posho hili lipo hapa kwa ajili ya wafanyakazi ambao wanahitajika kupewa posho maalum ambapo hivi karibuni Wizara ya Utumishi ya Umma imeamua, kuna baadhi ya madereva wa Waheshimiwa, masekreteri wa Waheshimiwa kuanzia Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais, Ofisi ya Faragha lakini pia katika Idara mbali mbali. Hawa wanalipwa posho. Ninaamini posho hizi ni hizo.

**Mhe. Ismail Jussa Ladhu:** Mhe. Mwenyekiti, nataka nitamke wazi kabisa kwamba siridhiki kabisa na maelezo yaliyotolewa. Siamini mimi labda nikitoa mifano nitaeleweka kwamba malipo ya posho maalum ya dereva yafikie katika shilingi thamanini milioni, wengine ishirini milioni na yapo kila Idara kama alivyosema.

Lakini zaidi Mhe. Mwenyekiti, kuna mifano tunaelewa hapa sio pahala pa kujadili hivi sasa, lakini kuna mifano tunaelewa kuwa kuna baadhi ya madereva wamefuatilia wameambiwa hakuna posho tena, mfano walinzi katika Wizara ya Fedha hakuna posho tena kwa sababu zote zimeingizwa kwenye mishahara.

Kwa hivyo ninasema maelezo yanayotolewa ni ya ubabaishaji zaidi Mhe. Mwenyekiti. Jana swali hili liliulizwa katika Ofisi ya Makamo wa Pili kuhusu matengenezo ya magari, mara tukaambiwa masuala ya ZSSF, leo tunapata maelezo mengine kuwa posho hizi ni za madereva na masekereteri wa viongozi.

Sasa ninajiuliza Mhe. Mwenyekiti, kwamba fedha hizi kwa wingi sana ambazo zipo kila Idara tuelezwe hasa nini *breakdown*, analipwa nani kwa sababu hivi sasa mishahara ipo katika *consolidation*, na hata hao wakubwa katika serikali wote huduma zao zote za msingi na marupurupu yao, maslahi na stahiki zao zimeingizwa kwenye mishahara yao. Kwa nini kuna fungu kubwa kama hili. Tutolee wasi wasi kwamba fedha hizi haziwekwi hapa na wakubwa ili kutumika kwa mambo wanayoyajua wao. Naomba tena Mhe. Mwenyekiti.

**Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Utumishi wa Umma na Utawala Bora:** Mhe. Mwenyekiti, naomba nitoe majibu ya nyongeza kutokana na suali la Mhe. Jussa ambalo ameliuliza katika mchango wake na Mhe. Waziri ametoa ufafanuzi, na mimi ninataka niongeze kutoa ufafanuzi juu ya posho hizi.

Ni kweli kwanza serikali imeamua kutoa posho maalum kwa baadhi ya watumishi hasa madereva, masekreteri pamoja na watu wanaofanya kazi katika maeneo ya kutunza kumbukumbu, yaani masjala za siri.

Posho hizi hazipo kwenye mshahara, yaani hazikuwekwa-consolidated ya mshahara, zimeekwa kama posho maalum na zipo katika *other charges* na sio kwenye fungu la mishahara.

Matumizi yoyote yale ambayo yanapangwa katika taasisi kwa uelewa wangu ni kwamba yanatumika stakabadhi maalum kwa watu ambao wakati ule wapo katika ile taasisi na ambao wanatumika katika zile nafasi ambazo zimepangwa.

Na sio lazima kwamba pesa hizi zote zitumike katika eneo hili. Kwa hivyo mimi ninamuomba Mhe. Jussa akubaliane na hili kwa sababu hizi hazimo katika fungu la mishahara, zimo katika fungu la *other charges* kwa ajili ya kulipa hizi posho, na kwa nini zimeekwa kwenye vifungu hivi.

Kwa sababu huyu dereva wa Waziri anaweza kesho asiwe dereva wa waziri. Maana yake kule atakapokwenda hatokwenda na posho hili badala yake yule atakayekuja ndiye atakayelipwa posho hili, sekreteri halikadhalika na wale watumishi wengine katika nafasi hii.

Nimuombe tu Mhe. Jussa aamini kwamba hizi posho ziliopo zimetengwa kwa madhumuni hayo. Ahsante sana.

**Mhe. Ismail Jussa Ladhu**: Mhe. Mwenyekiti, kwa heshima zote na taadhima bado ninatofautiana na Waheshimiwa Mawaziri kwa jumla na maelezo yao.

Mhe. Mwenyekiti, hawa wasaidizi kama hawa dereva au sekreteri wa Waziri au Mkurugenzi anaweza kuwa ni mmoja au wawili. Posho wanalolipwa pengine ni shilingi laki moja.

Lakini labda ili nieleweke hoja yangu ni kwamba nilichoeleza hapa lakini kinahusu kila Wizara. Chukua kwa mfano Idara hiyo ya Mipango, Sera na Utafiti, ukienda katika fungu la posho maalum kuna shilingi milioni kumi na tano, lakini ninasena ni *figure* tu.

Ukienda katika Idara ya Utumishi na Uendeshaji kuna shilingi milioni mia moja na saba kama posho maalum, kwenye Ofisi ya Faragha kuna shilingi milioni thamanini na nne posho maalum na kwengine ambapo sitaki kupoteza muda wako Mhe. Mwenyekiti.

Kwa hivyo ninachosema mara ya tatu hii, wala nisiitie hofu serikali, sikusudii kupigisha kura juu ya suala hili lakini ninachosema tu Mhe. Mwenyekiti, maelezo juu ya fungu hili la posho maalum yanaonekana hayapo tangu jana.

Kwa hivyo ninaruhusu tuendelee kwa sababu gani Mheshimiwa, tunayakusanya yote haya tunakuja kutaka jawabu kwa Wizara ya Fedha, kama hakuna jawabu za masuala haya Mhe. Mwenyekiti, wakati huo ukifika nitawaomba Waheshimiwa Wajumbe wenzangu katika hili tukubaliane kwamba fedha hizi hazina maelezo. Kwa sasa tuendelee Mhe. Mwenyekiti.

**Jumla ya Fungu** **shs.176, 251,000/=**

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

Kifungu 0601 Idara ya Dawa za Kulevya

**Mhe. Ismail Jussa Ladhu:** Mhe Mwenyekiti, kwanza hapa nimshukuru Mhe. Waziri kwamba hoja nyingi ambazo tumekuwa tumezitoa zimepata majibu. Nilikuwa naomba maelezo juu ya hoja mbili tu ambazo sikuzisikia kabisa katika ufafanuzi wake.

Kwanza nilitaka *specific committement* ya Mhe. Waziri katika Idara hii kiasi gani kitakwenda kwenye *sober houses*. Mwaka jana Mhe. Mwenyekiti, nililisimamia papatu zikapatikana shilingi milioni tisa. Kwa hivyo, ninasema tukilinganisha kama nilivyosema tutakapokuja kwenye Tume ya Ukimwi tutaona kwamba fedha zinazokwenda katika shughuli kama hizi tunataka kuona kuna fedha ambazo kwa wale wahusika hasa wenyewe.

Hivyo ninataka *committement* yenyewe ni kiasi gani katika hizi kitakwenda kusaidia *sober houses* kwenye fungu hili la Idara ya Dawa za Kulevya, ambapo kwa jumla fungu hili lina shilingi mia mbili na ishirini na saba milioni, ninataka niambiwe katika hizi ni ngapi zinakwenda kusaidia kwenye *sober houses* lakini ya pili niunganishe kabisa Mhe. Mwenyekiti, ili nisimsimamishe sana.

Niliuliza kwamba suala la kufungwa choo kile cha ku-flash dawa za kulevya. Nikasema kwamba ofisi mbili katika majibu yake hapa ya Makamo wa Kwanza na Makamo wa Pili, zote ni ofisi za Serikali ya Mapinduzi moja hii, kwa nini kuna mvutano baina yao mpaka suala hili linachukua mpaka leo choo hicho hakijafungwa, kiasi wale waliotupa msaada wamefika pahala kutuona kama vile hatuna haja ya kusaidiwa. Nilikuwa naomba maelezo Mhe. Mwenyekiti.

**Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais:** Ninakushukuru Mhe. Mwenyekiti, naomba kujibu hoja za Mhe. Ismail Jussa Ladhu kama ifuatavyo.

Katika mwaka wa fedha wa 2012/13 Tume ya Uratibu na Kudhibiti Dawa za Kulevya katika bajeti yake imetenga jumla ya shilingi milioni kumi na tano kwenda kwenye *sober houses.*

Kuhusiana na kufungwa choo, mimi ninataka Mhe. Jussa aniachie hili suala na ninafikiri kipindi kifupi tutampa jibu, kwa sababu dhamana hasa kwanza ilikuwa ya Jeshi la Polisi. Hata ufungwaji wa choo chenyewe katika ile hatua iliyofika Mhe. Hamza hayupo hivi sasa lakini yeye ni shahidi kwamba Ofisi ya Waziri Kiongozi ndiyo iliyosaidia alau kikafungwa.

Sasa tunachoona kwamba commitment ipo ndogo kwa Jeshi la Polisi, lakini sisi kupitia Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais, jana nilieleza wameshapelekewa barua walete *assessment* na Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais itatoa fedha hizo ili choo hicho kifungwe haraka iwezekanavyo.

Kwa kusema kweli Mhe. Makamo wa Pili amefanya mawasiliano na Kamishna wa Polisi na tayari ameshampatia *assessment*, kwa hivyo shughuli hii karibu itakamilika.

**Mhe. Ismail Jussa Ladhu:** Mhe. Mwenyekiti, tuendelee.

| | |
|---|---|
| Jumla ya Kifungu | shs.247, 091,000/= |

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

| | |
|---|---|
| Kifungu 0901 Idara ya Mazingira | shs.399, 669,000/= |
| Kifungu 2101 Idara ya Watu Wenye Ulemavu | shs.532, 532,000/= |
| Kifungu 2102 Idara ya Faragha | **shs.511, 324,000/=** |
| **Jumla ya Fungu** | **shs.2, 770,000,000/=** |

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

**TUME YA UKIMWI ZANZIBAR**

Kifungu 0201 Utawala Unguja

**Mhe. Ismail Jussa Ladhu:** Mhe. Mwenyekiti, ninashukuru kwa kunipa fursa kwa mara nyengine tena.
Mhe. Mwenyekiti, nilipokuwa nikitoa mchango wangu nilieleza nia ya kuondoa shilingi katika bajeti ya Tume ya Ukimwi, kwa sababu kama nilivyosema siridhiki na *priorities* na matumizi ya fedha ambazo zinaingizwa katika

Tume hii. Na nikasema Mhe. Mwenyekiti, kuna-*tendency* ya kudhani kwamba fedha zikitoka nchi za wahisani wa ushirika wa maendeleo kama hizi hazina mwenyewe, hivyo zinaweza kutafunwa tu kadri tunavyopenda.

Mhe. Mwenyekiti, ukiangalia matumizi yake sehemu kubwa sana fedha hizi zinaelekezwa katika utawala, kujengeana uwezo, kujenga ofisi, semina, makongamano, warsha na mikutano. Lakini kile kifungu ambacho kinakwenda kwa wahusika wenyewe ni kidogo.

Nilisema hapa kwenye hotuba ya Mhe. Waziri ndipo nilipotoa maelezo kwamba *ZAPH+* imepangiwa shilingi milioni kumi na tano, hatukutajiwa maeneo mengine yamekuja katika maelezo ya Mhe. Waziri.

Sasa nitoe mfano Mhe. Mwenyekiti, ili nipate hoja yangu kueleweka naomba maelezo zaidi.

Katika bajeti ya mwaka huu Mhe. Mwenyekiti, nikichanganya fedha za *recurrent* za maendeleo za Tume ya Ukimwi zinafika jumla ya shilingi bilioni moja mia sita thamanini milioni laki saba na sitini elfu, hizi ni fedha nyingi sana Mhe. Mwenyekiti. Lakini katika fungu kama hilo ukute jumuia ambayo ya kuwasaidia watu hawa kupata vyakula vizuri, kuweza dawa za kurefusha maisha wanapangiwa shilingi milioni kumi na tano ambapo hata haijafikia asilimia mbili au tatu ya fedha, hata asimilia moja sijui kama inafika.

Kwa hivyo Mhe. Mwenyekiti, nilikuwa anieleze hasa anitosheleze, kwa nini niliruhusu fungu hili ikiwa priorities zake ni mambo haya ya utawala kuliko kwenda kuwahudumia waathirika wa Ukimwi na kukabiliana kweli na Ukimwi katika nchi yetu. Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti.

**Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais:** Ninakushukuru sana Mhe. Mwenyekiti, naomba nitoe maelezo kama hivi ifuatavyo.

Tume ya Ukimwi Zanzibar ina majukumu tofauti na taasisi nyengine nyingi ambazo sisi tunazifahamu ambazo nyingi zao huwa zinafanya vitu vinavyoonekana au kukamatika. Shughuli nyingi za Tume hii tumezieleza ni kuratibu, kutoa elimu, kutayarisha Ripoti na shughuli nyengine zinazofanana na hizo.

Hata hivyo naomba nimuhakikishie Ndugu yangu Mhe. Jussa kwamba, ni agizo la serikali kwamba fedha zinazotengwa kwenye bajeti ya taasisi yoyote ioneshe *priorityies* zake katika maeneo ambayo ndio *core functions* za taasisi hiyo.
Nataka nimuhakikishie kwamba nitalisimamia fungu hili na kuhakikisha kwamba tutakapokuja hapa mwakani ataona maeneo fedha hizi zimeelekezwa katika shughuli ambazo ndio hasa shughuli ambazo taasisi hii ya Tume ya Ukimwi inapaswa kuzifanya, lakini pia kuweza kuwafikia kama anavyosema waathirika wa gonjwa hili la ukimwi kwa namna ambavyo hali itaruhusu.

**Mhe. Ismail Jussa Ladhu:** Ninakushukuru Mhe. Mwenyekiti, malengo ninamuelewa sana Mhe. Waziri na ninataka nieleweke nikisema sina nia kabisa ya kusema kwamba Ofisi ya Waziri au Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais yenyewe kuwa yenyewe ndio inayohusika na masuala haya, kwa sababu wao ndio wasimamizi wa fedha hizi, wao ndio wanaowajibika ndani ya Baraza hili.

Shughuli Mhe. Mwenyekiti, zimetajwa hata ukitazama kwenye ukurasa wa 38 katika malengo ya mwaka huu wa fedha, yametajwa na ukitazama haya Tume ya Ukimwi ndio hayo ninayozungumza mimi zaidi ni mambo ya kiutawala na semina na mambo mengine.

Sasa Mhe. Mwenyekiti, sitaki kupoteza muda wa Baraza. Katika maelezo ya jumla aliyotueleza Mhe. Waziri mapema alisema kwamba programu hizi zinahusu na mambo mengine na kuandika ripoti, na katuletea ripoti tuzione. Lakini Mhe. Mwenyekiti, hizi ripoti ni za kiingereza hata hazikusudiwi sisi wasomaji wa Kiswahili.

Hizi zinaandaliwa maalum kwa kwenda kuwafurahisha hao wanaotoa fedha zao huko, kwamba fedha zinatumika vile inavyopaswa. Mimi Mhe. Mwenyekiti, nina-*doubt* kakaa Mzanzibari kaziandika hizi lakini huko sitaki kuingia. Kwa sababu ya kuheshimu ofisi hii na jana nilisema ninaheshimu sana Ofisi ya Makamo wa Kwanza, ninakubali tuendelee lakini Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri ametoa *commitment* kwamba atazifuatilia, na ninaomba na Baraza hili kwa sababu Kanuni zetu zimeipa madaraka Kamati ya PAC, mbali ya ripoti ya CAG kuchunguza fedha mahususi, ninawaomba PAC na Baraza hili liridhie kwamba waende wakafanye ukaguzi wa kina kwa fedha

zinazotumika katika Tume ya Ukimwi kama kweli zinatumika ipasavyo. Baada ya hapo Mhe. Mwenyekiti, ninasema tuendelee.

**Mhe. Asha Bakari Makame:** Mhe. Mwenyekiti, na mimi nilitoa maelezo kuhusu habari ya Kitengo hiki cha Ukimwi na maelezo mengi tu ingawa sikupata majibu. Lakini kwa sababu kajibu kwa pamoja Mhe. Waziri sawa, na mimi kwenye huu ukurasa wa 38 ninaungana na Mjumbe ambaye amepita hivi sasa.

Hivyo kweli shilingi bilioni hii moja *point something* ni kuratibu mambo haya matano? Mbona hamna kuwasaidia wale waathirika wa Ukimwi na anatwambia nini. Mhe. Mwenyekiti, atawasaidiaje ukiacha kuwapa taaluma na nini, lakini na wale wanahitaji kugaiwa chochote kujiendeshea maisha yao kuwawekea kitu ambacho kitawaendeshea maisha yao.

Naomba Mhe. Waziri anipe ufafanuzi kidogo.

**Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais:** Mhe. Mwenyekiti, ni kweli dada yangu Mhe. Asha Bakari alikuwa na mchango wake mkubwa, na niliomba radhi pale kutokana na wakati kutokana na michangio hii iliyokuja kama sikumridhisha mtu anisimamishe.

Ni bahati mbaya sana huu mchanganuo ambao tumeutoa haujamfika yeye akaona jinsi gani fedha zimegaiwa. Kwa kweli ni nia ya serikali ikiwezekana kuwasaidia watu hawa ambao wanaathirika na ukimwi. Lakini kwa kweli tatizo ni kubwa sana.

Katika hawa wanaoathirika wako ambao wanaishi na virusi, wapo watoto ambao wameachwa na ni mayatima ambao pia wameachwa na virusi. Kwa hivi sasa kwa utaratibu wa mila na silka zetu za Kizanzibari, watoto hawa wanaendelea kuishi katika *extended family* na kutunzwa na familia hizo.

Kwa kweli kama serikali iweze kubeba mzigo mkubwa ambao tunao ndani ya jamii ya watu wote ambao wameathirika kwa njia moja au nyengine na gonjwa la ukimwi, nina mashaka sana kwamba hata bajeti ya serikali itatushinda.

Hata hivyo, Mhe. Mwenyekiti, mimi ninapenda nimuhakikishie dada yangu kwamba tutakaa katika ofisi tuone ni jinsi gani na kwa kiasi gani kwa sababu tayari tunafanya, tunazisaidia taasisi ambazo zinahusika moja kwa moja juu ya kutoa huduma na kudhibiti gonjwa la ukimwi.

Lakini kama tutaweza kwenda mbele tuweze kuangalia jinsi gani tutaweza kusonga mbele. Kwa kweli uwezo bado ni mdogo. Ukitaja shilingi bilioni moja au mbili, unaweza kwa ghafla ukaona ni pesa nyingi. Lakini ukikusanya na *demand* iliopo kwa watu wanaoishi na ukimwi lakini pia wale walioathirika ambao wameachiwa familia ambazo hazina wazazi, kwa kweli mzigo huu ni mzito sana kwa serikali kuweza kuubeba.

Lakini ofisi yangu itaangalia kila uwezekano kuona hata kidogo kidogo kwa jinsi gani tutaweza kupenya kuwasaidia wale waathirika ambao tunahisi wanahitaji msaada wa dharura. Ninakushukuru Mhe. Mwenyekiti.

**Mhe. Asha Bakari Makame:** Mhe Mwenyekiti, namshukuru sana Mhe. Waziri kwa maelezo yake mazuri sana, lakini bado nitaiomba Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais. Kwa sababu hawa hawana mategemeo, mategemeo yao ni madogo. Kwa hivyo, naomba tuwakusanye kama vikundi, ili kuweza kuwasaidia katika zile sehemu tuwakusanye kama vikundi vya ushirika waweze kuendesha maisha yao. Lakini tukisema pesa zote tunazifanyia masemina na mambo mengine. Hawa ndio waathirika wenyewe, tuwape haki yao kwa kuwakusanya kwa pamoja vikundi, na kuna Wizara mbali mbali mtasaidiana. Baada ya kusema hayo Mhe. Mwenyekiti, naomba tuendelee.

| | | |
|---|---|---|
| | Jumla ya kifungu | 554,042,000 |
| Kifungu 0301 | Ofisi Kuu Pemba | 184,958,000 |
| | Jumla ya Fungu | 739,000,000 |

**FUNGU 06 – OFISI YA MAKAMO WA KWANZA WA RAIS**

Kifungu 0401 Idara ya Mipango Sera na Utafiti 1,496,052,000

Jumla ya Fungu

**UTARATIBU**

**Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais:** Mhe. Mwenyekiti, nina wasi wasi sana Baraza lako lisije kupitisha fungu ambalo silo. Katika ukurasa huu umefanyiwa marekebisho na sijui kama Waheshimiwa Wajumbe wamepewa.

Kifungu 0401 Idara ya Mipango Sera na Utafiti 960,600,000

**Mhe. Hija Hassan Hija:** Mhe. Mwenyekiti, nataka tupate muongozo wako ili baadae Baraza lisije likapotoka, kwa sababu kitu ambacho mnakipitisha ni mikononi mwa meza na wazee yaani makatibu mezani, lakini Waheshimiwa Wajumbe hawana taarifa hiyo. Kwa hivyo, naomba utusaidie muongozo ili angalau tujue ni shilingi ngapi na ilikuwaje.

**Mhe. Mwenyekiti:** Waheshimiwa Wajumbe, mabadiliko ya marekebisho ya vifungu hivi yaligaiwa. Au alikuwa nayo peke yake Waziri.

Waheshimiwa Wajumbe, yuko Mjumbe ambaye anayo marekebisho haya. Mawaziri. Tunamuomba Mhe. Waziri atoe maelezo, anasema kuna mradi umepunguzwa.

**Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais:** Nakushukuru Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa nafasi ya kutoa ufafanuzi ili kuwaondosha wasi wasi Wajumbe wako.

Ukurasa uliopo katika kitabu ambacho wanacho, kwenye ukurasa wa 694 kuna fedha katika Fungu 750043. Mmeliona hilo fungu. Fungu limeandikwa ‘uimarishaji na usambazaji wa maji katika kijiji cha Nungwi, yaani *Improvement of Nungwi Water Supply.*

Mhe. Mwenyekiti, mradi huu niliueleza katika kitabu changu kwamba huu umekamilika, na kwa mwaka huu hatuna hizi fedha, hizi fedha tulishazipata na mradi umekamilika. Kwa hivyo, ofisi yangu baada ya kuona ukurasa huu haukukaa sawa, basi tuliwasiliana na Wizara ya Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo ambao wao wenyewe ndio waliotoa marekebisho haya, na kwa taarifa niliyonayo ni kwamba barua imekuja kwa Mhe. Spika, na marekebisho haya yamewasilishwa rasmi.

**Mhe. Mwenyekiti:** Waheshimiwa Wajumbe, mmeridhika na maelezo ya Mhe. Waziri.

**Mhe. Hija Hassan Hija:** Mhe. Mwenyekiti, kwa sababu nilitoa hoja mimi na baada ya ufafanuzi na ili tuweke sawa Hansard, basi tuendelee na Wajumbe wamefahamu.

Jumla ya Kifungu 960,600,000

Jumla ya Fungu 960,600,000

**FUNGU 12 – TUME YA UKIMWI**

Kifungu 0201 Utawala Unguja 943,760,000

Jumla ya Fungu 943,760,000

*(Baraza lilirudia)*

**Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais:** Mhe. Naibu Spika, ilivyokuwa kamati ya matumizi imejadili na kupitisha makadirio ya fedha ya Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais, pamoja na mabadiliko. Sasa naomba kutoa hoja kwamba Baraza lako liyakubali. Naomba kutoa hoja.

**Mhe. Naibu Spika:** Waheshimiwa Wajumbe, sasa niwahoji wale waliokubali hotuba ya Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais, kuhusu makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka wa fedha 2012/2013 wanyooshe mikono. Waliokataa. Waliokubali wameshinda. *(Makofi).*

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

*(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)*

**Mhe. Naibu Spika:** Waheshimiwa Wajumbe, ahsanteni sana. Kwanza tunampongeza Mhe. Waziri. Vile vile nawapongeza Wajumbe wote kwa kazi nzuri tuliyoifanya tangu jana ilipoanza kusomwa hotuba hii na leo tumemaliza hivi jioni.

Kwa hivyo, kwa kuwa kazi tumemaliza, naomba kuahirisha Baraza hili mpaka kesho siku ya Ijumaa ya tarehe 29/06/2012, saa 3:00 za asubuhi.

*(Saa 1:35 usiku Baraza liliakhirishwa mpaka*
*tarehe 29/06/2012 saa 3:00 za asubuhi)*